BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR 2016 - 2020

1.	**Mhe.**	**Zubeir Ali Maulid**	**-**	**SPIKA**
2.	**Mhe.**	**Mgeni Hassan Juma**	**-**	**Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake**
3.	**Mhe.**	**Shehe Hamad Mattar**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni**
4.	**Mhe.**	**Mwanaasha Khamis Juma**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani**
5.	**Mhe.**	**Balozi Seif Ali Iddi**	**-**	**MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda**
6.	**Mhe.**	**Issa Haji Ussi Gavu**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka**
7.	**Mhe.**	**Haji Omar Kheri**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu**
8.	**Mhe.**	**Haroun Ali Suleiman**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi**

9.	**Mhe. Mohammed Aboud Mohammed**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais**
10.	**Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge**
11.	**Mhe. Mahmoud Thabit Kombo**	**-**	**MBM/Waziri wa Habari, Utalii,**
			na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki
12.	**Mhe. Riziki Pembe Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake**
13.	**Mhe. Balozi Amina Salum Ali**	**-**	**MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda / Uteuzi wa Rais**
14.	**Mhe. Balozi Ali Abeid Karume**	**-**	**MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais**
15.	**Mhe. Rashid Ali Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani**
16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake**
19.	**Mhe. Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi,**

			Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
20.	**Mhe. Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
21.	**Mhe. Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe. Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera**
24.	**Mhe. Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni**
25.	**Mhe. Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe. Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe. Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake**

29.	**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Uwezeshaji,**	**-**	**Naibu Waziri wa Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe. Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**
31.	**Mhe. Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini**
32.	**Mhe. Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara, na Viwanda /Jimbo la Welezo**
33.	**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo**
34.	**Mhe. Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe. Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
36.	**Mhe. Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
37.	**Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
38.	**Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
39.	**Mhe. Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
40.	**Mhe. Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
41.	**Mhe. Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
42.	**Mhe. Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
43.	**Mhe. Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
44.	**Mhe. Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
45.	**Mhe. Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
46.	**Mhe. Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
47.	**Mhe. Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
48.	**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**

49.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
50.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
51.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
52.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
53.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
54.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
55.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
56.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
57.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
58.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
59.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
61.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
62.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
63.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
64.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
66.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
67.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
68.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
69.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
70.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
71.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
72.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
73.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
74.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
75.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
77.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
78.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
80.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
81.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
82.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

83.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
85.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
86.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
	Ndg.	**Raya Issa Msellem**	**-**	**Katibu**

Kikao cha Thalathini – Tarehe 26 Juni, 2018

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mtakumbuka kuwa katika Kikao cha Kumi na Moja cha Mkutano wa Kumi wa Baraza hili la Tisa kilichofanyika tarehe 23/05/2018, Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto aliwasilisha Hotuba ya Bajeti yake kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Waheshimiwa wajumbe, katika Hotuba ya Bajeti hiyo Mheshimiwa Waziri alitoa Takwimu ambazo zilionekana kutofautiana na takwimu zilizotolewa wakati wa hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango ilipokuwa inawasilishwa.

Sasa namuomba Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto atoe maelezo ili kuweka sawa takwimu hizo. Ahsanteni. Mheshimiwa Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika**,** kwa heshima napenda kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Wakati nikiwasilisha hotuba ya bajeti ya wizara yangu, nilitoa taarifa iliyoonyesha idadi ya mikopo itakayotolewa ni mia sita (600). Hata hivyo, taarifa hiyo imeonekana kuwa tofauti na taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango alipokuwa akitoa ufafanuzi wa bajeti yake katika kikao cha Ishirini na Sita cha Mkutano wa Kumi wa Baraza hili uliofanyika mnamo tarehe 13/06/2018 ambapo alieleza idadi ya mikopo hiyo kuwa ni mia tano (500).

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa taarifa hii katika Baraza letu na kuweka sawa kumbukumbu zetu kuwa marekebisho yamefanyika na usahihi ni kuwa idadi ya mikopo hiyo ni 600 na siyo 500 ambayo ilitajwa kimakosa. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naomba tu niwataarifu kwamba swali Nam. 267 Mhe. Jaku Hashim Ayoub ameliondoa kwa hiyo tutaendelea na swali linalofuata.

Nam. 267

Ongezeko la Nyumba za Ibada Tunguu

(Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 276

Idadi ya Kesi za Serikali Walizoshitaki na Kushitakiwa

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny. Mhe. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:

Kwa mujibu wa sheria za nchi yetu serikali inaweza kushitaki na kushitakiwa mahakamani.

(a) Je, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita serikali imeshitaki kesi ngapi na kesi ngapi imeshitakiwa.

(b) Je, katika kipindi hicho kesi ngapi serikali imeshinda na ngapi imeshindwa au kusuluhishwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 276 lenye vifungu (a) na (b) kwanza naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwa mujibu wa sheria Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaweza kushtaki au kushtakiwa. Upo utaratibu maalum wa kushtaki au kushtakiwa kwa serikali. Kwa mujibu wa kifungu cha 6(2) cha sheria ya mwenendo wa madai ya serikali namba 3 ya 2010, mtu yeyote anaetaka kuishtaki serikali lazima atoe indhari ya kuonesha nia ya kuishtaki serikali ndani ya siku sitini kabla hajafunga shauri lake Mahakamani. Indhari hiyo itumwe kwa Katibu Mkuu Kiongozi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Baada ya siku sitini kumalizika na hakuna hatua yoyote serikali iliyoichukua dhidi ya tuhuma zilizoelezwa ndani ya indhari hiyo basi hakuna budi mtu huyo anaweza kuishtaki serikali.

Mhe. Naibu Spika, Aidha, kifungu cha 10 cha sheria hiyo kimempa mamlaka Mwanasheria Mkuu kushtaki au kushtakiwa katika kesi zote dhidi au kusimama kwa niaba ya serikali. Hivyo, kutokana na sheria hiyo ya mwenendo wa madai ya serikali namba 3 ya 2010 napenda kusisitiza kwamba serikali inaweza kushtaki au kushtakiwa na mtu yoyote au taasisi yoyote au kikundi cha watu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita kuanzia mwezi April 2013 hadi Mei 2018, Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar ilisimamia jumla ya kesi za madai 170. Kati ya hizo, kesi 25 zilifunguliwa na serikali yaani serikali ilishtaki na kesi 145 zilifunguliwa dhidi ya serikali yaani serikali ilishtakiwa katika ngazi za Mahakama tofauti za Unguja, Pemba na Tanzania Bara.

(b) Mhe. Naibu Spika, katika kipindi hicho jumla ya kesi 89 zilimalizika. Kati ya hizo kesi 63 serikali ilishinda, kesi 14 serikali ilishindwa na kesi 12 zilisuluhishwa. Nashukuru.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyogeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niipongeze Wizara au Serikali kwa kuhakikisha kwamba zinapopelekwa kesi za serikali kuwa zinashinda na kwa upande mwengine inaposhitakiwa serikali huwa panatokea changamoto ambao pia tunakuwa kwa asilimia kubwa.

(a) Je kwa kuwa mambo haya yanaendelea katika nchi yetu Unguja na Pemba Wizara imejipanga vipi kuhakikisha kuwaimarisha Wanasheria wetu na Mahakimu wetu ili wawe na uwezo zaidi wakuondoa matatizo haya ambayo yanajitokeza hasa inaposhitakiwa serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Serikali imekuwa mara kwa mara inatoa mafunzo kwa Wanasheria wakiwemo Mahakimu na Wanasheria wengine ambao wamo Mawizarani. Kwa hivyo serikali tunafanya jitihada ya kuwapa mafunzo zaidi ili kujiweka vizuri zaidi katika kazi zao za kila siku.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuweza kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora napenda kumuuliza kwamba ni sababu zipi zilizopelekea serikali kushindwa kesi na wakati inawataalamu na inaajiri wataalamu wa kutosha.

(b) Ni kiasi gani serikali imelipa kwa kesi ambazo Jamhuri imeshindwa. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Yussuf Hassan Iddi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jawabu langu la msingi kuna baadhi ya kesi serikali imeshinda na baadhi ya kesi serikali imeshindwa sasa Mhe. Yussuf Hassan Iddi alitaka kujua kwanini serikali inakuwa inashindwa.

Mhe. Naibu Spika, kuna sababu mbali mbali ambapo serikali huwa inapoteza kesi lakini miongoni mwa sababu hizo sababu ya kwanza ni shahidi au mashahidi pale ambapo kutakuwa na kesi na mashahidi wakawa hawendi Mahakamani, hawendi kutowa ushahidi Mahakamni basi hii ni sababu ya msingi kuwa wakati mwengine serikali inapoteza kesi kwa sababu hatukupata ushirikiano mzuri na mashahidi.

Lakini Mhe. Naibu Spika, swali la pili ni ushahidi namna ushahidi unavyotolewa Mahakamani na yule shahidi inawezekana shahidi ni mzuri tu na amekuwa na mambo mengi ambayo anaelewa katika kutoa ule ushahidi, lakini shahidi wenyewe namna atakavyotowa ushahidi wake Mahakamani ku-*convince* yaani kushawishi Mahakama nalo vile vile linakuwa tatizo wakati mwengine. Kwa hivyo namna ya shahidi anavyotoa ushahidi Mahakamani wakati mwengine inakuwa tatizo na inapelekea kwamba Hakimu au Jaji kutoridhika au kutoshawishika na ule ushahidi ambao mashahidi ambao wanatowa Mahakamani hii ni sababu ya pili.

Lakini Mhe. Naibu Spika, sababu nyengine utaratibu wakati mwengine utaratibu huwa unakosewa sasa utaratibu ukikosewa hapa vile vile inaweza ikawa pia serikali ikaweza kutoshinda hiyo kesi. Kwa hivyo kuna sababu nyingi kama nilivyoeleza awali lakini hizo ndio sababu za msingi ambazo serikali huwa inashindwa kesi, kwa hivyo nitowe wito wangu kwa wale watendaji wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanaposhughulikia haya masuala ya kesi basi ni vyema wakaendeleza umakini zaidi, naelewa ni makini, naelewa kwamba ni makini lakini wakaendeleza umakini zaidi ili kutupelekea serikali kushinda hizi kesi na badala yake tuweze kushinda kesi zote.

(b) Mhe. Naibu Spika, Mhe. Yussuf Hassan Iddi aliuliza alitaka kujuwa idadi ya kesi, kwa hivyo hili niseme kwamba sasa hivi sina idadi hiyo halisi ya kesi ambazo alizoulizia Mhe. Yussuf Hassan Iddi kwa hivyo nimwambie wache niende nikafanye utafiti zaidi kuja kumpa hizo *data* za kutosha ili niwe na uhakika zaidi juu ya hili. Nashukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nami kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza kabla sijauliza swali naomba kwamba nimpongeze sana Mhe**.** Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa majibu yake mazuri na ya ufasaha ambayo ameyatowa katika swali hili.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika Mahakama nyingi miongoni mwa Mahakama hizo

ikiwemo Konde inakosa maeneo maalum kwa ajili ya watu wanaokwenda kusikiliza kesi ama mashahidi, hasa katika kipindi ambacho kunaweza kukatokezea masuala ya mvua wanashindwa watu wale kupata eneo wakaweza kukaaa ili kusubiri kesi zao na kuweza kusikiliza na badala yake huhangaika kwenda maeneo ili na hata ikifika wakati wakutafutwa labda mtu atafutwe fulani yuko wapi kesi yake ina maana inashindwa kuweza kumpata. Je kuna utaratibu gani ambao mtaufanya kwa baadhi ya Mahakama hizo ambazo zinakosa maeneo hayo kuweza kurejesha ili wananchi wale wanapokwenda kusikiliza kesi waweze kupata huduma hiyo ikiwemo na vyoo. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakar swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, nadhani sote ni mashahidi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kufanya jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba Mahakama zetu zinakuwa na mazingira mazuri Unguja na Pemba nadhani Mhe. Ali Khamis Bakar nawe pia shahidi Mahakama yetu ya Chake Chake tayari imeshafanya marekebisho, huu ni mfano tu lakini kuna Mahakama nyingi ambazo tunaendelea kuzifanyia marekebisho ikiwemo Mahakama ya Mwanakwerekwe.

Sasa Mahakama ya Konde ni kweli eneo wanapokuwepo wale wanaosikiliza kesi ni dogo lakini tuelewe kwamba serikali itaendela na jitihada zake za kufanya marekebisho katika Mahakama mbali mbali ikiwemo hiyo ya Konde na ukizingatia kwamba Mahakama ya konde kuna kiwanja pale Mhe. Ali Khamis Bakari kwa hivyo ni habari njema tu pale ambapo Inshaallah tutakapokuwa tayari basi tunaweza *either* kufanya marekebisho zaidi katika Mahakama ile ile au mambo yatakapokuwa mazuri kwa maana mfuko wa fedha utakapokuwa mzuri zaidi basi tunaweza tukajenga Mahakama nyengine katika eneo lile la Konde. Nashukuru.

Nam. 53

Vifaa vya Maabara vya Kufundishia

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:

Pamoja na Wizara ya Elimu kuwa na bajeti ya mwaka mzima wa fedha, kumekuwa na tatizo la upungufu wa maabara na vifaa vya kufundishia kwenye skuli mbali mbali jambo ambalo huleta changamoto kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi kwani vifaa vichache hupatikana muda mfupi kabla ya wanafunzi kufanya mtihani wa taifa wa kidato cha nne.

(a) Je, wizara ina mpango wa kupeleka vifaa vya maabara katika maskuli kabla ya kuanza kwa mtihani wa mock unaofanyika mwezi Mei, ambao huwa ndio kipimo halisi cha mwanafunzi huyo.

(b) Je, wizara ina mkakati gani wa kuzifanya maabara hizo ziwe "sc*i*ence *lab*" badala ya hizi sasa ambazo nyingi zao ni "*science room*" kutokana na kutofikia kiwango cha kuwa na "*laboratory*".

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu mhe. mwakilishi swali lake Nam. 53 lenye vifungu (a) na (b) kwanza naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa wizara inatenga fedha katika bajeti zake kila mwaka kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maabara na madawa kwa ajili ya ufundishaji wa masomo ya sayansi kwa vitendo. Vifaa hivyo hununuliwa na kusambazwa katika skuli zote zinazohusika mara mbili. Matumizi ya vifaa hivyo yanaweza kuchukua kipindi kirefu kutegemea na matumizi na uhifadhi wake. Katika mwaka 2017/2018, wizara imetumia jumla ya shilingi milioni mia tano na sitini (560,000,000/=) kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maabara na vifaa vyengine vya kufundishia na kusambazwa katika skuli zote za sekondari.

Baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid kama ifuatavyo:-

(a) Wizara yangu imenunua na kuvisambaza vifaa vya maabara katika skuli zote. Vifaa vilivyosambazwa maskuli ni kwa ajili ya wanafunzi kufanya mazoezi ya matumizi ya vifaa hivyo na pia kwa ajili ya kufanyia mitihani yote ikiwemo mtihani wa *mock* na mitihani ya taifa ya kidato cha nne au cha sita. Wizara imehakikisha kuwa hakuna skuli ya sekondari iliyokuwa haina vifaa vya maabara.

(b) Ni kweli kuwa Wizar ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina changamoto ya uhaba wa maabara zilizofikia viwango katika baadhi ya skuli za sekondari, hata hivyo, juhudi mbali mbali zinafanyika katika ujenzi na ukarabati wa maabara kwa kadri hali ya fedha inavyoruhusu. Katika mwaka 2017/2018, wizara inakamilisha ujenzi wa maabara katika Skuli za Miwani na Gamba kwa Unguja na pia imefanya matengenezo na ununuzi wa samani ya maabara ya Skuli ya Sekondari ya Chokocho kwa Pemba.

Aidha, kupitia mradi wa Uimarishaji wa elimu ya lazima ambao ni mkopo kutoka Benki ya Dunia, Wizara itafanya ujenzi wa maabara za kisasa katika skuli 25 za sekondari Unguja na Pemba. Maabara hizo zitakapokamilika zitatoa fursa kwa walimu na wanafunzi wa skuli jirani kuzitumia kwa kufanya mazoezi ya vitendo. Aidha, skuli mpya za sekondari 11 ambazo ujenzi wake unaendelea kwa mashirikiano na mfuko wa *OPEC*, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) na Mfanyabiashara Bwana Salim Said Bakhressa zote zitakuwa na maabara za kisasa. Pia utanuzi wa Skuli ya Sekondari ya Biashara, Mombasa unaofadhiliwa na Kampuni ya *SHA* nayo itakuwa na maabara za kisasa. Hivyo Wizara inafanya juhudi kubwa za kuhakikisha kuwa skuli za sekondari zinakuwa na maabara zinazokidhi viwango, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Swali la mwanzo la nyongeza, Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Omar Seif: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa ruhusa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Pamoja na majibu marefu ya Mhe. Waziri aliyoyaleta, napenda nimuulize na kabla ya hapo naomba niseme kwa sababu mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya skuli. Changamoto hizi nilizokuwa nazizungumza nimeziona mwenyewe nikiwa Mwenyekiti wa kamati ya skuli, na leo unasema Mhe. Waziri kwamba hakuna skuli ambayo haina upungufu wa vifaa vya maabara. Lakini mimi nilitaka nijue je, umehakikisha vipi kwamba kweli hakuna skuli ambayo haina upungufu wa vifaa vya maabara.

Kwa sababu bado katika skuli yangu ya Konde ninavyokwambia wewe umekwenda na mimi nimekwenda na skuli pale vifaa vya maabara ni vichache mno na wewe umesema hakuna , umehakikisha vipi kwamba hakuna la kwanza. Lakini la pili umesema kwamba kuna skuli ishirini na tano ambazo zitajengwa na zitakuwa na maabara za kisasa. Sasa hizi skuli zilizokuwa zinajengwa zenye maabara za kisasa ni kidogo lakini kwa uwezo wetu ndiyo tulizo nazo, utahakikisha vipi kwamba zile skuli za jirani zote kutakuwa na uwezo wa kuweza kuzihudumia ili wanafunzi wetu wapate kujifunza kwa vitendo katika hizo skuli za maabara ambazo ziko jirani na pale, ili watoto wetu na wazazi waondokane na yale malalamiko kwamba tumekwenda skuli sisi tumekosa vifaa vya maabara. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Omar Seif Abeid maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Katika jibu letu la msingi nimeeleza kwamba vifaa hivi huwa tunavigawa mara mbili kwa mwaka, na tunavigawa kwa matumizi ya aina mbili kwanza matumizi ya vitendo kwa ajili ya wanafunzi na pili kwa ajili ya kufanyia mitihani ya taifa ikiwemo na huu mtihani wa MOKO. Sasa tunachosema hapa na tunachosisitiza ni kwamba hakuna skuli ambayo haina vifaa ni tofauti kusema kwamba vinatosheleza nasema hakuna skuli ambayo haina vifaa. Na baada ya kuona kwamba baadhi ya skuli vifaa hivi vipo vya kutosha na havitumiki. Tumefanya utafiti huo tukagundua na baadhi ya skuli kuna upungufu sasa ule upungufu huwa unakuwa *covered* kwa njia nyingine mbali mbali, kwa mfano kuanzia mwaka huu tunatarajia kwamba skuli hizi zitaondokana na upungufu mkubwa wa vifaa vya maabara kutokana na matumizi ya fedha ambazo zimewekwa katika kila skuli ambazo tunaita *school brand*, hizi pamoja na matumizi mengine lakini pia ununuzi wa vifaa vya sayansi utakuwa umezingatiwa pamoja na juhudi nyingine ya wizara kuongeza bajeti yake ya ununuzi wa vifaa vya sayansi.

Maabara za kisasa zitakapo kamilika, tumejiandaa na tumepanga mikakati kwamba skuli za jirani na maabara hizo zitafaidika kwa sababu skuli hizi zitakuwa na vifaa vya kutosha lakini pia wanaweza kutumia utaalamu uliopo katika skuli ile lakini pia wanaweza kutumia walimu wao kwenda kufanya mazoezi ya vitendo na utaratibu huu umeanza hivi sasa upo, baadhi ya skuli ambazo hazina vifaa vya kutosha au hawana wataalamu wa kutosha wanahamia katika maabara ya skuli nyingine hivi sasa unaendelea mpango huu

tunaita ujirani mwema baina ya skuli "a" na "b" ambao wanabadilishana baadhi ya vifaa na hata walimu katika kusomesha. Ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda kuungana nanyi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma mwenye kurehemu, aliyeumba mbingu na ardhi na vilivyomo vyote, na kumtakia kheri Mtume wetu Muhammad SAW.

Mhe. Naibu Spika, nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini nina swali la nyongeza lenye (a) na (b).

(a) Kwa kuwa mitihani iko pande mbili baina ya *theory* na *practical* katika mambo ya sayansi, lakini tunafahamu kwamba mtoto utakavyomsomesha ndivyo atakavyokuja kujibu mitihani na walimu tunao tofauti pamoja na skuli ziko tofauti. Nataka kumuuliza Waziri, haoni sasa kama alivyosema mwenyewe kwamba kuna ujirani mwema wa skuli, haoni sasa kuna umuhimu wa kuzigawa hizi skuli ikawa skuli za sayansi wanafunzi wanapata elimu moja ili kwamba hapa ukiingia kwenye skuli hii ni skuli ya sayansi ambayo kuna vifaa vilivyotimia na walimu waliotimia ili wale wanafunzi waweze kukidhi haja ya kuweza kujibu mitihani yao ya sayansi kuliko kuwabagua na kuwa kila mmoja anakwenda katika skuli yake na mwalimu tofauti wakati mtoto ndiyo anakuwa anaumizwa kichwa. Kwa hivyo je haoni Waziri kuna haja ya kuwakusanya sasa kuzibagua skuli za sayansi na skuli za *Art* ziwe tofauti swali hili ni la kwanza.

(b) Sasa hivi kuna mpango mwengine umeletwa wa walimu wetu kutoka Nigeria wamekuja kutusaidia katika suala la sayansi, je mitaala yao ya Nigeria ya kisayansi na mitaala yetu ya kitanzania ya kisayansi inalingana ili wale walimu wanapotoa zile taaluma zao wanafunzi wawe rahisi kujibu mitihani yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Katika utaratibu wa sasa tulionao Wizara ya Elimu, tumeanza utaratibu tuna michepuo na katika michepuo hiyo tunayo michepuo ya sayansi ambayo wanafunzi wanaoingia katika michepuo hiyo wanasomeshwa masomo ya sayansi na walimu wenye sifa. Lakini hatujaenea sehemu zote za Unguja na Pemba lakini mchepuo umeanza na unaendelea. Na siyo huo peke yake lakini pia tunayo michepuo mingine ya Kiarabu, tunayo michepuo mingine ya *Art* na kadhalika. Kwa hivyo utararibu huu upo, lakini haujenda katika kiwango kikubwa sana. Sasa baadhi ya sekondari nyingine wamechanganywa wanafunzi wao humo humo wamo wa *Art* na wamo wa sayansi lakini katika michepuo tumeweza kutenganisha suala hili.

Kuhusu Walimu wa Nigeria na walimu wengine wote duniani kuna mambo ya msingi katika masomo ya sayansi yanafanana *physics* ya Nigeria, Marekani na kadhalika inafanana, kwa hivyo tofauti inaweza kuwa kidogo katika *methodology* labda na falsafa yenyewe ya elimu. Kwa hivyo hakuna tatizo lolote na si Nigeria tu hata mimi

nikipelekwa sehemu nyingine yoyote duniani nisomeshe somo fulani nafanya na nimeshafanya hivyo, nilipelekwa kusomesha Korea kule nilikwenda kusomesha bila ya tatizo lolote. Kwa sababu ile elimu inafanana kabisa. Ahsante.

Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, nampongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa kueleza mipango mizuri ya skuli zetu zote kuwa na maabara. Swali je wizara ina mipango gani katika hizi maabara kuzifanya ziwe na *reagents* au na *chemicals* kwa sababu nyingi ya maabara kwa kweli zipo kama maabara lakini hawafanyi mazoezi ya vitendo kwa sababu hakuna *chemicals* na *reagents* je wizara ina mipango gani kulifanya suala hili liwe endelevu. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ni kwamba hili swali lina pande mbili, upande mmoja ni kwamba upungufu wa vifaa lakini upande wa pili ni zile *attitude* za walimu wenyewe. Sasa kwetu sisi Wizara ya Elimu, sehemu zote mbili tutajaribu kuziangalia vya kutosha kwamba walimu wawe tayari kutumia vile vifaa vilivyopo katika skuli kwa ajili ya kusomesha wanafunzi wetu kwa vitendo. Lakini kuhusu vifaaa na *reagents* nyengine zote ni kwamba bajeti ya Wizara ya Elimu na hasa mwaka huu imeongezeka zaidi kwa ajili ya kununua vifaa vya maabara na vinginevyo.

Lakini pia nimesema *school grants* kwa kiasi kikubwa itatumika katika kununua vifaa vikiwemo vya sayansi, hiyo ni baadhi ya mipango na mipango mingine zaidi inaendelea kupitia miradi mingine mbali mbali. Ahsante sana.

Nam. 227

Magari yanayobeba Wanafunzi wa Skuli Binafsi

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:-

Skuli binafsi, mara nyingi hutumia magari ya aina mbali mbali kwa ajili ya kuwasafirisha wanafunzi wa skuli zao. Lakini kwa masikitiko makubwa, baadhi yao huchukuwa wanafunzi wengi, na kusababisha msongomano wa wanafunzi katika gari hizo. Kwa kuwa tatizo hilo ni hatari kwa wanafunzi hao.

Je, Wizara ina mpango gani wa kulinda usalama wa wanafunzi hao.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Ali Suleiman Ali, Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele swali lake Nam. 227 kama hivi ifuatavyo: -

Wizara yangu inatambua kuwa baadhi ya magari ya skuli binafsi yanayopakia wanafunzi yanajaza kupita kiasi jambo ambalo linaweza kuhatarisha usalama wa wanafunzi hao.

Wizara yangu imekuwa ikilikemea suala hili katika mikutano mbali mbali iliyofanyika na skuli za binafsi au viongozi wa umoja wa Skuli binafsi. Pia Wizara imeliwasilisha suala hili kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mjini Magharibi na kumtaka Askari wa usalama barabarani wawachukulie hatua za kisheria wenye magari wote watakaobainika wanakiuka taratibu za usalama barabarani. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Swali la mwanzo la nyongeza Mhe. Ali Suleiman Ali.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, gari zinazochukua wanafunzi mara nyingi huwa watoto wa kuanzia miaka mitatu na kuendelea, lakini mara nyingi watoto wale huwa umri wao hausimamiwi vizuri na askari wa usalama barabarani na kwa kuwa kunakuwa na mbinyano katika harakati zao, pamoja na Mhe. Waziri kutujibu tu kwamba wamezungumza na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi ili kunusuru hilo je, zaidi anatoa rai gani au Wizara inatoa rai gani au wito gani kwa wenye magari na maskuli hayo kuondoa tatizo hilo na kunusuru vijana wetu wasije wakapotea katika misingi inayoweza kuzuilika.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu swali lake Mhe. Ali Suleiman Ali kama ifuatavyo:-

Ni kwamba kama tulivyosema kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kazi yake kimsingi ni kutoa elimu na katika kutoa elimu na ili elimu iwe ya manufaa lazima anaepewa elimu hiyo apate mwamko na akipata mwamko anajitambua akijitambua anaamua akiamua anajua lipi sahihi na lipi si sahihi. Kwa hivyo Wizara ya Elimu itaendelea kuwaelimisha na kuwakumbusha kila siku wamiliki wa skuli hizi na tunafanya mikutano hii mingi kabisa tumefanya Pemba, tumefanya Unguja na tunaendelea mara kwa mara na tunategemea wakati mwingine tunapofanya uchunguzi wa haraka haraka tunakuta kidogo kuna unafuu fulani. Lakini pia kwa upande mwingine tukaziarifu taasisi zinazohusika na masuala ya usalama barabarani kwa mfano tarehe 24 April, 2018 tumemuandikia barua rasmi Kamanda wa Polisi Mjini Magharibi na nakala zikenda kwa Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magaharibi, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya ya Magharibi A na B ili kusaidiana tunakwenda ili kusaidiana katika suala hili. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Swali la pili la nyongeza Mhe. Shehe Hamad Mattar.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika kwa kunipa fursa hii. Namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yako mazuri, lakini Mhe. Waziri nikuulize kwa sababu jambo hili linaendelea hadi leo kupakiwa watoto kama mizigo ya mitumba ndani ya magari je uko tayari tukuletee namba za gari ambazo zinafanya hivyo na skuli ambayo inafanya hivyo ichukuliwe hatua. Kama Polisi wameshindwa kuchukua hatua wewe uko tayari tukuletee nambari za gari ambazo kuwa wanafanya utaratibu na utaweza kuchukua hatua gani.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar swali lake kama ifuatavyo:- Nadhani njia sahihi kama ni raia mwema unaripoti katika vituo vya polisi, lakini kama imeshindikana basi sisi Wizara tuko tayari kuzipokea nambari hizo na tuwasilishe. Ahsante sana.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika kwa kuniona na kunipa fursa hii, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri pamoja na majibu yake mazuri sana naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Mheshimiwa magari haya sio yanatumiwa na skuli binafsi tu hata skuli za serikali huwa zinatumia hasa pale wanafunzi wanapofanya ziara mbali mbali kutembelea.

Je Wizara yako ina mpango gani kuwaonya walimu na madereva wale wanaopakia wanafunzi ili isije ikatokea hasara katika wanafunzi wetu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu swali lake la yongeza Mhe. Shaib Said Ali wa Jimbo la Chonga kama ifuatavyo:-

Tunachosema ni kwamba katika sheria hakuna mtu ambae yuko juu ya sheria hakuna, kwa hivyo hata hao walimu wanapopakia wanafunzi katika ziara zao mbali mbali na wao pia wakizidisha vyombo vya Ulinzi na Usalama vichukue hatua yake. Ahsante sana.

Nam. 192

Mikopo katika Gharama za Uchumaji Karafuu

Mhe. Asha Abdalla Mussa - Aliuliza:-

Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) huwa linatoa mikopo katika gharama za awali za uchumaji karafuu.

a) Je, mikopo hiyo inaendelea sambamba na matarajio ya Shirika.

b) Je, iwapo mkulima atachelewa kurejesha mkopo kuna hatua gani zinazochukuliwa kudhibiti uchelewaji.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Asha Abdalla Mussa Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa swali lake Nam. 192 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika kumrahisishia mkulima hatua za mwanzo za uchumaji wa Karafuu, shirika limekuwa likitenga fedha kwa ajili ya kuwakopesha wakulima waliokidhi vigezo vya kukopeshwa na Shirika. Hadi sasa mikopo hiyo inaenda sambamba na

matarajio ya Shirika kwani wakulima wengi wameonesha uaminifu wa kukopa na kurejesha fedha kwa wakati.

(b) Miongoni mwa masharti yaliomo kwenye mikataba wa ukopeshwaji Mkulima hutakiwa kuwa na Mdhamini ambaye ni mfanyakazi wa Serikali ambaye yeye atakuwa na wajibu wa kulipa pale ambapo mkulima hatotimiza masharti ya mkataba ya kulipa kwa wakati. Aidha, mkulima atatakiwa kuwa na dhamana ya mali isiyohamishika ambayo hati ya umiliki wa mali hiyo huzuiwa na Shirika hadi mkulima atakapokamilisha kulipa mkopo wake. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, katika majibu ya Mhe. Waziri amesema kwamba wakulima wengi wameonesha uaminifu wa kukopa na kurejesha mikopo hiyo kwa wakati.

(a) Je, nataka kujua kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imetolewa mikopo mingapi na yenye thamani ya kiasi gani.

(b) Mpaka sasa imerejeshwa mikopo mingapi. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa minong'ono imezidi naomba tusikilizane humu ndani.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza napenda kuchukua fursa hii ya kuwapongeza wananchi wakulima wa zao la karafuu kwa kuonesha uaminifu mkubwa pale ambapo tunawakopesha pesa za kulimia karafuu na kuzirejesha kwa wakati na kwa uamini, wakulima wa karafuu msimu uliopita tumewakopesha Shs. Milioni 298 na mpaka hii leo wakulima wamesharejesha Shs. Milioni 279 na kilichobakia ni milioni 18.

Mhe. Naibu Spika, kwa mantiki hiyo nachukua fursa hii ya kuwapongeza wakulima wa karafuu na waendelee na moyo huo huo kwa kuonesha uaminifu mkubwa kukopeshwa na kurejesha kwa wakati kama ilivyotakiwa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spikan na nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake na suala la kumuliza Mhe. Waziri.

a) Kwa kuwa wakulima wetu hawa tunawakopesha kwa ajili ya kutuvunia zao la taifa, lakini je tunapowakopesha tunawatilia na riba, na ikiwa tunawatilia riba ni asilimia ngapi.

b) Kama riba ipo hatuoni kwamba tunawaongezea mzigo watu hawa wakati wanaokoa pato la taifa.

Mhe.Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu a na b kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, Mheshimiwa anauliza je kuna riba katika mkopo ambao tunautoa. Mheshimiwa aina ya mkopo tunaoutoa ni mkopo nafuu ambao hauna riba kwa sababu wakulima wetu tunawapenda na tunawataka wakaliokoe zao letu la taifa la karafuu, ili karafuu iendelee kuwa na soko na hadhi ile ile ya karafuu ya Zanzibar huko duniani.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri katika majibu yako umesema kwamba wakulima hawa wanatakiwa kupata wadhamini hususan wale wanaofanya kazi serikalini ili kuliendeleza zao hili la karafuu ili waweze kupata mkopo huo. Lakini wakulima wengi wanapata tabu kupata wadhamini hawa kwa sababu huyo mdhamini mwenyewe siku nyengine huko benki ana deni la miaka kumi au kumi na tano anajenga nyumba.

Je, huoni kwamba ipo haja ya kuwapunguzia gharama hizi au ukaweka mpango mwengine wa kuweza kunufaika na mikopo hii wakulima wetu ili waendeleze mashamba yao na kupata zao letu la karafuu kuliendeleza uchumi katika Zanzibar yetu hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu kama ifuatavyo.

Mheshimiwa tunachokizungumza hapa ni mkopo wa wakulima wetu mkopo nafuu, kunako masuala yote ya pesa duniani inapozungumziwa mikopo lazima uwe kitu kinachoitwa Security lazima hicho uwe nacho, sasa kwa sisi kwa sababu wakulima wetu tunawapenda tunawaambia usitafute mambo makubwa tuletee mdhamini mfanyakazi wa Serikali. Mheshimiwa naomba kumhakikishia kwa hili imekuwa si shida kwa wakulima wetu kwa sababu ndio maana wakaweza kurejesha mikopo yetu kwa wakati, imekuwa si shida tumewakopesha Milioni 298 washarejesha Milioni 279 kilichobakia ni milioni 18 huo ni ushahidi tosha wa kwamba wakulima wetu wamekuwa hawapati shida katika kukopa na kulipa mikopo yetu.

Nam. 256

Mauzo ya Zao la Karafuu Zanzibar Kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Mhe. Mussa Foum Mussa – Aliuliza:

Katika mwaka 2016/2017 kwa upande wa mauzo ya karafuu Shirika liliuza jumla ya tano 2,156 zenye thamani ya U$D 16.67 millioni sana ta Tsh. 36.0 billioni hadi tarehe 31/3/2017.

(a) Je, Shirika la *ZSTC* kwa mwaka 2017/2018 limeuza kiasi gani.

(b) Je, Shirika limepata faida kiasi gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 256 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Hadi kufikia tarehe 30/03/2018 Shirika limeuza karafuu tani 7,838 zenye thamani ya TZS. 138.9 Bilioni.

(b) Kwa vile msimu wa karafuu unamalizika rasmi mwezi wa Juni 2018 na kwa vile Shirika bado lina Karafuu ghalani, faida itakayopatikana na Shirika itajulikana baada ya kuuzwa kwa Karafuu zote na kutoa gharama zinazohusiana na Karafuu pamoja na uendeshaji. Hata hivyo, Shirika linategemea kupata faida kutokana na mauzo ya Karafuu.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba muulize suala moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wakulima wengi wa Unguja na Pemba wameuza karafuu zao katika Shirika la ZSTC na Serikali kwa mwaka huu imenunua karafuu nyingi, lakini kwa kuwa kuna baadhi ya wananchi bado wanaendeleza suala la magendo kuzisafirisha karafuu nje ya nchi.

Je, kwa mwaka huu ni tani ngapi zilizokamatwa zilizokuwa zinasafirishwa magendo?

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kumhakikishia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya kazi kubwa na inaendelea kufanya kazi kubwa katika kuzinusuru karafuu zetu zisifanyiwe magendo, mimi mwenyewe ni shahidi na wewe ni shahidi tumekwenda Pemba tumeona ulinzi mkali tuliouweka kila pahali katika kuhakikisha karafuu zetu hazifanyiwi magendo. Kwa mwaka huu zimekamatwa gunia kumi (10) kule Tanga za magendo uone juhudi na jukumu la Serikali katika kunusuru magendo.

Mheshimiwa nikwambie kweli hakuna sababu tena ya magendo kwa sababu walikuwa wanauza magendo watu kwa sababu ya kupata bei, sasa hivi karafuu zina bei nzuri Zanzibar kuliko huko zinakopelekwa magendo kuna sababu gani ya magendo, hizi gunia kumi ni wale wakora tu watu wanaotaka kuijaribu Serikali lakini wameona tulivyozikamata na karafuu hizo tulikwenda mimi na wewe tulipokuwa wajumbe wa kamati Tanga gunia kumi na hivyo ziko njiani kuhakikisha gunia kumi zetu tunazipata zinarudi Zanzibar. Hilo ni jukumu la Serikali yetu kupitia Wizara ya Biashara katika kuzilinda na kulihifadhi zao letu la karafuu na tupo wakali kweli kwa suala hilo.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Waziri na Naibu Waziri kwa majibu mazuri waliyoyajibu, lakini pili kwa kuwa zao la karafuu ni uti wa mgongo wa uchumi wa Serikali yetu au ya Zanzibar.

Je kwa kuwa karafuu hizo ziliibiwa katika maeneo ya Tanga Horohoro huko, je karafuu hizo zimerejeshwa, na kama zimerejeshwa kuna utaratibu gani wa mikakati wa kuhakikisha kwamba karafuu zetu hazivuki Zanzibar kati ya visiwa vyetu viwili vya Unguja na Pemba kwenda Tanzania Bara na kwengineko.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, karafuu hizo bado mpaka hivi sasa bado zipo Tanga lakini tupo na utaratibu mzuri wa kwamba tunafuata zile taratibu za kisheria na taratibu za nchi ambazo karafuu hizo ziweze kurudi, lakini nakuhakikishia karafuu hizo zitarudi tupo katika hatua nzuri ya kukamilisha taratibu.

Lakini suala la pili kuzifanya karafuu zetu zisichukuliwe magendo, nakuhakikishia karafuu baada ya hizo gunia kumi mpaka leo hakuna tena tuliposikia magendo, nimesema mwanzo sisi tupo wakali na Mheshimiwa unajua katika kuzilinda karafuu zetu za Zanzibar zisichukuliwe magendo, lakini nimekwambia pia Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jinsi alivyozipandisha bei karafuu ni wazi kwamba magendo hakuna tena, kwa sababu sisi tunanunua karafuu bei kubwa kuliko huko kwenye magendo.

Nam. 240

Uwezeshaji wa Akina Mama wa Jimbo la Paje

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny. Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:

Pamoja na juhudi za Serikali kuwawezesha wanawake nchini na jitihada za Rais wetu mpendwa Dkt. Ali Mohamed Shein, bado yapo maeneo yanahitaji kuongezwa juhudi hizo kama vile Jambiani, Michamvi, Muungoni na Bwejuu ambako wao akina mama wana miradi yao mbali mbali wanahitaji kuwezeshwa kupatiwa fedha na utaalamu ili waweze kujikwamua na umasikini.

(a) Je, Wizara imejipanga vipi kuwafikia wanawake wa maeneo niliyoyataja ili waweze kuendeleza miradi yao na kujipatia kipato.

(b) Lini Waziri na Naibu Waziri watafanya ziara ya makusudi kuwatembelea akina mama wa maeneo hayo na kuwasaidia.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe mnaongea sana yaani mnazungumza kiasi ambacho humu ndani hatusikilizani.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto –
Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambae nae anaendelea kutupa pumzi zake na asubuhi tukaweza kukutana hapa katika Baraza lako tukufu tukiwa wazima na afya njema.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 240 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto katika kuhakikisha inawawezesha wanawake katika vijiji vya Jambiani, Michamvi, Muungoni, Bwejuu na sehemu nyengine za Unguja na Pemba imekuwa ikiwashajiisha wanawake kuanzisha vikundi vya aina mbali mbali vya uzalishaji mali na kuvipatia mafunzo na mitaji. Baadhi ya wananchi wa vijiji hivyo wamehamasika kwa sababu hadi kufikia tarehe 20 April, 2018 jumla ya Shilingi 69,500,000/= zimetolewa kwa vikundi tisa vya kinamama katika maeneo hayo.

Vikundi hivyo Mhe. Naibu Spika, napenda nivieleze kama ifutavyo, Jambiani Wengi Wape Biashara Shs. 2,500,00/= Malengo Group Kilimo cha Mwani Shs. 3,000,000/= Tuwajibike Biashara Shs. 4,000,000/= Tunabahatisha Biashara Shs. 3,000,000/=

Paje: Subira ni Moyo Biashara Shs. 1,000,000/= Masinyaa Group Mkahawa milioni mbili, Baloon Fara maduka ya nguo milioni tatu, Mnyonge Hanuni Duka milioni tatu, Juhudi Zetu Lilimo milioni 39 jumla ni milioni 69,500,00/=

Aidha maombi 24 ya mikopo katika vijiji hivyo yamepokelewa kwa mwaka 2017/2018. Hivi sasa Wizara imejipanga kuendeleza kuwaelimisha kinamama wa maeneo hayo na mengine juu ya taratibu za kuanzisha vikundi vya ushirika na masharti ya upatikanaji wa mitaji.

Mkakati mwengine ambao Wizara imejipanga kuwawezesha akinamama ni kuwaelekezea fursa za kiuchumi zilizomo katika maeneo yao na jinsi ya kuweza kuzitumia kikamilifu fursa hizo. Miongoni mwa fursa zilizomo katika maeneo hayo ni fursa katika sekta ya Utalii, Kilimo na huduma.

(b) Wizara imejipanga kuvitembelea vikundi hivyo tukiwa tumeambatana na Mhe. Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wengine ili kushirikiana katika kubadilishana mawazo na uzoefu katika uendeshaji wa shughuli za uzalishaji.

Mhe. Spika, pia nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi kuvitembelea vikundi vya ushirika katika majimbo yao ili kuunga nguvu za Wizara za kuleta maendeleo ya wananchi wetu.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kupitia Wizara yake kwa majibu mazuri na ambayo ya kukidhi haja juu ya maendeleo kwa vikundi vyetu vya ushirika Unguja na Pemba.

Lakini pili katika majibu mazuri ambayo yamejibiwa hapa juu ya taaluma ambayo inatolewa na Wizara kupitia idara inayohsika katika kuwafikia walengwa yaani wanavikundi juu ya kuwaelimisha. suala langu lipo hapa.

Kwa kuwa wananchi wa vijijini hasa wa ukanda wa pwani wamebahatika sana na kuwa na sehemu ya utalii ni biashara kubwa, lakini pia sehemu za kilimo wanazipata kwa wingi kwa mfano sehemu za Bwejuu, Paje na kwengineko. Je, Mhe. Waziri kwa kuwa maeneo yetu sie ya Mkoa wa Mjini wa Magharibi na kwengineko bahati mbaya utalii haupo hasa katika jimbo langu la Kijitoupele na sehemu nyengine.

Je, Wizara ina mpango gani pamoja na juhudi za Mwakilishi na Mbunge wa maeneo haya kuwafikia wananchi wetu kwa ngazi ya jimbo lakini si vibaya hata kushirikishwa katika Wilaya, ili waweze kuwekwa pamoja wale viongozi wa vikundi mbali mbali ili nao wajielewe kile wanachokikopa kinafanya kazi na kupata faida.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu katika kuwaelimisha kinamama kama alivyosema Mhe. Mwakilishi kwamba katika majimbo yao wao hawako na bahati wako mbali na bahari, kwa hivyo Wizara yangu ina mpango mbadala wa kuelimisha kinamama wale katika maeneo yao kuona ni biashara gani inayoweza kwenda pale ili wanawake wale wakaweza kujikwamua katika maisha yao na kuweza kufanya biashara nyengine.

Lakini vile vile nimwambie kwamba Wizara yangu iko tayari kushirikiana na Mwakilishi na Mbunge katika kuona kwamba tunawasaidia katika majimbo yao ili wananchi wetu waepukane na matatizo madogo ya maisha, ili waweze kujikwamua na kupata maisha yao ya nafuu.

Mhe. Zaina Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii adhimu katika asubuhi hii ya leo kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia sote uhai na uzima na kuwa salama, pili nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri sana ambayo amejibu, lakini pamoja na majibu yake mazuri napenda kumuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, Serikali ina mpango wa kuwezesha wananchi kiuchumi lakini kuna wananchi ambao watu wenye ulemavu wana vikundi vyao ambavyo vinataka kuwezeshwa lakini vikundi hivi bado havijaweza kuwezeshwa.

Je, Mhe. Waziri Wizara yake ina mpango gani ambao mahususi ulioandaa kuwapitia watu wenye ulemavu katika vikundi hivyo kuwawezesha na kuwapa elimu elekezi ya kuendeleza miradi yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu imejipanga kwanza kuwahudumikia wanawake wote na hatujalishi kuwatenga walemavu, kwa mwaka uliopita kuna vikundi kama 10 vya walemavu tuliweza kuwasaidia lakini katika mwaka huu tumejenga bajeti ya makusudi ya kuwalenga na kuwatembelea wenzetu hao wenye ulemavu kuhakikisha kwamba nao wanafaidika na wananufaika na mfuko huu, ili na wao waweze kujikwamua kimaisha.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niongezee tu swali lililokuwa limeulizwa na Mhe. Ali Suleiman Ali kuhusiana na kwamba sehemu ya pwani wanashughulika na masuala ya utalii, lakini wanaoishi mjini tumepeleleza katika maeneo wanayouza biashara, wanauzia vifaa watu ambao ni watalii wengi. Kuna vifaa ambavyo vinaweza kutengenezwa kwa mkono, kuna vitu vingi sana ambavyo vinaweza kutengenezwa na watu wote wanaoishi sehemu mbali mbali hasa waliokuwepo mjini ambao tunafuatilia sasa hivi. Kuna vitu vidogo vidogo ambavyo vinachukuliwa kama ni *sample* ya watu Wazanzibari. Ukiona kama Nigeria wanatengeneza vinyago vya watu ambavyo vinatengenezwa kama midoli mbali mbali. Kwa Zanzibar wanahitaji sana kuona midoli iliyotengenezwa ikiwa imevalishwa kanzu, imevalishwa kofia imevalishwa na makubazi ambavyo vinaweza vikauzwa na pia kwenye mavazi ya kike.

Sasa vitu vyote hivyo tumeviona kwamba inawezekana kabisa wale watu ambao hawaishi kwenye sehemu za pwani wakafaidika na wao katika biashara za utalii katika maeneo haya. Lakini pia kuna vyakula mbali mbali ambavyo vinatengenezwa ambavyo navyo tunajaribu kuangalia kwamba kuna Soko la Jumapili tunataka tuangalie ni jinsi gani tunaweza kuliweka katika mtandao kuhakikisha kwamba watalii wanaweza kufika pale kuja kuhakikisha kwamba wanafaidi masuala yale kwa wale watu wanaoishi mjini. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni kama tunavyojua kwamba tutakuwa na wiki ya ushirika duniani. Katika majibu yake Mhe. Waziri amesema kwamba wanaendeleza

kuwahamasisha wanawake kuendeleza vikundi vya Ushirika. Je, nilitaka kujua kwamba Pemba vipo vikundi vingapi vya ushirika na Zanzibar ni vingapi.

Lakini pia nataka kujua kwamba ni vikundi vingapi ambavyo vimeleta matumaini mazuri hasa tukizingatia fedha nyingi ambazo zimeshatoka. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Ni Pemba na Unguja sio Pemba na Zanzibar, Unguja na Pemba ndiyo iliyofanywa kuita Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mwakilishi kwamba sasa hivi tunakaribia kuwemo katika wiki ya Ushirika duniani ambapo kwa upande wa Zanzibar wiki hii itafanyika Wilaya ya Kaskazini (“A”) Mkokotoni Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Swali lake alilotaka kujua kwamba tuna vikundi vingapi vya ushirika hadi kufikia Machi 2018. Jumla ya vikundi 3033 vimesajiliwa. Vikundi hivyo ikiwa Unguja ni 2198 na Pemba ni 1135. Lakini vile vile ametaka kujua katika vikundi hivyo ni vikundi vingapi ambavyo vimeweza kufanya marejesho vizuri.

Namuomba Mheshimiwa Mwakilishi jibu lake hili niweze kumjibu kwa maandishi ili tuweze kupata jawabu sahihi. Ahsante Mheshimiwa.

Nam. 157

Kuweka Uwanja wa Ndege Mdogo Nungwi Unguja na Mkoani Pemba

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa kuwajibika kwa wananchi na kuleta maendeleo pamoja na kukuza utalii lakini kuna tetesi za ujenzi wa uwanja wa ndege mdogo Nungwi na Mkoani Pemba ili kurahisisha usafiri wa anga.

(a) Je, suala hili ni kweli.

(b) Je, kama ni kweli tayari eneo limeshapatikana au bado.

(c) Je, kama ni kweli mpango huu utatekelezwa katika Bajeti ya mwaka gani ya fedha.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali 1a lake Nam. 157 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar katika hatua ya kuimarisha sekta ya usafiri wa Anga Zanzibar imekusudia kujenga kiwanja kidogo cha ndege Nungwi, Shehia ya Kilindi Wilaya ya Kaskazini "A" kwa Unguja, lakini pia kiwanja kama hichi kitajengwa Pemba Wilaya ya Mkoani katika sehemu ya Muambe.

(b) Mhe. Naibu Spika, maeneo hayo tayari yameshaainishwa na Mamlaka tayari imeshapata hati kwa eneo la Kiwanja cha Ndege kilichopo Nungwi na pia kinafanya maandalizi ya kiwanja cha Ndege cha Muambe Pemba.

(c) Mamlaka tayari imeshaanza utekelezaji wa mpango huo kwa kuanza kusafisha maeneo ya Kiwanja, pia kulipa fidia ya mazao katika viwanja hivyo na tayari wanafanya tathmini ya mazingira katika viwanja hivyo.

Aidha, Mamlaka katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa kiwanja cha Nungwi imetenga fedha za maendeleo ambayo yanaanza kwa matayarisho baadae watafanya tathmini ya kiwanja chenyewe kwa ujumla ili kuweza kujua ni gharama kiasi gani itakayoweza kutumika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nimshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Lakini pia nimpe pongezi kwa kuizungumzia ChakeChake mjini, mimi ni Mwakilishi wa ChakeChake mjini. Maana ChakeChake ina Chonga, Wawi ina sehemu mbali mbali, lakini ni mjini ninamshukuru sana Mhe. Waziri. Lakini nina swali la nyongeza ni kumwambia kwamba namshukuru Waziri katika jitihada zake za kuweza kuuleta ukaribu baina ya Unguja na Pemba kwa usafiri kutokana na mkondo wa bahari tulionao.

Katika suala la anga ametutia moyo sana katika kutaka kutukaribisha zaidi. Nimuulize waziri, wasafiri wengi wa Unguja na Pemba ni wa meli, ana mpango gani wa kutukaribishia kama hivyo baina ya Mkoani na Nungwi kutujengea bandari ya meli.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba usafiri wote uwe wa anga uwe wa meli vyote vinatakiwa kufanywa kwa ukaribu zaidi. Kwa hivyo kwa vile Nungwi kunajengwa Uwanja wa Ndege tunategemea Mkokotoni tutajenga bandari. Bandari ya Mkokotoni sio ngeni tangu asili ilikuwepo watu wakifia pale, kwa hivyo sasa hivi kitakachofanyika ni kuimarishwa zaidi iwe ni bandari sahihi ambayo inaweza ikarefusha safari za watu wa Pemba.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, hasa tukiangalia kwamba wakati wa sasahivi biashara ndio maendeleo. Kwa kuwa mwenzangu kaniwahi suala la bandari ndogo ndogo kwa upande wa Nungwi au Kaskazini Unguja kuelekea Pemba.

Lakini je, katika jibu hilo zuri ambalo lina matayarisho kajibu vizuri tu lina matayarisho yake na huenda likawa na *Inshaallah* liwe ili kuongeza ajira kwa vijana wetu. Ana mpango gani Mhe. Waziri kupitia Wizara yake kwa kuwa Kizimkazi ni watu wanaofiri

kwenda Bara na kurudi mara kwa mara na pale ni urahisi zaidi wa kuhakikishwa kwamba wananchi wanasafiri kwa wepesi na kuingia Unguja kwa wakati unaofaa. Wizara nayo ina mpango gani wa kulifikiria hilo juu ya kuharakisha harakati zetu za maendeleo katika nchi yetu na vijana kupata ajira.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, ni kweli haya anayoyasema na sio kwamba ni bandari hizo mbili tu nilizozitaja kutakuwa na nyengine nyingi. Lakini ili kuweza kujengwa bandari ndogo ndogo inategemea na maeneo husika yafanyiwe uchunguzi, yakidhi haja.

Ni kweli watu wa Kizimkazi wanakwenda unununio mara kwa mara ni sehemu ndogo ambayo inachukua tu nusu saa, lakini lazima tuangalie na uhalisia wa maeneo husika, pengine kwa jahazi au kwa ngarawa unaweza ukavuka, lakini bandari ni lazima iwe inakidhi vigezo vile vinavyotakiwa kujengwa. Hatujafanya shughuli hiyo kwa Kizimkazi lakini tutalitilia manani tuliangalie ikiwezekana nako tunaweza tukapapendekeza.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo sana la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha (c) cha majibu ya Mhe. Waziri alieleza kuwa utekelezaji wa mpango huo kwa kuanza safi tayari umeanza. Lakini vile vile alizungumza kwamba kutakuwa na tathmini ya mazingira kwa viwanja hivi.

a) Nimuulize Mhe. Waziri lipi linatakiwa litangulie mwanzo, kati ya usafi na tathmini za kimazingira na kwa sababu zipi.

b) Kwenye kifungu hicho hicho cha (c) mwisho alisema kwamba tayari mwaka huu 2018/19 imetenga fedha za maendeleo kwa ajili ya uendelezaji kiwanja hicho. Je, Mhe. Waziri fedha zilizotengwa hizo ni kiasi gani na katika bajeti hii zipo katika fungu gani kwa sababu sikuwahi kuziona ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake (a) na (b) kama hivi ifuatavyo.

a) Mheshimiwa Mwakilishi nataka tufahamu kitu kimoja kwamba kwanza mipango na matayarisho ni katika kusafisha na pia katika kufanya tathmini ya mazingira. Kwanza sehemu yenyewe iweze kupitika, ili watu waweze kupita kuweza kufanya hayo, haimaanishi kwamba tunasafirisha eneo lote lile kabla hatujafanya tathmini ya mazingira.

   Ili hayo mazingira yaweze kufanyiwa kazi ni lazima watu wapate pa kupita, kwa hiyo hicho ndicho kitakachofanyika mwanzo. Tathmini ya mazingira na yale yote yanayohusiana na hayo yanafanywa mwanzo ili kufika katika sehemu hiyo ni lazima pasafishwe ili watu waweze kupita na hicho ndicho nilichokikusudia katika kusafisha.

b) Tunasema kwamba tulitenga pesa katika maendeleo. Nilichokizungumza hapa kweli ukiangalia kwenye bajeti yetu hutoweza kulikuta hili kwamba limeandikwa kwamba katika maendeleo bandari tulizonazo ni zile kubwa ambazo sasa hivi zipo. Lakini ili hili nalo liweze kutekelezeka lazima tuwe tuna fedha. Kwa hiyo tutaomba fedha *specific* kwa ajili hii ya kufanya hiyo kazi. Kwa vile hizi bandari zinatengenezwa na serikali na mara nyengine huwa tunapata wafadhili kwa hivyo tunaweza tukachukua fungu la wafadhili tukaweka pale kwa kuanza matayarisho. Mwaka huu hatuijengi bandari hii ni matayarisho yake tu.

Nam. 218

Kuboreshwa kwa Barabara Unguja na Pemba

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ujenzi wa miundombinu ya barabara nchini, Unguja na Pemba, nakutumia fedha nyingi kwa barabara hizo. Kwa kuwa barabara zinatumia fedha nyingi katika ujenzi wake.

Je, Wizara haioni ipo haja ya kuzijengea kingo za pembeni ili kuzinusuru wakati wa mvua.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 218 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, nimuunge mkono Mhe. Mwakilishi kwa kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dk Ali Mohammed Shein, kwa ujenzi wa miundombinu ya barabara Unguja na Pemba ambayo huwa inatumia fedha nyingi. Pia napenda kusisitiza kwamba, katika wizara ambayo inatumia asilimia kubwa ya Bajeti ya nchi basi ni Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji karibu asilimia 40 ya bajeti inatumika katika masuala ya barabara.

Mhe. Naibu Spika, haja ya kuzijenga kingo za pembeni mwa barabara, ili kuzinusuru wakati wa mvua zisiharibike kuna umuhimu wake. Kwani maji yakituwama pembezoni mwa barabara yanarowanisha na kulainisha udongo ulio chini ya barabara na kuozesha lami iliyowekwa juu yake. Kwa hiyo magari yakipita huko husababisha mmongo'nyoko wa pembeni mwa barabara hizo.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Mawasiliano kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza thamani ya barabara ujenzi wake ni ghali mno, na katika jibu ambalo linalo mimi Mhe. Waziri pamoja na yeye kunijibu nimeridhika, tunaambiwa kama tunampa Mkandarasi kutoka nje kilomita moja inatumia 1.2 bilioni lakini kama tunawapa wazalendo UUB Idara yetu maalum ya Wizara ambayo inahusika watatumia milioni 750 mpaka milioni 800 kwa kilomita moja lakini naamini ubora upo pale pale au wetu siye unaweza ukawa mzuri zaidi.

Swali langu lipo hapa kwa kuwa katika kilomita moja tunatumia bilioni 1.2 lakini barabara hiyo tunaamini ipo katika kiwango kizuri. Je, Mhe. Waziri atatwambia thamani ya hayo matofali ya pembeni ya kudhibiti barabara ile yatakuwa kiasi gani ili ishindwe kutekeleza hilo kunusuru barabara zetu zitumike kwa muda mrefu kuliko muda mfupi ambalo hatutegemei litokezee hilo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, ni kweli hizo gharama alizozisema ndivyo zinavyokuwa. Lakini mara nyingi barabara zinazojengwa na wakandarasi kwa utaratibu kama huo zinakuwa ni zile barabara zinazotolewa kwa ufadhili, sio zile zinazojengwa na serikali. Sasa wafadhili wanapokuwa wanatoa ufadhili yale yote yanakuwa yanajumuishwa na wafadhili wanakubali. Ukiangalia mara nyingi barabara za wafadhili utazikuta ndiyo hizo ambazo zimejengwa na kingo na kila kitu kwa sababu ule unakuwa aidha ni mkopo au serikali imetunukiwa na wafadhili wengine kujenga barabara zile.

Lakini zile barabara tunazozijenga sisi wenyewe mara nyingi ndio hizo zinazoishia bila ya kujengwa kingo kwa sababu tunakuwa hatuna fedha za kutosha. Kama tunaweka kingo ina maana tujenge barabara fupi ili tuongeze zile pesa kwenye kingo au tujenge barabara ndefu ili watu waweze kupita sehemu ndefu lakini bila ya kingo. Sasa kupanga ni kuchagua, kama tunaamua tujenge barabara ya nusu kilomita ili tutie kingo au tujenge barabara ya kilomita tatu bila ya kingo huwo ni uchaguzi wetu, kama utapendekeza hivyo niko tayari kuchukua ushauri kutoka kwako.

Mhe. Zaina Abdalla Salum: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona tena mara ya pili. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri napenda kumuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri kuna miundombinu ambayo imekwisha kujengwa imekuwa haizingatii miungombinu ya kupitia waendaji wa maguu au watu wenye ulemavu hasa wale wenye vigari na wale wanaokata njia. Na nyengine zinazotarajiwa kujengwa nadhani itakuwa ndiyo hivyo hivyo. Je, Mhe. Wizara wizara yako pamoja na wakandarasi ina mpango gani wa kuzirekebisha barabara zilizokwisha kujengwa na zile ambazo itakazojengwa ili kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanaweza kuzitumia.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu mpenzi wangu na najua kaniuliza kwa madhumuni mazuri tu kwa sababu anapenda nimsaidie. Ni kweli katika kupita kwangu kwa kipindi hichi kifupi nilichoishi pale kwenye Wizara ile hilo naona kama halikuzingatiwa. Mara nyingi barabara ni chache sana ambapo utakuta zinakingo pembeni. Lakini kwa vile kuna umuhimu wa hilo na walemavu sasa hivi wanapewa kipa umbele kwa sababu na wao kwao ndio hapa hapa

na maisha yao tunayafahamu, tutajitahidi kuona kwamba tutakapojenga barabara hizi mpya au kuzifanyia ukarabati nyengine pale ambapo pana nafasi.

Maana tukiangalia barabara zetu nyingi za zamani watu wamejenga mpaka chini ya barabara wakati kuna eneo linatakiwa kuwe na *buffer zone*, ambapo barabara ikitakiwa kutanuliwe kuwe na nafasi. Hili nyuma linaonekana kwamba halikuzingatiwa kwa hivyo watu wamesogea unaweza ukakuta mpaka nyumba imegusa barabara. Pale ambapo uwezekano wa kupitisha barabara ndogo kwa ajili ya waenda kwa miguu tutafanya hivyo. Lakini mbele katika barabara tutakazozijenga kwa pale panapostahiki kufanya hivyo tutalizingatia hilo.

Nam. 187

Uimarishaji wa Shamba la Mifugo Pangeni

Mhe. Asha Abdalla Mussa – Aliuliza:

Lengo la Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ni kuendeleza mashamba ya mifugo yaliopo Unguja na Pemba kwa kuimarisha mifugo n.k likiwemo shamba la mifugo Pangeni.

Je, Wizara ina mpango gani kwa sasa ili kuhakikisha kuwa mashamba hayo yanaimarika kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi – Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii kwanza kabisa naomba nizungumze haya kidogo yafuatao machache, kwanza nampongeza sana Mhe. Asha Mwakilishi wa Kiwengwa huyu kwa kutaka kujua mustakbali wa shamba la Pangeni, najua limo katika Jimbo lake. Kwa hivyo tushirikiane nae ili tuliendeleze hili shamba.

Halafu nampongeza Mhe. Said Soud anataka kuanzisha shamba la mifugo kule Pemba kwa hivyo na yeye tutashirikiana naye hakuna tatizo.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 187 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali inaendelea kuhamasisha na kuwaendeleza wafugaji wa ng'ombe na mifugo mengine kwa kutumia mashamba binafsi pamoja na mashamba ya Wizara ya Kilimo. Mashamba ya Pangeni na Kizimbani (Unguja) na Chamanangwe (Pemba) ni maeneo yaliyotengwa na Serikali kwa ajili ya kufanyia tafiti mbali mbali za mifugo wakiwemo ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku, bata, sungura, ndege, malisho pamoja na maradhi mbali mbali ya mifugo. Mashamba haya yanaimarishwa kwa kujenga na kukarabati miundombinu ya majengo, usambazaji wa maji, uimarishaji wa maeneo ya malisho ya mifugo pamoja na kuongeza watendaji wenye sifa zinazostahiki ili kufikia lengo hilo lilokusudiwa ahsante sana.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, napenda nimuulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

1) Mhe. Waziri katika majibu yake amesema kwamba maeneo haya yalitengwa na Serikali kwa ajili ya kufanyia utafiti mbali mbali za mifugo ikiwemo ng'ombe, mbuzi na mifugo mengineyo, nilitaka kujua katika shamba hili la Pangeni lina ukubwa gani shamba hilo.

2) Mifugo iliyopo pale ni mifugo mingapi ya aina gani. Mhe. Naibu Spika, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: kwa ruhusa yako na kwa idhini ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi naomba kumjibu Mhe. Asha swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Kwanza kabisa lina ukubwa gani shamba hilo, kwa sasa nasikitika kusema kwamba hatuwezi kutoa takwimu kwa sababu shamba hilo limevamiwa kuna watu wamelivamia wamejenga majumba wanalima mashamba kwa hivyo tabaan limepungua lile ukubwa wake, kwa hivyo namuahidi kwamba tutafanya *survey* ya kulipima shamba lote ili kujua shamba hilo lililobakia.

b) Ni aina gani ya mifugo iliyopo hapo Pangeni, Pangeni mpaka sasa hivi wapo ng'ombe, ng'ombe wa maziwa tulitegemea pia pawe na mbuzi, lakini utafiti wetu utakapoanza tutaona ni aina gani zaidi ya mifugo ambayo tutaiweka pale zaidi ya hao ng'ombe ambao wako hivi sasa ahasante Mheshimiwa.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia na mimi fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri, shamba la Pangeni, ni shamba kubwa lilikuwa na mifugo mizuri mimi nalijua, lakini katika majibu yako umesema shamba hili limevamiwa na hapa sisi huwa tunapiga kelele kila siku kuhusu uvamizi wa mashamba haya ya serikali.

Nilitaka kujua shamba waliolivamia wamechukuliwa hatua gani mpaka muda huu tulionao, lakini je, shamba hili lina hatimiliki.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba nimjibu Mhe. Panya Viti Maalum wanawake swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Anataka kujua hatua tulizochukua ni kwamba kwanza niseme kwamba shamba la Pangeni hapo katikati siku za nyuma kidogo lilikuwa limesuwasuwa sana watu wakaanza kulivamia, sasa hatua zilizochukuliwa kwanza ni kupanga mpango ambao utawezesha kurudisha hadhi ya shamba lile, kwa sababu baada ya Mapinduzi shamba lile lilikuwa limekusudiwa liwe ni shamba la utafiti na litakuwa ni shamba la utafiti.

(b) Kwa hivyo mipango imekwisha pangwa kulitumia shamba lile kama shamba la utafiti na uimarishaji wa miundo mbinu pale umeshaanza kuna kisima kimeshachimbwa pale. Kwa hivyo hatua tutakazozichukua kwa watu ambao wamevaa tutakwenda kuzungumza nao tutawaeleza madhumuni ya kuliendeleza shamba lile kwa faida yao na hatimae tutafikia makubaliano ya kuliacha pengine lile shamba, au tutafikia makubaliano yoyote ambayo tutakubaliano nao ili waweze kutoa nafasi ya kuendeleza shamba lile. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Jibu (b) bado hajanijibu shamba lina hati miliki.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa namna anavyoendelea kujibu maswali ambayo yamefanyiwa kazi.

Lakini pia nichukue nafasi hii, kumpongeza Mhe. Panya kwa namna anavyolifahamu lile shamba, ni kweli analifahamu shamba ni kubwa linalingana na shamba lile ambalo liko kule Pemba Chamanangwe na mashamba mengine ambayo yaliwekwa toka hapo asili kwa ajili ya utafiti.

Sasa nataka nimwambie kwamba uvamizi uliofanyika pale watu wamefanya uvamizi sio kisheria na serikali ina sheria na taratibu zake na kanuni zake juu ya watu walovamia, Wizara imejipanga hatua ya mwanzo kama alivyosema Naibu Waziri, tayari tumeweza kuwa *identify* kuwajua watu waliovamia, wapo watu ambao wamevamia kwa kuweka mifugo yao, wapo watu ambao wamevamia kwa kujenga majengo ya kudumu.

Kwa hivyo zipo hatua ambazo tutazichukua kwa yale majengo yalowekwa ya kudumu kama taratibu zetu zitavyoeleza. Ni wazi kwamba watu wale wamekaa kwa muda mrefu kwa hivyo serikali itatizama utaratibu namna ya kuwaondosha ili lengo lake la kuweka ile taasisi ya kufanyia utafiti iweze kufanya kazi zake kikawaida.

Kama tunavyojua hivi karibuni tu serikali imeweza kuweka taasisi inayojitegemea wakala wa kufanya tafiti za mifugo na moja ya sehemu iliyolengwa ni shamba hili la Pangeni. Kwa hivyo serikali inafanya mazungumzo nao na hatua zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria zetu.

Lakini swali zima kwamba shamba hili limepimwa lina hati au halina hati, mashamba ya kilimo takriban yote yana hati, hati zipo ndani ya wizara yetu na zile hati zitakuwa ni usimamizi wa wale waliovamia kuja kufanya yale mambo ambayo hayakufanyika sheria ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Hidaya Ali Makame: ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona na mimi kuweza kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri pamoja na Mhe. Waziri kwa majibu yao mazuri na ufatiliaji mzuri kuhusiana na mashamba ya kilimo ili kuweza kufanikisha katika maswala haya.

(a) Lakini ningependa kumuuliza swali dogo la nyongeza, Mhe. Naibu Waziri katika majibu yako hapa umetaja kwamba na shamba la Kizimbani kwamba nalo ni miongoni mwa mashamba hayo.

Lakini kama tunavyofahamu kwamba pale Kizimbani ni eneo la Utafiti pia na shamba lile lilikuwa linawasaidia sana sana wanafunzi na hata walimu ambao wanahusika na chuo kile cha utafiti pale Kizimbani.

Lakini kwa sasa hivi shamba lile na uzuri lilo nao na ukubwa lilonao na uzio mzuri ambao upo wa kulikinga lile shamba kuto kuvamiwa bado upo na wananchi wanaliheshimu sana lakini shamba lile bado halina mifugo kiufupi ya aina yoyote ambayo yanaweza kuwasaidia wananchi au wanafunzi wale wanaokwenda kusoma pale chuo cha kilimo Kizimbani.

Je Wizara yako ina mpango gani wa kuweza kuliimarisha shamba lile na kurudi kwenye hadhi yake ile ambayo ilikuwepo kwa ajili ya wale ng'ombe ambao walikuwa wanapatikana pale, ili wanafunzi waendelee na masomo yao na zile tafiti kama zilivyokusudiwa ziendelee kufanyika.

(b) Ndani ya shamba lile sasa hivi kunaonekana kuna vigombe viwili vitatu Mhe. Naibu Waziri nataka kujua je Ngo'mbe wale walioko mule ni wanahusika na lile shamba yaani wa Chuo au ngo'mbe wale ni wa wananchi tu wa kawaida nataka kujua hilo Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika kwa ruhusa yako sasa na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi naomba kumjibu mjukuu wangu huyu Mhe. Hidaya Ali Makame swali lake alilouliza, kwanza alitaka kujua mpango wa kuliimarisha hilo shamba la Kizimbani.

(a) Mpango upo, tumesema kwamba tunataka kuyatumia mashamba yale kwa utafiti na kama alivyosema Mhe. Waziri hapa kwamba kumeundwa wakala wa utafiti ambayo inaitwa zaliri hao ndio watakaoshughulikia na uimarishaji wa shamba lile la Kizimbani pamoja na mashamba mengine ambayo tumeyataja ya mifugo.

Kwa hivyo usiwe na wasiwasi Mheshimiwa shamba lile litaimarishwa pengine zaidi hata kuliko hivyo lilivyokuwa hapo awali.

(b) Ngo'mbe waliopo ni wa nani, ngo'mbe waliopo pale taarifa ziliopo ni wa mifugo hatujasikia kwamba kuna ngo'mbe wa watu binafsi lakini kama wapo basi pia kama ambavyo tutachukua hatua ya huko Pangani basi na hapa pia tutafanya tathmini kujua na nani pengine kaweka mifugo yake ili tuweze kuliimarisha shamba lile kama lilivyotakiwa. Ahsante sana Mheshimiwa.

Nam. 22

Ziara ya Ghafla ya Mheshimiwa Waziri wa Afya Hospital ya Mnazi Mmoja

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny .Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:

Mnamo tarehe 2/3/2018 mara baada ya kuapishwa Waziri wa Afya alifanya ziara ya ghafla nyakati za usiku katika Hopitali ya Mnazi Mmoja.

(a) Mambo gani aliyoyaona Mheshimiwa Waziri katika ziara hiyo.

(b) Mikakati gani ya uhakika ya kutatua changamoto sugu za Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Afya naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 22 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibu swali naomba kusahihisha kidogo swali la Mhe. Jaku ili swali liendane na jawabu la Serikali.

Mara baada ya kuapishwa Waziri alifanya ziara ya ghafla nyakati za usiku, lakini usahihi ni kwamba mara baada ya kuteuliwa Mhe. Waziri alifanya ziara ya ghafla wakati wa usiku katika hospitali ya Mnazi Mmoja. Sasa naomba nimjibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba mara baada ya kuteuliwa Mhe. Waziri wa Afya alifanya ziara ya ghafla katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, na katika ziara hiyo Mhe. Waziri, pamoja na mambo mengine alipata nafasi ya kujionea mambo mengi yakiwemo yafuatayo:-

- Uhaba mkubwa wa wafanyakazi
- Wingi wa ndugu na jamaa wa wagonjwa
- Wingi wa wagonjwa waliofika kupata huduma ingawaje ilikuwa ni usiku
- Hali isiyoridhisha ya usafi kwa baadhi ya maeneo katika hospitali hiyo.

(c) Mhe. Spika**,** katika hatua ya kutatua changamoto katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, Uongozi wa hospitali kupitia bodi yake ya ushauri, imeandaa mpango kazi wa mwaka mmoja kwa ajili ya kukabiliana na changamoto hizo na Wizara ya Afya umeuridhia mpango huo, na imejipanga kusimamia na kuhakikisha unatekelezwa ili kuondosha changamoto ambazo hazina ulazima na ni za muda mrefu ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Afya, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu mazuri ambayo yanatupa faraja kuwa ya uwazi na ukweli hasa tukizingatia kwamba kuna mambo manne aliyoyagusa hapa.

(1) Uhaba mkubwa wa wafanyakazi

(2) Wingi wa ndugu na jamaa wa wagonjwa

(3) Wingi wa wagonjwa wanaofika kupata huduma pamoja na kuwa wakati huo ulikuwa ni usiku lakini

(4) Hali isiyoridhisha ya usafi kwa baadhi ya maeneo katika hopitali hiyo

Swali langu liko hapa je kwa kuwa Mhe. Waziri mara baada ya kuteuliwa alifanya ziara hiyo ghafla na usiku akakuta hali hiyo, kwa sasa.

(a) Uhaba mkubwa wa wafanyakazi umefikia wapi.
(b) Hali isiyoridhisha usafi kwa baadhi ya maeneo katika hopitali hiyo nayo imefikia wapi ili wananchi waridhike kwamba hospitali ile ni kiyoo na jamii ya wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Shihata Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, katika jibu langu la msingi nimemjibu kwamba viongozi wa wizara wamekaa pamoja na kupanga mikakati maalum mpango kazi wa mwaka mmoja ili kufatilia changamoto hizi ambazo hazina ulazima kuisumbua hospitali yetu ya Mnazi Mmoja.

Sasa nataka tu nimjibu kwamba katika mikakati hiyo ilopangwa kwanza imeanza kutatua huu uhaba wa wafanyakazi tumeruhusiwa na serikali kuajiri wafanyakazi, kwa hivyo tumeajiri wafanyakazi ingawaje bado hawajatosha au uajiri unaendelea.

Lakini kuhusu hili suali la usafi pia hawa wafanyakazi tuliowaajiri basi wanaendelea pia wamegaiwa katika sehemu ya kufanya usafi. Hata hivyo tulikuwa tuna mpango wa kuajiri kampuni kwa ajili ya kufanya usafi sasa juzi kama mnakumbuka vijana wana kumbukumbu tumetoa matangazo ya kwamba wananchi watoto wetu vijana waombe ajira ya *Ordely*.

Ordely wakifika katika hopitali zetu kazi yao moja ni kufanya usafi wa nje na wandani. Kwa hivyo Mheshimiwa ondoa wasiwasi suala hili la usafi katika hospitali zetu licha ya Mnazi mmoja litatuka baada ya muda mfupi.

Lakini nampa kutoa ushauri na ombi maalum kwa *relative* yaani hawa ndugu na jamaa ambao wanakwenda hospitali na jamaa zao hawa ni watu wazuri ambao wanaharibu mazingira katika hospitali. Mara nyingi wanakuwa hawana utulivu wa kutulia sehemu moja hawana uangalifu wa kutumia zile huduma ambazo tumeziweka kwa mfano ndoo zile za plastic (*dust bin*) za kuweka takataka hawazitumii wao wanaweka tu taka popote ambapo wanakaa na kusubiri mda ili wakaone wagonjwa au kushuhulikia wagonjwa.

Kwa hivyo kupitia kujibu swali hili Mheshimiwa naomba sana niwambie wananchi wanaokwenda hospitali zetu hususan hopitali ya Mnazi Mmoja basi waangalie sana zile sehemu ambazo tumeelekeza taka zitupwe ili kuchelea kuharibu mazingira ya hospitali yetu.

Nam. 127

Udhibiti wa Vyakula na Vinywaji Vinavyotoka Nje ya Nchi

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Vyakula na vinywaji ambavyo vinatoka nje vinaingizwa nchini na wafanyabiashara wadogo wadogo pengine bila "Agent" na vitu hivyo vinatiliwa mashaka kuwa huleta madhara kwa mlaji au watumiaji na pengine kusababisha madhara makubwa kiafya au kifo.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi katika vyakula na vinywaji vinavyoingizwa nchini bila "*Agent*."

(b) Je, mtumiaji akipata tatizo kwa vyakula na vinywaji vilivyoingizwa, mtumiaji atapata malipo ya matibabu kupitia wapi.

(c) Je, imeshawahi kutokea tatizo hilo na Wizara ililimaliza vipi.

a) Je, imeshawahi kutokea tatizo hilo na Wizara ililimaliza vipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Afya naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake Pemba swali lake Nam. 127 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa napenda nichukuwe nafasi hii kulieleza Baraza lako Tukufu kwamba waingizaji wote wa bidhaa zinazotoka nje ya nchi yetu zikiwemo vyakula na vinywaji, wanatakiwa kufuata utaratibu maalum wa uingizaji wa bidhaa nchini iliwemo vyakula kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa kiafya kwa watumiaji wa bidhaa hizo.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nijibu swali kama ifuatavyo:-

a) Wizara ya Afya kwa kupitia Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi *(ZFDA)* inasimamia usalama wa bidhaa zote zinazoingia nchini, zikiwemo za vyakula na vinywaji na kuhakikisha usalama wa bidhaa hizo kwa watumiaji bila kuangalia vimeingizwa na *Agent* au Wafanyabiashara wadogo wadogo. Aidha, waingizaji wa

bidhaa hizo wanatakiwa wawe na kibali maalum kutoka kwa Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi kinachowaruhusu kuingiza bidhaa hiyo nchini.

b) Kwa bahati mbaya sana ikitokezea mtumiaji kupata tatizo lililosababishwa na utumiaji wa bidhaa hizo, atalazimika kutoa taarifa pamoja na ushahidi wa uthibitisho wa aliponunua bidhaa hiyo, kwa Ofisi ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi kwa ajili ya kuipa nafasi ofisi hiyo kufuatilia na kuchukua hatua. Aidha, matibabu ya malipo yanatokana na tatizo hilo yatapatikana kutokana na matokeo ya ufuatiliaji wa mchakato mzima wa uingizaji na uuzaji wa bidhaa hizo.

c) Hadi sasa Wizara haijapokea taarifa ya tatizo la kiafya lililosababishwa na utumiaji wa chakula au kinywaji. Tunawaomba wananchi kupitia kujibu swali hili watupe taarifa yenye uthibitisho kamili mara itokeapo tatizo hilo miongoni mwao.

Kikawaida mwananchi akisumbuliwa na bidhaa mfano kanunua mkate au kanunua pipi au kanunua soda ambayo imesha-*expire* katumia na kapata madhara basi tunachokifanya ni kwenda kwenye duka lile kuipeleka soda ile na kumwambia soda imesha-*expire* mheshimiwa hili si sahihi moja kwa moja nyamaza kimya uje katika bodi yetu utowe taarifa wao watamfatilia, kwa sababu utakapokwenda kwake unampa nafasi nzuri ya kuficha ile bidhaa mbovu ambayo alikuwa anaiuza, tukumbuke kwamba hauzi kwa makosa alikuwa anaiuza.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa punguza maelezo makubwa muda haupo Mhe. Suleiman Sarahan swali nitatoa moja kwa sababu dakika za kuongeza tayari zimeshamalizika na naomba Mhe. Waziri umjibu kwa ufupi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini mimi nimuuliza Mhe. Waziri kwamba mimi sina tatizo na kwamba una Bodi inayoshughulikia na chakula lakini ninavyohamu ni kwamba serikali huwa inatoa vibali kwa wafanya biashara wanaoleta bidhaa ili bidhaa zile zinajulikana kama ni mfanyabiashara.

(a) Tatizo langu linakuja kwamba vifaa vinavyoletwa na watu wasiokuwa na vibali mtu yule akishaingiza mtu yule hajulikani tena na wala hajulikani *agent* gani, lakini tukumbuke kwamba madhara ya chakula hayatokei siku hiyo kwa hiyo sasa tatizo langu linakuja hapa kwamba je, serikali imethibiti vipi watu waanaoingiza chakula au vinywaji waliokuwa hawana leseni au hawana vibali maalum kwa kuingiza ndani na athari zake zikapatikana vipi au yule mtu ambaye amepata athari atalipwa vipi.

(b) Nakumbuka hata humu katika Baraza letu tumeipitisha sheria hata kama zile video zinakuwa kama ushahidi. Mheshimiwa hivi sasa katika mwezi wa Ramadhani uliopita ilitoka sadaka katika wilaya nyingi sana, zikiwemo mambo ya tende na michele na kila kitu na zimerushwa video nyingi za mchele unaonyeshwa na jamaa mmoja anayesema daktari na hiyo *clip* ipo na kila kitu. Mtu huyu amesema yuko tayari kutoa ushahidi kwamba yeye mchele huu ulioletwa, sasa nikuulize tu waziri je suala hili

unalifamu au mtu huyu aliyeleta mchele huu anafanyiwa utaratibu gani wa kukamatwa na kuweza kufikishwa kwenye vyombo vya sheria kutokana na tatizo hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan swali lake la nyongeza (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mheshimiwa kuhusu ambao wanaingiza bila ya vibali kikawaida hawapiti kwenye njia ambazo zimewekwa na serikali hawa ni binadamu na kama binadamu anapotaka kufanya jambo lake wana njia zao ambazo wanazipita na wananchi ndio wanazifahamu zaidi kulikoni sisi kwa hiyo tunawaomba wananchi wakigundua na wanafahamu watujulishe ili na sisi tuweze kudhidhibiti njia hizo kuzifalitia na kuweza kuwadhibiti. Lakini tukiwapata basi vyombo vya sheria vinafanya kazi yake.

(b) Kuhusu hili la mchele naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan kwamba hili tunalo, tunalifahamu na tumeshachukua hatua ya kuwapeleka wanaohusika katika vyombo vya kisheria, hatua zinachukuliwa baada ya muda mfupi.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante mheshimiwa tunaendelea Waheshimiwa Wajumbe kabla ya, Mhe. Mohammedraza nimesimama mimi nikisimama hutakiwi kusimama wewe subiri nikae halafu utaendelea na wewe.

Nini tangazo hapa la Mhe. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti naomba wajumbe wote wa Kamati hii wafike katika ukumbi mkubwa baada tu ya maswali na majibu ahsante. Naam Mhe. Mohammedraza kuhusu utaratibu.

TAARIFA

Mohammedraza Hassanaali Mohamedali: Mhe. Naibu Spika, hii ni mara yangu ya kwanza katika historia ya Baraza la Wawakilishi kusimama na kanuni ya 42 na nikipenda kutoa taarifa isiyo na mjadala wala nisipoteza muda wako uweze kuniruhusu ili tupate kauli ya serikali hilo tu nililokuwa nalo Mhe. Naibu Spika, sitaki lijaliwe wala sitaki kupoteza muda kwa katumia kanuni ya 42 ni jambo ambalo muhimu linatugusa zote Wazanzibari na Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima kwa kutumia kanuni ya 42 Mhe. Naibu Spika, ningeliomba Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar itowe tamko maalum kwa serikali kwa wafanyabiashara na kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni kumejitokeza na mambo ya uwazi yanafahamika suala la chakula, madawa, *pampers* na tunazishuhudia sehemu zinazokwenda kuangamizwa.

Mhe. Naibu Spika, hii itatuathiri sote si kila anayepepesuka mlevi, wafanyabiashara wanafahamika, *container* walizoleta zinafahamika lakini Mhe. Naibu Spika, leo wafanyabiashara hatujamuona hata siku moja mtu kwenda kwenye karatinga au akakamatwa. Kwa hivyo naomba kauli ya serikali kama sisi wafanyabiashara tuna uwezo wa kutoa zaka basi tumuamini Mwenyezi Mungu.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo wanaoathirika zaidi sisi watendaji wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hatuendi Mnazi Mmoja tukatibiwa, wanaoumia ni wakulima na wakwezi wa shamba kwa hivyo maradhi yatazidi serikali itabeba mzigo tena ya kuhudumia wale na matokeo yake kule shamba atasema huyu karogwa kumbe kile chakula kibovu ndio kilomfanya asiwe na akili nzuri.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba kwa heshima zote serikali itowe tamko misaada yote itakayotolewa zipite kwenye njia za taratibu hata kama Mhe. Rais, Mhe. Makamu wa Pili, Viongozi wote watakapopokea misaada zitazamwe zipimwe na wahusika halafu kama mtu anataka kutoa msaada zakka zijadiliwe.

Mhe. Naibu Spika, mfano wangu kama mimi juzi nilikwenda kukabidhi msaada Tanzania Bara kwa Waziri Mkuu, kile chakula nilichokipeleka mchele, sukari, unga wa ngano, mafuta walikuja wataalamu wakavipima baada ya kuvipima nilipopeleka Ofisi ya Waziri Mkuu na Waziri Mkuu akaleta madaktari mabingwa kutizama uhai wa binadamu ule.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo mimi naomba serikali itowe tamko kwa wafanyabiashara kwa wananchi na wale wachukuliwe sheria inafahamika kontena tusisingizie Dubai...

Mhe. Naibu Spika: malizia mheshimiwa malizia naomba umalizie.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Naibu Spika, kwa taarifa hii fupi nashukuru sana sitaki mjadala lakini tamko la serikali walitoe. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Mhe. Mohammedraza kaja na hoja nzuri na muhimu sana na mwenyewe amesema kwamba hataki ijadiliwe na nadhani hoja hii si ya kujadiliwa lakini kubwa kabisa ambalo amelisema ametaka kauli kutoka serikalini na nadhani kwenye swali ambalo amelijibu Mhe. Waziri wa Afya amesema kwamba matokeo hayo yapo, kwa hivyo serikali inayafanyia kazi ndio ambapo nafikiri ni kauli kubwa ya Mhe. Waziri wa Afya.

Lakini mimi niiombe serikali kwamba suala hili walichukulie umuhimu mkubwa na niombe sana serikali ipo hapa kwamba majibu yaje ndani ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na suala la vyakula vibovu ambavyo vinaingia ndani ya nchi yetu Naomba sana serikali hili walichukuwe na naamini kwamba watalifanyia kazi na hatua kali vile vile tungeliomba kama Baraza hatua zichukuliwe kwa hao watu ambao wanaleta chakula kibovu.

Baada ya kusema hayo hilo nawaachia serikali wenyewe watajua ni muda gani wataweza kuleta majibu ahsante, nashukuru sana naona mheshimiwa anataka kusema machache mheshimiwa karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kama ulivyokwisha kusema kwa niaba ya

Makamu wa Pili wa Rais serikali ipo Barazani na kwasababu tumetakiwa tutowe kauli naomba niseme yafuatayo.

Hoja ya mjumbe tumeisikia au taarifa ya mjumbe tumeisikia na serikali itachukua hatua kwa mfanyabiashara yoyote, kwa mfadhili yoyote ambaye ataleta chakula kisichofaa kuliwa na binadamu nchini na hata vile vyombo ambavyo vinasimamia serikali tunachosema kwamba vile vyombo ambavyo vinasimamia hasa Bodi ya Madawa na Chakula inapaswa kufanya wajibu wake vizuri na serikali ikibaini kwamba ndani ya vyombo na taasisi za serikali wamo watu ambao wanashirikiana na wafanyabiashara kuleta chakula kisichofaa basi serikali haitosita kuchukua hatua na hatua kali za kisheria zitachukuliwza dhidi ya huyo mfanyabiashara pamoja na mtendaji mwengine yoyote wa serikali ambaye atashiriki katika kudhibitisha kwamba ni safi na kumbe chakula sio safi kwa niaba ya serikali naomba niseme hivyo.

Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri.

Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
kwa mwaka 2018/2019
na
Makadirio ya Mapato na Matumizi ya
Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
kwa mwaka 2018/2019

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea nina wachangiaji saba na kama mnavyojua kwamba kanuni zetu zinatutaka tutumie dakika ishirini kwa hivyo naomba mjali sana wakati, mchangiaji wa mwanzo atakuwa Mhe. Bahati Khamis Kombo baada aya hapo atafuata Mhe. Shehe Hamad Mattar na ajitayarishe Mhe. Yussuf Hassan Iddi, Mhe. Bahati karibu.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika na mimi leo kuwa mtu wa mwanzo kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu alijetujaalia kufika hapa tukiwa katika hali ya uzima na wale wenzetu ambao wana matatizo mbali mbali namuomba Mwenyezi Mungu awajaalie awape wepesi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kumtewa Mhe. Waziri wa Fedha kwa juhudi zake kubwa anazozichukua waziri huyu kuona kwamba anazitekeleza yake majukumu aliyopangiwa.

Mhe. Naibu Spika, pia niwapongeze sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na watendaji wake wote niwapongeze wenyeviti wetu wote wa kamati za sekta kwa mashirikiano makubwa waliyonayo ambayo na sisi tuliweza tukaa na Waziri wa Fedha pamoja na wao kuijadili bajetu yetu hii na leo iko mbele yetu.
Mhe. Naibu Spika, mimi nianza tu moja kwa moja katika ukurasa wa 31 lakini nitasoma kipengele cha chini kinasome kwamba serikali imependekeza kurekebisha sheria ya ushuru wa stempu kwa kufuta ushuru huo kwa uingizaji, usambazaji na uuzaji wa bidhaa za mchele na unga wa ngano nchini ili kutoa unafuu zaidi kwa bei za chakula.

Mhe. Naibu Spika, suala hili nalipongeza sana kwa sababu hawa wananchi ambao wana kipato cha chini wataweza kufanya juhudi zao kubwa ili kuendeleza maisha yao katika majumba yao, lakini pia Mhe. Mwenyekiti hapa tumeona kwamba kuna marekebisho mengine yanayopendekezwa katika sheria hii na kufuta kwa ushuru wa stempu kwenye tiketi za ndege zinazotolewa na mashirika ya kimataifa hapa Zanzibar kwa kusafiri nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, tunaipongeza sana serikali yetu kwa kuliona hili tunaamini kwamba hata yule mfanyakazi wa chini ataweza kutembea sehemu mbali mbali na bila ya kutolewa ushuru wa aina yoyote hili ni jambo jema tunaipongeza sana serikali yetu.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia niende moja kwa moja katika TRA na ZRB kwa kweli wemechukuwa juhudi zao kubwa kukusanya mapato tunawaomba kwamba waendelee zaidi kukusanya mapato haya ili serikali iweze kuifanya mambo yake kwa ufanisi zaidi. Lakini pia naamini kwamba juhudi hizi zote zimefanywa na Mhe. Waziri kwa kusimamia kwa kina ili tuweze kwenda kwa wakati na tuache ile tabia ya kurudi nyuma ili tuweze kuimarisha juhudi zetu kubwa kuleta maendeleo kwa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja sasa katika Shirika la Meli. Mhe. Naibu Spika, tumeomba kwamba sasa hivi tunataka kuleta meli zetu mpya lakini pia tunaiomba serikali kwamba tuendelee kuwa na juhudi kubwa zaidi ili kuweza kuzisimamia zile meli zetu. Tumeona huko nyuma tumepata matatizo makubwa juu ya meli yetu ya MV. Mapinduzi meli iko vizuri lakini kwa bahati mbaya tu imetokea matatizo ambayo hayakuweza kuepukika na hivi sasa wananchi wanaisubiri kwa matumaini mazuri.

Mhe. Naibu Spika, tuseme tu kwamba jambo lolote unapo lisimamia vizuri basi linaendelea lakini ikiwa jambo hukulisimamia vizuri basi jambo lile linaweza kufa mara moja na kutia hasara serikali. Mhe. Waziri wetu wa Fedha tunamuamini na tunamuona kiasi gani juhudi zake ambazo anazithamini kwa Wazanzibari wote.

Mhe. Naibu Spika, nisemee kuhusu bandari tumeona kwamba hivi sasa bandari yetu ya Malindi imekuwa ndogo lakini pia tumeamua kuijenga bandari ya Mpiga duri, lakini niseme tu kwamba isiwe bandari ya Mpiga duri tu kwa sababu hivi sasa tumeona wafanya biashara wamekuwa wengi Unguja na Pemba. Niombe tu kwamba bandari zetu iliyoko Wete, iliyoko Mkoani basi iweze kutanuliwa ili wafanyabiashara wale waweze na wao kuleta makontena yao pale na waweze kupunguziwa ule ushuru mkubwa ambao unahitaji kutolewa.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa niwaombe wajumbe wote wa Baraza la Wawawakilishi tumuunge mkono Mhe. Waziri wa Fedha na tuipitishe ripoti hii kwa asilimia mia moja ili aweze kutekeleza majukumu yake yote. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Bahati Khamis Komba mchangiaji anayefuata ni Mhe. Shehe Hamad Mattar baada ya Mhe. Shehe Hamad Mattar atafuata Mhe.Yussuf Hassan Iddi ajitayarishe Mhe. Masoud Abrahman Masoud.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima tukaweza kufanya shughuli zetu kama tulivyozikusudia.

Mhe. Naibu Spika, shukurani za pekee zikufike wewe Naibu Spika ambaye umeniruhusu niweze kuwajibika kwa kuchangia hotuba hii ya Bajeti ya Serikali, chini ya Waziri wa Fedha na Mipango ambaye ni waziri mahiri Dkt. Khalid Salum Mohamed.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na shukurani zangu nawashukuru sana wajumbe kwa jitihada zao ambazo wameonesha katika kuchangia bajeti zetu za serikali tokea mwanzo hadi mwisho, lakini nina masikitiko kuona kwamba tumekuwa tukianza vizuri bajeti zote tatu hizi lakini tumepata msiba kidogo wa kuondokewa na mheshimiwa mwenzetu ambaye tunampenda Mhe. Abdalla Maulid Diwani lakini ni ajali iliyotokezea na ajali haina kinga, na pia ni fundisho kwa sisi wengine ambao tunaendelea na chombo hiki. Lalomo nimuusiea mwenzetu huyu wasia wangu aendelee kuwa mtulivu na kutii adhabu ambayo amepewa asichoke kwani anaweza kwenda kupiga goti kwa mzee wake baada ya adhabu aliyopewa na akaweza kumuhurumia, kwani mtoto akinyea kiganja hakikatwi kinakoshwa. Ni imani yangu kwamba ataendelea kuwa mtulivu na raia mwema.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo niende kuchangia kwenye taarifa ya Kamati ya Bajeti iliyowasilishwa hapa juu ya makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2018/2019. Niipongeze sana Kamati ya Bajeti kwa juhudi kubwa sana iliyofanya ikishirikiana na Wenyeviti wa Baraza pamoja na Wajumbe wenyewe wa Baraza la Wawakilishi. Pia niwashukuru wale wananchi ambao walikuwa wanaitwa na Kamati hii ya Bajeti kutoa mawazo yao na michango yao kuhusu mwenendo mzima wa serikali na michango ambayo wameitoa jinsi gani serikali itaweza kupata mapato na namna gani itaweza kutumia. Michango yao ilikuwa ni mizuri na yenye busara na walikuwa wanaitoa kwa nia safi kabisa.

Ni imani yangu kwamba wataendelea kufanya hivyo na nawapongeza popote walipo wanasikia waendelee kufanya hivyo, hii ndio itakuwa bajeti shirikishi ya wananchi. Kwa sababu hapo nyuma walikuwa wanalalamika kwamba mawazo yao watu hawa wanaitwa hapo Barazani lakini hayafanyiwi kazi. Niipongeze sana serikali kupitia Waziri wa Fedha na Mipango kwamba yale ambayo tunashauri Kamati ya Bajeti kwa kushirikiana na wenzetu hawa tayari yamefanyiwa kazi na matokeo yake ndio haya. Bajeti ya leo ni

bajeti ya wananchi imewagusa kila sehemu katika huduma za kijamii ambazo zimeonesha kama vijana imewagusa, wana michezo, sekta za afya, maji na nyenginezo.

Mhe. Naibu Spika, hii ni bajeti ya wananchi naipongeza sana kamati kwa kuibua mambo mbali mbali ambayo tayari yameleta matumaini. Kwa hivyo, sasa tuendelee kushirikiana na watu kama hawa kwa lengo la kufanikisha nchi yetu izidi kupiga hatua.

Baada ya hapo niende katika ukurasa wa 11 kwenye suala zima kuhusu pato la mwananchi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza katika bajeti hii inaonesha safari hii tayari wananchi wameona kwamba kuna ongezeko la kipato hii ni ishara njema, kwa kweli inaonesha tayari ukiangalia katika nchi yetu kuna mabadiliko ya wananchi jinsi wanavyotumia mapato haya kwa kuboresha shughuli zao za maisha. Ukiangalia hata katika mambo ya makaazi ni nyumba ndogo ndogo sana ambazo wana ujenzi ule wa kizamani, wengi wao wanajenga nyumba ambazo ni za kisasa kwa kutumia vyanzo vya kudumu kama matufali na bati, hii ni ishara ya kukua kwa mapato.

Pia tayari wameweza kuangalia kwa mambo ya usafiri yote haya ni kuonesha kwamba mapato yao ya mtu mmoja mmoja yameongezeka na yataongezeka pindipo yale mambo manne yakifanyiwa kazi zaidi ambayo ndio yaliyotufikisha hapa. Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alitueleza kwamba ili tuendelee lazima tuwe na mambo manne. Watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Mhe. Naibu Spika, mambo haya manne ndio yaliyotufikisha hapa, watu wako huru, ardhi tunayo tunaitumia, siasa safi tunaongozwa hapa na Chama cha Mapinduzi ndio tunayoendelea nayo, utawala bora ukisimamiwa na Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein ni kinara wa utawala bora na ndio tukaweza kufikia hapa. Nchi iko salama kila mmoja anafanya shughuli zake kwa amani kabisa ndio tukaweza kuongeza kipato hiki.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa Nam.13 kwenye kitabu hiki cha bajeti alipozungumza suala zima la kuongezeka bidhaa za kutoka nje. Bidhaa zinapoingia kutoka nje kwa kweli zinalazimisha kutumia dola na mahitaji ya dola yanaongezeka, hivyo inaathiri pesa zetu zilizomo ndani ya nchi zinatumika kwa wingi. Kwa hivyo, ili tuweze kulinusuru jambo hili nina shauri sana suala la kutafuta wawekezaji watakaoleta viwanda hapa nchini ambavyo vitaweza kufanya ile kazi ya kununua bidhaa za nje kama vile vyombo vya moto vilivyokuwa vinanunuliwa hapa, vipuri, vitu vya umeme tayari naona kama kuna ishara ya wawekezaji ambao wanaweza kutaka kutengeneza hapa tuwatengenezee mazingira yaliyo bora waweze kuekeza hapa ili tuweze kunusuru zile fedha ambazo zingeweza kununulia bidhaa kutoka nje.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni suala zima la biashara ya Zanzibar na Tanzania Bara. Kwa kweli inaonesha katika taarifa hii hapa biashara ya Zanzibar imedorora kwenda Tanzania Bara kiasi ambacho imefika chini ya asilimia 50, ni bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara. Jambo hili sio zuri wakati huko nyuma nchi kama hii enzi ya Dkt. Salmin

Amour Juma wafanyabiashara walikuwa hapa wamefanya ni kitovu cha biashara, lakini leo imekuwa kuna vikwazo ambavyo wafanyabiashara wanavunjika moyo na kuna vikwazo ambavyo sio vya lazima vinavyowekwa kwa wafanyabiashara wa Zanzibar kupeleka bidhaa zao. Najua kwamba Wizara ya Biashara na Viwanda imeshaweka mikakati mizuri kwa hivyo hili jambo waliwekee mikakati ambayo itaondoa hizi kasoro nchi yetu hii ya Muungano wazee wetu hawa wawili waliofanya Muungano walisema kwamba hii nchi ya Zanzibar ni ndogo, lakini watu wake wataongezeka.

Kwa hivyo, ili tukiungana watapata fursa wenzetu hapa kwenda kuuza bidhaa zao kule na kufanya shughuli zao nyengine za kiuchumi. Lakini hii azma hii kuna wengine wanaipinga Mhe. Naibu Spika, naomba sana, sana wakumbuke wazee hawa wamekufa lakini mawazo na busara zao bado zipo na zinaendelea kufanyiwa kazi. Kwa hivyo, tuzitunze na tuziheshimu.

Mhe. Naibu Spika, ongezeko hili la kuona kwamba vitu mpaka kufikia asilimia TSH 84.7 bilioni hadi kufikia 33 bilioni mwaka 2017. Kwa kweli ni ishara mbaya tusingependa nchi moja ambayo inatumia sarafu moja, Muungano mmoja uliokuwa madhubuti unafanya mambo kama haya. Naomba sana Mhe. Naibu Spika, waziri wanaohusika na mambo haya wayafanyie kazi mambo haya tuone kwamba yanaleta tija ya nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, niende katika suala zima la ukurasa wa 14 mambo ya uingiaji wa watalii. Hapa taarifa ya hotuba ya bajeti inaeleza kwamba wameongeza watalii kutoka 376,242 hadi 433,474. Tunasema kwamba sekta ya utalii kweli ndio inatuongoza katika mapato yetu, lakini je hakuna mianya ambayo kuwa inapoteza? Bado kuwa na idadi kubwa ya watalii hakujasababisha kwamba ndio kuongezeka kwa mapato. Mimi nataka atakapokuja Mhe.Waziri atwambie hili ongezeko katika pato la taifa limeweza kuongezeka kiasi gani hawa watalii. Kwa sababu hawa watalii sasa hivi wengine wana ujanja au wana utaratibu wanautumia kufanya malipo wanakotoka. Malipo makubwa wanayafanya kutoka nchi wanazotoka kwa mawakala wao hapa wanakuja kumalizia matumizi. Sisi tunaambulia pesa za kununulia ndogo ndogo tu pipi pipi. Kwa hivyo, matumizi kama haya kama yangefanywa ndani ya nchi hii tayari tungeweza kunyanyua zaidi uchumi wetu. Naomba kama kuna marekebisho yakufanya matumizi yafanywe hapa, basi yafanyike au kujua namna gani tutagawana mapato yale ambayo yanakusanywa kule kupitia watalii wanaokuja hapa.

Mhe. Naibu Spika, niende katika suala zima la ugharamiaji wa mpango wa maendeleo. Kwa nini fedha zilizotengwa katika mpango huu wa maendeleo zimefika chini ya asilimia 50? Utakuta kwamba fedha za maendeleo ni muhimu sana maana hiyo ndio *asset* ya nchi. Sasa tukiangalia kuwa zimetengwa fedha nyingi lakini kutolewa kwake kumekuwa na uhafifu. Naomba sana, sana tuangalie suala zima la fedha za maendeleo kuzipa kipaumbele, kama tunavyotoa kipaumbele vitu vya maendeleo basi ziwe kwa ukweli, isiwe tunasema ni kipaumbele lakini ikifika wakati wakati wa kuzipa fedha hatutoi fedha katika hili ni hasara kwa kweli. Na nataka kujua ni kitu gani kinachosababisha wale washirika wa maendeleo na wao hawakutoa zile fedha wakati wao wenyewe walishaahidi kwamba watatufidia kiasi hiki, lakini sijui kulitokezea nini?

Naomba Waziri wa Fedha na Mipango atakapokuja atueleze ni kitu gani ambacho kuwa kimesababisha kwamba washirika wa maendeleo wasiweze kutupa fedha zile walizokusudia.

Mhe. Naibu Spika, niende katika suala zima la kuimarisha kilimo cha kujenga miundombinu ya umwagiliaji maji, uvuvi na mifugo. Shughuli ya uhifadhi wa maji ya mvua kwa ajili ya umwagiliaji maji, ujenzi wa matuta, Uzini, Muyuni Unguja na Msaani kwa Pemba. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mimi ni shahidi kwamba shughuli hii inaleta tija, nikiwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Katibu Mkuu na uongozi mzima wa kilimo tuliondoka hapa tukenda Pemba tukaweza kutembelea bonde la Msaani tukaona wale ambao wameitikia wito huu wa kukinga maji ya mvua kuyatumia kwa kilimo faida yake ipo. Tumeona mpunga umenawiri vizuri na wale ambao hawakufahamu au wamepinga tumeona athari yake. Sasa hivi nina taarifa kwamba kuna mipunga inaanza kukauka na nikiuliza naambiwa ni wale ambao hawakuingia katika mpango huu.

Ni imani yangu kwamba Wizara ya Kilimo itaendelea kutoa elimu kwa wale wakulima ambao bado hawajataka kujiunga na mpango huu. Na niwapongeze sana Maafisa wa Kilimo baada ya kuona kwamba ule mpango walioupanga katika bonde la Msaani ni kwamba hawakutimiza wakaweza kuwahamasisha watu wa bonde la Kiungoni Mchangamdogo. Wenzetu hawa wameupokea mradi huu, ni mradi mzuri una muhagharamia mkulima pembejeo zote na gharama zote na bado wengine wameukataa, lakini walioupokea wameona faida yake. Mimi ni shahidi tumekwenda tukaona mpunga umenawiri nawaomba wananchi wanaonisikiliza mpango huu waukubali serikali haiwezi kusema jambo lake kwa wananchi wake ikawa ina nia mbaya, ni mpango mzuri utasaidia sana katika kilimo chetu badala ya kutegemea mvua moja kwa moja.

Mhe. Naibu Spika, nina masikitiko katika suala zima la huu utengenezaji wa miundombinu ya umwagiliaji maji ambayo imetengeneza mita 480 kwa misingi ya umwagiliaji maji ya saruji imejengwa katika kisiwa cha Unguja mita 480, lakini kwa nini Pemba hakuna hata mita 100? Naomba kujua kitu gani kilichosababisha kwamba jambo hili lisiwepo na hawa ni watoto mapacha. Hili jambo sio zuri.

Mhe. Naibu Spika, niende katika masuala ya MTAMBUKA na udhalilishaji. Mhe. Naibu Spika, kutokana na janga litofukia nchini mwetu naipongeza sana serikali kwa kuona jambo hili ni muhimu sana na kuzindua mpango wa miaka mitano wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto. Mhe. Naibu Spika, na wanaume sasa hivi wanadhalilishwa sio wanawake peke yake na watoto.

Mhe. Naibu Spika, pia kwa kuwa na kamati 24 za Unguja na Pemba kupinga ukatili na udhalilishaji na kujengewa uwezo wa kazi zao. Hili ni suala muhimu sana kwa sababu hii shughuli ya udhalilishaji na ukatili inatakiwa tufanye kazi kwa pamoja. Serikali imeamua kufanya hivyo pamoja na kushirikisha vyombo vya dini vimeweza kupewa uwezo kwa Wilaya zote, naomba sana, sana iendelee kufanya shughuli hii na kwa pamoja tutafika.

Mhe. Naibu Spika, niende katika mwelekeo wa uchumi wa Zanzibar 2018. Nakubaliana na mpango huu wa Dira ya Maendeleo ya 2020 MKUZA III pamoja na utekelezaji wa ilani ya CCM ya mwaka 2015. Kwa kweli pato la taifa limeongezeka na linatarajiwa kuongezeka kutoka 7.5 mpaka 7.7. Hii inawezekana na itawezekana baada ya kutekelezeka mambo ambayo yalitajwa katika ukurasa wa 37 na kifungu cha 48, pamoja na shabaha na malengo ya mapato ya kodi ya mwaka 2018/2019.

Mhe. Naibu Spika, ili tufikie huko kuna mambo ya kuangalia tena kwa uono mkubwa nayo ni kama yafuatayo.

Mhe. Naibu Spika, kuendelea kuibua vyanzo vya mapato vipya, kuimarisha na vile vikongwe ambavyo tumeanza kuviona vinaleta tija. Lakini pia vile vile usajili wa umiliki wa vyombo vya nchi kavu kama vya usafiri tumeviona hapa fedha zilizoingia katika masuala ya mali zisizohamishika zimeingizwa fedha nyingi sana…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakisha dakika tano.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Pia nashauri kwamba kuna vyombo vya baharini navyo vinakuwa sijui umiliki wake ukoje, navyo viangaliwe katika sehemu hii ya kuweza kupata mapato na wao wasajili vyombo vyao kama vile walivyofanya vyombo vya usafiri wa nchi kavu.

Mhe. Naibu Spika, suala zima la taasisi yetu hii ya *TRA* na *ZRB*, hizi ni taasisi zinatoa mchango mkubwa sana katika mapato yetu lakini naomba sana, sana *TRA* bado kuna harufu ya upoteaji wa mapato. *TRA* naona hapa inahitaji Mhe. Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. John Pombe Joseph Magufuli aweze kuja hapa atumbue majipu maana kuna watu bado Mhe. Naibu Spika, hawataki waguswe na wao ni wachangiaji wazuri wa mapato, lakini bado kuna watu wanawaogopa, hawa watu ni hatari kuona kwamba mapato yetu yanapotea. Naomba sana uangaliwe tena uongozi mzima na utaratibu mzima wa mapato uliopo *TRA*.

Mhe. Naibu Spika, pia tuangalie sehemu za bandari vile vile mapato yanapotea, pia na kuongeza bandari nyengine kama alivyotangulia mwenzangu hapa Mhe. Ali Suleiman Ali hizi bandari tusione ni ndogo ndogo zikiwepo zitaweza kutuzuilia yale magendo na kutuongezea mapato japo ni kidogo kidogo ziboreshwe.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango wale wafanyabiashara maarufu wa humu nchini je ulipaji wao wa mapato ukoje, kwa sababu wengine wana ubabaishaji. Mtu ana kampuni kama tano zinapata msamaha akiona kampuni hii imemaliza muda fedha zake ahamishia katika kampuni inayoendelea, huu ni ujanja fulani. Lakini waangaliwe je wanalipa vipi *cooperative tax* inalipwa inavyotakiwa? Sawa ni sehemu ambazo wao wataweza kupata mapato kuona kwamba serikali inaongeza nguvu yake.

Mhe. Naibu Spika, misamaha ya kodi inayotolewa iangaliwe vipi inaleta faida kwa wananchi, kwa sababu tumeona hapa mwezi wa Ramadhani imetolewa misamaha lakini

wananchi hawakufaidika. Ukiuliza kitu kile mfanyabiashara anayeuza anakwambia mimi nimepokea hivi kutokana na mimi nilivyouziwa na mimi nauza hivi. Sasa kwa hivyo ule msamaha haukuleta faida tuangalie sana makampuni hayo ili kuona yanaweza kusaidia katika mchango wetu wa kila siku. Mhe. Naibu Spika, kuimarisha mfumo mzima wa upokeaji wa mapato wa mashine zile ni sehemu moja wapo ambayo itaweza kutusaidia kuona mapato hayapotei.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa nimuombe sana Waziri wa Fedha na Mipango katika kupunguza matumizi. Mhe. Waziri wa Fedha kuna utaratibu kuona fedha zinatoka kwa ajili ya maposho ya viongozi kama suala la mafuta. Suala la mafuta katika taasisi zetu kuna viongozi wanapewa posho la mafuta lakini hawazitumii, ukweli ndio huu hawazitumii. Waziri au Katibu Mkuu au Mkurugenzi anaweza akapewa posho la milioni moja na laki tano lakini anarudi kwenye mafuta ya *OC*. Hapa tunarudi nyuma aangalie sana Waziri wa Fedha na Mipango jambo hili lipo tunatokea huko huko tunayaona.

Mhe. Naibu Spika, mwisho niombe katika vipaumbele alivyotoa Mhe. Waziri naomba sana kuna masuala ya ununuzi wa boti ya uokozi hata Shirika la Bandari ilisema itanunua boti ya uokozi. Naomba sana niishauri serikali hata kama mwaka huu haikununua lakini iweze kununua *helicopter* ya uokozi ni muhimu sana. Tumeona wakati wa ajali ilipotokezea ya meli *helicopter* ilieweza kutoa taarifa sehemu gani watu wapo na hii itaweza kusaidia haraka lakini pia kwa ulinzi wa nchi yetu na ulinzi wa bahari yetu kuu ambayo sasa hivi inagharamika kwa kukodi ndege kulinda baharini baadhi ya siku. Kwa hivyo, ni imani yangu kwamba tukifanya hivi tutaweza kusaidia katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, mwisho niunge mkono na niwapongeze sana wale ambao walifanya juhudi hii lakini tuendelee kushikamana naunga mkono hoja hii mia juu ya mia na nawaomba wenzangu waweze kuipitisha hoja hii bila ya mabadiliko. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Shehe Hamad Mattar mchangiaji anayefuata ni Mhe. Yussuf Hassan Iddi baadae ajitayarishe Mhe. Masoud Abrahman Masoud baadae tutampa nafasi Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi ya kutoa mchango wangu katika Bajeti hii ya Serikali ambayo iko mbele yetu kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) kwa kunijaalia uzima na afya njema na leo hii nimesimama katika Baraza lako hili tukufu kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu ya kawaida.

Pili, nishukuru sana, nitumie fursa hii kumshukuru sana Spika wetu wa Baraza la Wawakilishi, wewe Mhe. Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza, Katibu wa Baraza, Wajumbe wote wa Baraza hili tukufu pamoja na wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi kwa michango na dua mbali mbali ambazo wameniombea ili afya yangu itengemae na nashukuru sana sasa niko vizuri *Alhamdulillah*.

Lakini la tatu, nitumie fursa hii kuwashukuru sana wananchi wangu wa jimbo la Fuoni kwa kuwa na subira, utulivu kwa kipindi chote cha mitihani na ninawaambia kwamba nimesharejea na naendelea kutekeleza majukumu yetu kama kawaida. *(Makofi)*

Nne Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati yangu ya Fedha, Biashara na Kilimo nichukue fursa hii kuwashukuru sana mawaziri wote na manaibu mawaziri kwa mashirikiano ya hali ya juu tokea tulipoanza hadi hii leo. Lakini shukurani za pekee zimwendee Waziri wa Fedha na Mipango ambaye yumo katika kamati yetu, Waziri wa Biashara na Viwanda pamoja na Naibu Waziri wake na Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kipindi kile Mhe. Hamad Rashid na Naibu Waziri wake Mhe. Lulu Mshamu Abdalla na sasa hivi ni Mhe. Rashid Ali Juma na Mhe. Dkt. Ali Makame.

Kwa kweli kamati yetu wameipatia mashirikiano ya hali ya juu na kuweza kumaliza kazi zetu kwa salama na amani. Tunawatakia kila la kheri mawaziri wote waendelee kuchapa kazi na waendelee na juhudi ili mafanikio haya ambayo yamepatikana katika mwaka huu wa 2016/2017 basi ya mwaka 2017/2018 vile vile yapatikane katika mwaka wa fedha ujao ambao tutauanza hivi punde mwaka 2018/2019.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo mfupi sitokuwa na michango mingi sana kwa sababu Waheshimiwa wengi tayari mambo mbali mbali wameshayazungumza kwa hiovyo mimi nitavitia baadhi ya vipengele ambavyo nahisi kwamba ipo haja ya kuweza kuvitolea mchango.

Mhe. Naibu Spika, nianze na suala la mapato, tuipongeze Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kutekeleza kwa vitendo ahadi yake ya kukusanya shilingi 800 bilioni kabla ya mwaka 2020. Ni dhahiri kuwa muongozo wake mbali mbali aliokuwa akiitoa iliyojaa hekima na busara. Hiyo ndio iliyotufikisha leo mwaka ujao wa fedha 2018/2019 basi tunategemea kukusanya shilingi 800,000,007. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba mwaka huu mambo yatakuwa mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa mapendekezo haya ya kitabu cha bajeti mapato ya ndani yanaendelea kuimarika kila uchao. Hadi kufikia Machi, 2018 mapato ya ndani yamefikia shilingi 506.6 bilioni sawa na asilimia 74.7, haya ni mafanikio mkubwa sana ambayo yamepatikana.

Mhe. Spika, Naibu Spika, mapato haya ya ndani yameletwa katika maeneo makubwa mawili, Kuna mapato ya ndani ambayo ni ya kodi, yanayohusiana na kodi na mapato ambayo na yasiyokuwa na kodi. Nigusie kidogo kwenye haya mapato ambayo sio ya kodi.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Machi, mapato yasiyokuwa na kodi yamefikia shilingi 41.4 bilioni sawa na asilimia 113, kati ya shilingi 36.6 bilioni ambapo zilitarajiwa kupokelewa katika mwaka wa fedha 2017/ 2018. Kwa kweli tuwapongeze sana wenzetu wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa juhudi mbali mbali ambazo wanazozichukua kuhakikisha kwamba suala la kuimarisha mapato hasa haya yasio ya kodi yanaongezeka kila uchao. Juhudi hizi zimekuja kutokana na kuanzishwa pale kitengo maalum cha

revenue ambapo sasa taasisi zote za serikali zinapitia moja kwa moja Wizara ya Fedha kwa hivyo, tuwapongeze sana lakini tumuombe Mhe. Waziri na Mhe. Waziri wa Fedha ni msikivu akiombwa anaombeka.

Katika kitengo hiki cha *revenue* pamoja na kile cha matumizi, kwa sababu kuna vitengo viwili pale, kuna kitengo kinachohusiana na matumizi ya serikali na kitengo kinachohusiana na makusanyo ya fedha za serikali. Sasa katika vitengo hivyo viwili kwa kweli hawa wafanyakazi wanafanya kazi kubwa sana na ndio maana sasa hivi tumefikia mafanikio ya kukusanya fedha hizi ambazo zimo kwenye kitabu hiki cha bajeti. Basi tumuombe Mhe. Waziri kwamba watendaji hawa wa vitengo hivi viwili vya mapato na matumizi basi wapate *training* kila uchao, kwa sababu wanatumia masuala ya mitandao na masuala ya mitandao kila siku yanabadilika.

Mhe. Naibu Spika, tukitizama kwa upande wa kitengo cha matumizi tulianza na *article* 7 lakini baadae sasa tunakwenda kwenye *article* 10. Kwa hivyo, ukitizama *article* 7 na 10 ziko tafauti kiutendaji bila ya *training* ni ngumu. Kwa hivyo, tumuombe Mhe. Waziri watendaji hawa wapatiwe elimu ili waweze kuwa na ufanisi zaidi. Vile vile ipo haja ya kuangalia zaidi kwenye masuala ya posho ili kuwajenga ari zaidi ya makusanyo na wawe wana *moral* ya kutosha katika ufanyaji wao wa kazi.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa mapato ya nje hadi kufikia Machi, 2018 serikali imekusanya shilingi 151 bilioni sawa na asilimia 22.3, sasa hivi zinasimamiwa na kuratibiwa na Idara ya Fedha za Nje. Kwa hivyo basi, tuwaombe watendaji wa Idara ya Fedha za Nje waongeze ubunifu katika kazi zao hizi za kuratibu na kusimamia na watumie lugha ya ushawishi kwa wafadhili mbali mbali ili basi, makusanyo katika mwaka wa fedha ujao 2018/2019 ya shilingi 464.1 bilioni basi angalau tuweze kufikia kwenye asilimia.

Hili Mhe. Naibu Spika, inawezekana iwapo tutajituma na kuongeza bidii. Fedha nje zipo lakini zinahitaji mipango mizuri na ufuatiliaji. Kwa hivyo, tuwaombe wenzetu hawa wa Idara ya Fedha za Nje wajifunge mkaja ili kuhakikisha basi mapato haya ya nje yanaongezeka kutoka shilingi 151 bilioni kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na angalau tupate asilimia 50 na tuondoke na hii asilimia 23 ambayo ipo.

Pia nitakuwa sikuwatendea haki taasisi mbali mbali ambazo zina majukumu ya kukusanya mapato. Kwanza kabisa tuwapongeze sana wenzetu wa *TRA* kwa mwaka uliopita wamekusanya shilingi 190.5 bilioni sawa na asilimia 99 ya shilingi 193.2 bilioni. Kwa kweli wenzetu wa *TRA* wamefanya kazi kubwa sana na wanastahiki kupongezwa.

Halkadhalika wenzetu wa *ZRB* wamekusanya shilingi 258.9 bilioni sawa na asilimia 96 kwa makadirio ya shilingi 269.5 bilioni. Kwa hivyo, haya ni mafanikio mazuri kwa taasisi zetu hizi mbili, tunataka na mwakani tuje tuwapongeze kwa sababu mwakani tumewapa jukumu kubwa wenzetu hawa kwa hivyo, na wao tunawataka waongeze bidii na juhudi, tunawaamini sana watendaji wa taasisi hizi mbili *TRA* na *ZRB* ili basi makisio ya mwaka wa fedha mpya wa 2018/2019 ya shilingi 301.1 bilioni kwa upande wa *TRA* na shilingi 485.4 bilioni kwa upande wa *ZRB* yaweze kufikiwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa matumizi ya serikali, hadi kufikia Juni matumizi ya serikali kwa ujumla yamefikia shilingi 865.1 bilioni sawa na asilimia 80 ya makadirio ya shilingi tirilioni moja na bilioni 87.4. Tuipongeze serikali kwa kufanya *saving* katika matumizi yake na hii ni dhahiri kwamba ile ahadi ya Mhe. Rais aliyoisema ya kubana matumizi yasiyokuwa ya lazima hapa imefikiwa. Kwa hivyo, tumefanya *saving* matumizi tumefikia asilimia 80, asilimia 20 tume-*save*. Kwa hivyo, tumuombe basi Mhe. Waziri hasa katika mwaka huu wa fedha ambapo tumekusudia kutumia trilioni moja na 315 bilioni basi nazo tufanye *saving* ili kwa ajili ya kufanya matumizi mengine. Lakini vile vile nishauri tu kwamba, katika matumizi haya ya serikali tujitahidi sana kuzingatia *value for money* ili lile lengo lililokusudiwa la matumizi haya ya pesa yaweze kufikiwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa matarajio ya Mpango wa Maendeleo mwaka 2017/2018 hadi kufikia Juni shilingi 305.9 bilioni zinakusudiwa kutumika hadi kuishia mwezi huu wa Sita. Pesa hivi Mhe. Naibu Spika, zilikusudiwa kutumia programu 27 pamoja na miradi 46, basi tumuombe Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango atapokuja kufanya majumuisho yake basi atueleze katika hizi programu 27 katika mwaka wa fedha 2017/2018 ni programu ngapi zimeweza kutekelezwa na miradi hii 46 ni miradi mingapi ambayo imetekelezwa. Katika miradi hiyo ambayo imetekelezwa ni miradi mingapi tayari imeshakamilika katika kipindi hiki cha mwaka 2017/2018, miradi mingapi imo kwenye *progress* yaani inaendelea na miradi mingapi ambayo haikutekelezwa.

Mhe. Naibu Spika, tumuombe Mhe. Waziri wa Fedha atakapofanya majumuisho basi atupatie mchanganuo wa programu na miradi mbali mbali ambayo imekusudiwa kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 katika fedha za mipango ya maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa deni la taifa tumeshuhudia kuongezeka kwa deni hili la taifa kutoka shilingi 371.1 bilioni mwezi Machi, 2017 hadi kufikia shilingi 519.7 bilioni mwezi Machi, mwaka 2018. Kwa mujibu wa takwimu tumeambiwa kwamba deni letu halitishi, kwa mujibu wa takwimu na kitabu hiki tumeambiwa halitishi ni himilivu kwa asilimia 16.8 na tunayo fursa ya kuweza kukopa zaidi. Tutoe ushauri basi tuli-*manage* vizuri deni letu hili na tudhibiti kiwango hiki cha uvumilivu wa deni ili tusije tukapindukia ile asilimia zaidi ya 51 ya pato letu la taifa.

Pia Mheshimiwa nilikuwa nataka kujua, kwa vile...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiwa na dakika tano.

Mhe. Yusuf Hassan Idd: Naomba uniongeze na tano ili nipate kumalizia. Nataka kujua kwamba tumeelezwa kuwa deni letu ni la ndani na nje, lakini vile vile kuna deni la muda mrefu na muda mfupi. Sasa Mhe. Waziri wa Fedha atakapokuja ilikuwa atueleze katika deni hili la shilingi 519.7 bilioni je, ni kiasi gani deni hili la muda mrefu na kiasi gani deni la muda mfupi na kiujumla wake je deni letu hili tunapaswa kulipa riba ya kiasi gani.

Mhe. Naibu Spika, niende haraka haraka kwa vile muda unatuacha mkono tuje kwenye gawio la *BoT*. Mhe. Naibu Spika, tunajua kwamba serikali yetu inapata gawio la *BoT* la asilimia 4.5 na hadi kufikia Juni, 2018 tunategemea kuzipata hadi kufikia Juni shilingi 13.5 bilioni sawa na asilimia 337.5 ya makadirio ya shilingi bilioni nne. Haya ni mafanikio makubwa lakini hapa Mhe. Waziri atapokuja kufanya majumuisho atueleze kwa nini katika mwaka huu wa fedha 2018/2019 gawio hili la *BoT* limechanganywa makisio yake na gawio la mashirika ya serikali, wakati kwa mwaka 2017/2018 zilikuwa ziko tofauti. Gawio la *BoT* lilikuwa liko mbali makisio yake pamoja na makusanyo yake pamoja na gawio la mashirika. Lakini kwa mwaka 2018/2019 gawio la *BoT* pamoja na gawio la mashirika lote limeunganishwa pamoja na limekuwa shilingi bilioni tisa na wakati makusanyo ni zaidi ya asilimia 300 zaidi ya makusanyo. Kwa hivyo, atueleze kwa nini hapa mwaka wa fedha 2017/2018 tumekadiria pesa kidogo lakini tumepata nyingi, mwaka huu wa 2018/2019 tumeweka pesa kidogo, basi Mhe. Waziri aje atueleze.

Mhe. Naibu Spika, tuziombe serikali zetu mbili SMT na SMZ kwa vile kiwango hiki cha asilimia 4.5 cha gawio la *BoT* ni cha muda mrefu hakiendani na wakati uliopo, basi kwa kupitia ile Tume ya Pamoja ya Fedha wafanye mipango ili tuhakikishe kwamba hii asilimia 4.5 inaongezeka na isiishie hapo hapo.

Vile vile kwa upande wa deni la *ZECO* kwa *TANESCO* tushukuru sana serikali yetu kwa mipango mizuri ya kumaliza deni hili. Kwa kweli deni hili lilikuwa mzigo kwa wenzetu hawa wa *ZECO*, lakini serikali ililibeba deni hili na kwa mujibu wa kitabu hiki basi mzigo huu *ZECO* karibu watautua. Kwa hivyo, tuwashauri wenzetu wa *ZECO* kwamba abebwae hujikaza. Kwa hivyo, wajitahidi sana baada ya deni hili kukamilika wasije wakarundikiza deni jengine miaka inayofuata, tunawaamini sana watendaji wa *ZECO* na tunawaomba wajitahidi mzigo huu wamesaidiwa kwa hivyo, watekeleze majukumu yao ipasavyo ili tusije tukaingia deni jengine katika miaka ya mbele.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kuhusiana na kitabu cha mwelekeo wa hali ya uchumi kuhusiana na thamani ya shilingi. Tumeshuhudia kwamba thamani ya shilingi imeshuka ukiangalia kwenye ukurasa wa 12 kifungu cha 17 shilingi yetu imeshuka kwa asilimia 2.4. Sasa kwa kweli kushuka kwa thamani inaathiri sana ukuaji wa uchumi na hata kuathiri deni letu la taifa. Kwa upande wa ukuaji wa uchumi shilingi hii inaathiri kwa sababu gharama za uzalishaji (*coast of production*) zinakuwa kubwa. Kwa upande wa deni hata ukisoma kitabu hiki cha bajeti ukurasa wa 19 katika sehemu ya deni la taifa kifungu cha 45(4) imeelezwa kwamba, deni la nje athari ya mabadiliko ya kiwango cha kubadisha fedha (*Exchange rate*). Kwa hivyo, *exchange rate* inasababisha kwamba deni liongezeke na *exchange rate* inasababishwa na kutokuwa na uimara wa shilingi yetu. Kwa hivyo, tuwaombe wenzetu wa Wizara ya Fedha kupitia *BoT* wao ndio wanapaswa wana jukumu hili la kuimairisha shilingi yetu ili basi hizi athari za ukuaji uchumi pamoja na deni la taifa lisiwepo. Kwa hivyo, tuombe wenzetu watumie mbinu zao na utaalam wao mbali mbali kuhakikisha kwamba shilingi yetu inaimarika katika miaka ya fedha ijayo na sio kushuka kama ilivyoshuka katika mwaka uliopita wa 2017/18.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Fuoni tunaunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Yussuf Hassan Iddi mchangiaji anaefuata ni Mhe. Masoud Abraham. Samahani kuna mabadiliko kidogo kwa sababu namuona Mhe. Mwenyekiti Mwanaasha ameshaingia na nimeliona jina lake lipo ili nimmalizie yeye halafu baadae atakuja Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na baadae atafuata Mhe. Said Soud Said. Mhe. Masoud Abrahman Masoud karibu.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuendeleza Baraza letu hili.

Lakini la pili ni kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Mawaziri na Naibu Waziri Makatibu Wakuu pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na watendaji wote wa serikali kwa jinsi wanavyosimamia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nichukuwe nafasi ya pekee kumshukuru Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na watendaji wake jinsi walivyoandaa kitabu kizuri cha Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye suala zima la ukusanyaji wa mapato. Mhe. Naibu Spika, niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada zake kubwa kwa kupitia *ZRB* pamoja na *TRA*. Kwa kweli makusanyo yaliyopatikana kwa mwaka huu ni mara mbili zaidi ya Bajeti ya 2016/17. Kwa hiyo, tumpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa jitihada kubwa ambayo wameichukuwa na tukaweza kufanikiwa kwa asilimia hiyo.

Mhe. Naibu Spika, lakini kuna tatizo ambalo limejitokeza kwa wafanyabiashara unapokwenda kununua biashara kwenye maduka bado wafanyabiashara wanakwepa kodi, unapewa virisiti vilivyokuwa havina *TIN number*. Baadhi ya wafanyabiashara wanatoa risiti zenye *TIN number* lakini baadhi ya wafanyabiashara mpaka sasa bado hawatoi risiti zenye *TIN number*. Bahati nzuri ukisafiri ukienda Dar- es Salaam siku hizi unaponunua chipsi kuku basi unapewa risiti ambayo ina *TIN number* unalipa kodi. Leo wafanyabiashara wakubwa hapa Zanzibar unanunua vitu karibu milioni tatu milioni nne lakini kirisiti unachopewa hakiridhishi.

Kwa hiyo, niombe wale watu wa TAKUKURU wale wasiwasubiri wanasiasa tu na hawa wanafanyabiashara wawakamate wanaokwepa kodi. Mhe. Mwenyekiti, kama tutafanikiwa kuiwabana kweli kweli wafanyabiashara hawa ikawa wanalipa kodi naamini ongezeko hili la serikali litaendelea kuwa kubwa zaidi na tutafanikiwa katika masuala yetu ya kimaendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze serikali kwa suala zima la upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo yetu. Tumeiona Bajeti ya Serikali ya mara hii ambao wenzetu

serikali wametafuta mikopo kwenye nchi mbali mbali ili wananchi wake tupate kufaidika kwa maji safi na salama. Lakini bahati nzuri visima vinavyochimbwa vinachimbwa ndani ya Wilaya ya Magharibi A na Magharibi B kwa Mkoa wetu wa Mjini Magharibi. Lakini aghalabu maji huwa yanapatikana mjini zaidi.

Niombe serikali kwenye maji Mkoa wa Mjini Magharibi ambao wafadhili wetu au mikopo tumeipata kutoka India na yale majimbo ambayo yako vijijini na wao tuwekewe visima maalum ambavyo vitakuwa wananchi wetu na sisi tunapata kufaidika kwa maji safi na salama. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, kama ingekuwa si baadhi ya wananchi wenye uwezo kuchimba visima huko mitaani basi tungekuwa tunapata tabu sana.

Niombe serikali niisimamie kwa ukaribu sana ili hizi fedha zilizopo zifanye kazi kwa muda mfupi hata kwa kupitia vikosi vyetu wanaweza wakapewa kazi ya kuchimba misingi na kufanyaka kazi nyengine ili maji yakapatikana kwa haraka zaidi na wananchi wetu wakapata kufaidika.

Mhe. Naibu Spika, jengine niipongeze Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuongeza Bajeti hasa kwenye suala la Kilimo cha Umwagiliaji Maji. Kilimo cha Umwagiliaji maji sasa hivi ukitaka usitake ndio mkombozi. Kwa mwaka huu ambao uliomalizika sasa hivi wakulima waliolima msimu wa masika ongezeko la kipato tumeliona kwa asilimia kubwa sana. Lakini kilichongeza kipato zaidi ni kilimo cha Umwagiliaji maji.

Niombe serikali wanapoamua kuweka miundombinu katika eneo la Umwagiliaji basi walifatilie kwa ukaribu, kuna maeneo mengi kuna miundombinu ya umwagiliaji lakini visima havifanyi kazi na inaonekana kuna *forgery* ya makusudi. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri, Naibu Waziri muwe mnafatilia kufanya ziara za mara kwa mara kwenye maeneo hayo kuzungumza na wakulima ili wakulima waweze kutoa changamoto zao.

Lakini kwenye hilo kuna suala zima usomeshaji wa mabibi shamba na mabwana shamba. Niipongeze serikali kwenye hilo imefanya juhudi ya kusomesha mabibi shamba na mabwanashamba lakini watakapomaliza *course* zao wawe zaidi wanakwenda kwa wakulima. Sasa hivi mageuzi haya ya tabia ya nchi maradhi mbali mbali ya kwenye kilimo yanakuwa yanajitokeza.

Kwa hiyo, yanapojitokeza maradhi ikiwa mabibi shamba na mabwana shamba hawako karibu na wakulima wakulima wanakuwa wanaathirika sana. Jana nakumbuka kwenye masuala na majibu Mhe. Naibu Waziri aliulizwa hapa kuhusu wakulima ambao wamepata maharibiko makubwa ya mipunga yao na yeye akaahidi kuwa serikali itakuwa karibu nao na watawasaidia. Niiombe serikali iwaangalie wakulima ambao wameharibikiwa sana na mazao yao kwa mwaka huu.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye suala zima la barabara. Niipongeze serikali kwa barabara ambazo zimetajwa kutoka Bububu kwenda Mkokotoni. Lakini na zile za Pemba ambazo serikali tayari imeshaweka mkataba na watu wameshaanza kazi. Ni suala muhimu sana ambalo litakuza uchumi wetu. Lakini niiombe serikali barabara nyingi ambazo zinajengwa zikinyesha mvua kubwa zinaharibika inaonekana ziko chini ya kiwango. Kwa

hiyo, tuiombe serikali isimamie kwa karibu wakati wa ujenzi ili tusiwe tunakabidhiwa barabara muda wa miaka mitano tayari kumeshachimbika na hatima yake inakuwa hazipitiki.

Lakini nimpongeze Mhe. Waziri wa Mawasiliano kwa kazi nzuri ambayo sasa hivi tunaona baadhi ya wafanyakazi wanafanyakazi ya kuziba ziba mashimo ambayo yako katika barabara za mjini hapa.

Mhe. Naibu Spika, nichukuwe nafasi hii kuipongeza serikali kwa kuamua kuwasaidia *ZECO* kulipa deni ambalo tunadaiwa na wenzetu wa Tanzania Bara. Mhe. Naibu Spika, deni hili lilikuwa kubwa serikali imejitahidi kusaidia kulipa na wenyewe *ZECO* wanajitahidi kulipa. Lakini bado serikali kupitia wizara na taasisi mbali mbali kuna madeni makubwa ambayo tunadaiwa pamoja na wananchi pengine na Waheshimiwa waliomo ndani. Niwaombe wananchi serikali pamoja na taasisi ziweze kuwalipa *ZECO* ili wapate nguvu zaidi ya kwenda kumalizia hilo deni ambalo lililopo sasa hivi.

Mhe. Naibu Spika, nizungumzie suala la uwajibikaji na hasa suala la Wizara ya Afya. Mhe. Naibu Spika, mara hii serikali imeamua ...

Mhe. Naibu Spika. Mheshimiwa Mjumbe, Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Naibu Spika, mara hii serikali imeamuwa kuwaongezea fedha nyingi sana Wizara ya Afya kwa ajili ya upatikanaji wa dawa na huduma mbali mbali ambazo zinatakiwa zipatikane.

Mhe. Naibu Spika, nilizungumzia suala la uwajibikaji jana tu nilipigiwa simu na jamaa mmoja kwenye Hospitali ya *cottage* Makunduchi kulikuwa na mama mmoja anataka kujifungua lakini hali ikawa ngumu sana gari zipo lakini mafuta hakuna, ikabidi walioko pale watafute namna ya kwenda kukopa mafuta lita ishirini lakini wanasema bado mgao wa mafuta ndani ya Hospitali ile upo. Sasa suala la uwajibikaji naomba viongozi wakuu tuweze kusimamia, serikali inajitahidi kuhakikisha haya matatizo hasa ya Wizara ya Afya yanapungua, lakini yanalazimishwa na baadhi ya watu yaendelee kujirudia.

Juzi tulikuwa na kesi hapa na Mhe. Waziri wa Afya alikuja baada ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub kusema dawa hakuna hospitali akazitaja. Lakini Mhe. Waziri alikuja na watendaji wake hapa akataja dawa fulani ipo, dawa fulani ipo,dawa fulani ipo. Lakini sisi tuliomo humu asilimia kubwa tulikuwa tunaamini ni kweli Mhe. Jaku Hashim Ayoub kaambiwa na wananchi wake zile dawa hakuna kwa sababu ukienda Hospitali unaambiwa hakuna. (*Makofi*)

Lakini Mhe. Waziri pengine watendaji walioko huku kwenye ghala la madawa kwa urasimu wao tu hawapeleki dawa kule hospitali. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hapa alijikakamua na kusema kuwa dawa ziko lakini sisi na mmoja mimi siamini kama dawa wale waliokuwa kule hospitali wanazipa kwa sababu ukienda dirishani *simple* tu unaambiwa dawa hiyo hakuna nenda kanunuwe.

Kwa hiyo, niiombe serikali hasa hao wasimamizi wamawaziri na Manaibu Waziri wawasimamie watendaji wetu ili tuhakikishe serikali imejibana kwenye bajeti mawizara mbali mbali, lakini kuhakikisha Wizara ya Afya ina bajeti kubwa ili kuwapunguzia mzigo wananchi wetu wanyonge wapate dawa wanapokwenda hospitali. Lakini bahati nzuri wenzetu hawa ambao hatujui nia yao nini wanaisababisha serikali kusemwa, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inazungumzwa vibaya kuhusu suala la madawa. Niombe serikali hasa Mhe. Waziri, Naibu Waziri waweze kuwajibika kuwasimamia hawa watendaji ili zinapotolewa dawa ziweze kuwafikia wananchi kama ilivyohitajika.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe. Rais pamoja na Mhe. Waziri wa Elimu , pamoja na sisi wenyewe kwa suala zima la kutoa elimu bure ya msingi pamoja na sekondari. Kwa kweli wananachi wengi tulikuwa tukibebeshwa mzigo mkubwa hasa Waheshimiwa Wabunge pamoja na Wawakilishi na Madiwani. Mwananchi yoyote akienda Skuli akiambiwa mwanangu anahitajika ada ya shilingi elfu ishirini au elfu kumi na tano unaanza kupigiwa simu. Lakini sasa hivi naamini serikali baada ya kuamua kwa makusudi kuweka elimu bure ya msingi na sekondari zile simu zitapungua na wananchi wetu wataweza kusoma au vijana wetu watapata kusoma vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea niipongeze serikali sasa hivi kwa suala zima la uajiri...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Masoud Abrahman Masoud naona Mhe. Mwenyekiti kakukaa na roho endelea tu. Sasa sijui yupi maana kuna wawili maana kuna wenyeviti wawili. (*Makofi*)

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Naibu Spika, kwa muda mrefu tulikuwa na kilio ndani ya Baraza la Wawakilishi kuna nafasi nyingi ambazo wazee wetu wanastaafu kwenye mawizara tofauti y serikali lakini lilikuwa suala la uajiri linakuwa zito sana. Lakini sasa hivi kila siku ukifungua redio, TV unasikia matangazo mbali mbali kwenye Tume ya Utumishi wanatangazwa watu wenye sifa za kwenda kuomba ajira na bahati nzuri wanaajiriwa.

Kwa hiyo, tuipongeze serikali kwa kufanya kazi hiyo nzuri Mwenyezi Mungu ajaalie wale vijana wetu wote waliokuwa wana elimu ya juu wapate ajira ili wapate kuisaidia nchi yao.

Mwisho Mhe. Naibu Spika, niseme tu suala la udhalilishaji. Suala la udhalilishaji kwa kweli sasa hivi limekuwa sugu. Niombe serikali baada ya bajeti hii kamati itakayokuwa inashughulikia suala la Wanawake na Watoto wapewe nafasi wapite jimbo kwa jimbo wende na wao wakatoe maoni yao au wakatoe semina kwa wananchi wetu ili wapate kujua kama suala hili la udhalilishaji si zuri katika jamii pamoja na kuwa kila siku Vyombo vya Habari, vipeperushi lakini viongozi wetu wakuu na viongozi wa majimbo tunalizungumza kwenye maeneo tofauti. Lakini bado suala hili linaendelea hapa Zanzibar.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, niendelee kumpongeza Mhe. Rais kwa kusimamia vizuri serikali, lakini niendelee kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha kwa kazi

nzuri ambayo anaifanya nimuombe tu aendelee kufanya juhudi zaidi lakini kubwa asimamie wafanyabiashara wanaokwepa kodi, lakini pia asimamie wafanyabiashara wanaoleta bidhaa mbovu Zanzibar wasiweze kuingiza ili kuwaponesha wananchi wetu na maradhi ambayo yanaweza kusababisha matatizo kwa afya zetu.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, niunge mkono hotuba hii ya Waziri wa Fedha ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na niseme naipongeza kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Masoud Abrahman Masoud ahsante sana kwa mchango wako umekuwa ukirudia Mhe. Mwenyekiti. Sasa sijui mimi na Mhe. Mwenyekiti, tumefanana na nafikiri ni mazoea tu basi.

Sasa tumpishe Mhe. Mwanaasha Khamis Juma atoe na yeye mchango wake baada ya hapo atafuata Mhe. Dokta Makame Ali Ussi na mchangiaji wetu wa mwisho kabisa atakuwa Mhe. Said Soud Said Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi. Karibu Mhe. Mwanaasha Khamis Juma.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia Hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed lakini pia ni Mwakilishi wa Jimbo la Donge kuhusu Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2018/19.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa na mimi nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia siku hii ya leo niweze na mimi kuchangia machache katika Hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Naibu Spika, pia nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na watendaji wake wote ambao wanafanyakazi kwa pamoja. Lakini pia niishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzabar ikiongozwa na Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt Ali Mohamed Shein kwa kusimamia Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kutuletea hotuba hii pamoja na mipango waliyoipanga katika serikali ili kuona wananchi wetu wanapata zile huduma kwa uhakika.

Mhe. Naibu Spika, mimi nije moja kwa moja wenzangu wamechangia mengi ila mimi sitakuwa na michango mikubwa sana lakini nataka niongezee tu katika ukurasa za 12 kuhusu utekelezaji wa hatua za kuimarisha mapato 2017/18. Mhe. Waziri ametaja marekebisho ya Sheria ya Ajira namba 11 ya mwaka 2005 katika kifungu cha 100(ii) kwa kuelekeza malipo yote ya mishahara ya waajiriwa kulipwa benki.

Mhe. Naibu Spika, huu mpango ni mzuri sana na ni hatua nzuri ambayo ameifikia, mimi naomba niwapongeze sana. Lakini nilikuwa na ushauri tu kidogo kuhusiana na yale ambayo tunayaona katika huduma hizi.

Mhe. Naibu Spika, katika huduma hii nilikuwa namshauri Mhe. Waziri au naishauri serikali kwa jumla kupunguza kwa vikwazo vya huduma za kibenki kwa wananchi. Hivi sasa tumeshuhudia Mhe. Naibu Spika, mwisho ya mwezi ukifika kunakuwa na misururu mikubwa kwenye *ATM* na huduma hizi huwa zinazorota.

Mhe. Naibu Spika, mie nilikuwa nashauri katika kutumia huduma hii basi Mhe. Waziri tuandae mpango wa kuweka hizi huduma za kibenki kupitia simu yaani *Mobile Bank*. Miamala ya Benki iunganishwe na simu za wateja mtu akitaka kutoa pesa yake aende moja moja kwa wakala na atatoa hii itapunguza usumbufu kwa watu wetu kwa hivyo naomba sana nishauri hilo Mhe. Naibu Spika kwa Mhe. Waziri. Lakini la pili tuje katika uk. 14 *paragraph* 34 kuhusu usajili wa namba binafsi za magari yaa *private number registration.* Mhe. Waziri ameleza kuwa utekelezaji wake umeanza tokea mwezi Disemba 2017 baada ya kusainiwa kanuni sasa sijafahamu Mhe. Waziri akija anieleze tu kwa nini alisema lengo linaelekea kufikiwa wakati hakuna mwananchi aliyesajili maana serikali haijapata mapato yoyote.

Mhe. Naibu Spika nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri aje anifafanulie ni malengo yepi yamefikiwa wakati hakuna fedha iliyoingia.Lakini pia nilikua natoa ushauri kwa serikali kupitia Wizara ya Fedha nilikua naomba sana kwenye eneo hili lifanyiwe kazi kwa sababu inaonekana ni eneo lenye kupata mapato lakini pia waweze kujitangaza ili kuwavutia watu kuja kusajili vyombo vyao binafsi.

Mhe.Naibu Spika, nije katika uk.31 kuhusu mapendekezo ya hatua za kuimarisha mapato katika *paragraph* ya 76 amesema katika eneo hili kufanya mapitio ya mfumo wa misamaha ya ushuru wa stempu kuhaulisha mali katika mali za urithi na hasa hiba au zawadi, hatua ni nzuri ni ya kupongezwa lakini kwa hivi sasa Mhe. Naibu Spika kunaonekana utaratibu ule wa kutoa ushuru wa tempu kwenye mali za urithi na hiba lakini pia unanyima fursa wananchi kusajili mali zao na kupata haki za umiliki na katika hili.

Mhe. Naibu Spika wanaoathirika sana ni wanawake na watoto ambao wengine hawajui taratibu hizi na kupelekea kudhulimiwa mali zao za urithi au hiba za kukosa hati za umiliki. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri naomba sana mapitio haya ya mfumo wa ushuru wa stempu yafanyike ili pale mwenza wake mtu anapompatia zawadi kwa mfano nyumba kiwanja gari na kadhalika iweze kuhaulishwa bila ya vikwanzo na kuepusha usumbufu wa umiliki ule kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri katika eneo hili nalo waliangalie.

Mhe. Naibu Spika, katika uk 34 wa kitabu cha Mhe. Waziri kuhusu kodi ya majengo *paragraph* 81, waziri nimpongeze sana na alitueleza kodi hii itakusanywa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa majengo ya biashara. Alisema kwa jumla ya bilioni 5 zinatarajiwa kukusanywa na zinapelekwa serikali za mitaa. Mhe. Naibu Spika, nimpongeze sana na ni jambo zuri sana kufikia hilo lakini nilikuwa na ushauri sana kuwa waweke yaani *formula* ile nzuri ya kuhakikisha fedha hizi zinafikishwa kwa serikali za mitaa.

Kwa sababu Mhe. Naibu Spika imeonekana kuwa baada ya kipindi kifupi tu kuhusiana na suala zima la ugatuzi basi kupitia halmashauri wanafanyakazi vizuri sana na mpaka sasa inaonekana kuwa kazi zao zinaenda vizuri. Mhe.Naibu Spika, kwa ushahidi nipo katika Kamati ya Ustawi wa Jamii kabla ya ugatuzi basi ilikuwa kuna tabu kidogo katika vile vituo vya afya kuna vitu vyengine ni kidogo tu yaani vya idadi ndogo ya fedha basi inakuwa hakuna au mfano masuala ya umeme pamoja na maji.

Lakini baada ya kugatuliwa tumeona kuwa zile huduma kwa kipindi kile cha ugatuzi basi huduma zile katika vituo vya afya na hasa katika skuli hizi za msingi zinapatikana kwa ufasaha. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri wawe na *formula* nzuri kwa vile katika kitabu chake kimeonesha kuwa wanataka kuzipelekea fedha ili izifikishe serikali za mitaa basi wawe na *formula* maalum ili zile fedha ziwafikie walengwa na waweze kufanya kazi zao kwa umakini na na kwa ufasaha kuwaletea wananchi wetu matokeo mazuri kwa vile hii ni bajeti inayozingatia matokeo na nina imani kuwa waziri ni msikivu na anaweza kufatilia hilo na kufanya hivyo alivyokusudia lakini kwa *formula* maalum ili serikali za mitaa zipatiwe zile fedha ziweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, kama nilikvyosema mimi nilikuwa sina mengi ya kuchangia kwa sababu mambo mengi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamechangia vizuri sana lakini na mimi nimepitia hichi kitabu nikaona katika maeneo hayo niweze kutoa ushauri wangu kwa serikali yetu ili iweze kufanya kazi vizuri na wananchi wetu wawe na imani kwa Chama cha Mapinduzi lakini pia wawe na imani na serikali yao waliyoiweka madaradakani.

Mhe. Naibu Spika kwa hayo machache nichukue nafasi hii tena kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa hutuba yake hii nzuri na niseme katika baraza lako hili tukufu naiunga mkono hutuba hii kwa asilimia mia na nadhani mapendekezo haya ambayo nimeyatoa Mhe. Waziri atayachukua na kuyafanyia kazi kwa umakini zaidi nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti Mwanaasha Khamis, sasa nimpe nafasi Mhe. Waziri wa Kilimo Mifugo na Uvuvi Dkt. Makame Ali Ussi anafuata mchaniaji wetu wa mwisho kama nilivyosema mwanzo Mhe. Waziri asiye na wizara maalum Mhe. Said Soud.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nikifuatilia sana jinsi unavyoliongoza Baraza unavyoliendesha ni vizuri sana na mimi naogapa sasa hivi nisije nikakosea ukaja ukaja ukanikosoa maan yake unaweza sana kukosoa papo kwa papo. Sasa Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwanza naomba kumpongeza sana Mhe.Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake bora kuiwezesha kupatikana kwa bajeti hii ambayo kwa kweli ni bajeti ya mfano. Bajeti nyingi sana duniani hazipiti bila ya kukosolewa sana wakati mwengine kurudishwa lakini hii inaweza kupita bila ya matatizo na kwa sababu iko safi sana na imeeleza mambo mengi kwa uwazi. Kwa hivyo nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi pamoja na watendaji wake wote kwa bidiii wanaoichukua kuendeleza wizara hii.

Pili nizipongeze sana hizi kamati Kamati ya Bajeti pamoja na Kamati ya Fedha, Biashara, Kilimo, Kamati ya *PAC* pamoja na kamati zote ambazo kwa kweli zilikuwa zikufuatilia kwa karibu sana shughuli hizi za bajeti. Aidha nazipongeza sana wizara zimefanya kazi kubwa kuwasilisha bajeti ambazo zinaeleweka na zikaiwezesha Wizara ya Fedha kuleta bajeti pia inayoeleweka.

Sasa Mhe. Naibu Spika, baada ya kueleza hayo sasa niinginge katika mchango wangu. Kwanza nitaanza na mapato na matumizi nitaeleza kwa ufupi tu kwa sababu mambo mengi yamelezwa na haya nitakayoeleza sio kwamba nayaeleza hayamo, yamo lakini nataka kuweza mkazo tu kabisa katika utekelezaji wa haya. Kwanza mapato na matumizi uwiano wa mapato na matumizi ulioainshwa uko *balance* yaani uko sawa kwa sawa 1.3 trilion mapato 1.3 trilion ni matumizi ni vizuri tutatumia tulichokipata. Lakini sasa nashauri tu wenzangu tutekeleze hii bajeti kama inavyosema ili tuweze kupita matumizi tuweze kukusanya kupita yale matumizi ili tuweze kupata akiba ya kuweza kuweka katika mfuko wetu mkuu. Hayo tu ndio niliyotaka kusema kuhusu mapato.

Sasa nikenda kwenye muelekeo wa uchumi Wizara imeeleza vizuri sana kwenye uchumi na umelenga kwenye kuimarisha biashara ya ndani na nje ya nchi kuimarisha vitega uchumi vya utalii vya kilimo, mifugo, maliasili, uvuvi na sehemu nyengine za kutoza kodi. Nasema kwa kweli tushirikiane sana katika kuimarisha kwani bila ya haya mambo ambayo ameyataja Wizara ya Fedha kusimamiwa vizuri basi kutakuwa muelekeo wetu wa uchumi unaweza ukenda kombo. Kwa hivyo nawashauri wenzangu wote tushirikane katika kukifata kitabu hichi juu ya maelezo yaliyotolewa kwenye muelekeo wa uchumi.

Pili tuende kwenye mfumko wa bei, mfumko wa bei uliotajwa hapa kwa kweli sio mkubwa sana ukilinganisha na nchi nyengine lakini naomba tu kusema kwamba tujitahihidi sana mfumko huu wa bei usiende mbali sana ukaja ukatuathiri. Tunafarijika sana tukiona kwamba wale wenye mahusiano mazuri na sisi kama vile China, India, *UAE* na kwengineko mfumko wa bei hautarajiwi kwenda mbali sana na sisi hapa Zanzibar tutagemea kwamba hakutakuwa na athari kubwa kwenye mfumko wa bei kwa hivyo tujitahidi ili huu mfumko wa bei usije ukatuathiri.

Jengine ambalo tutalielezea kwenye kitabu hichi ni kuhusu matarajio ya uchumi tu nategemea kuongezeka kwa pato kwa kasi ya asilimia 7.7% sasa na hii nayo ni nzuri sana kwa sababu hata hizo nchi zinazoendelea pamoja na kwamba uchumi wao ni imara wana mali nyingi sana lakini hawafikii wao wako kwenye 3, 3.2 zaidi ya hapo sisi tuko 7 na kuendelea lakini kwa sababu uchumi wetu mdogo tunapaswa twende hivyo. Lakini sasa nina matumaini makubwa kama tunaenda kwa kasi hii mara mbili zaidi ya wanavyokuwa wao basi tuko mbioni kuwafukuza kuna wakati hwenda tukawakuta tukawa tuko sawa kimaendeleo. Kwa hivyo tusimamie sana bajeti yetu hii ili tuweze kwenda mbele.

Sasa kwenye kilimo sasa nakwenda kwenye Wizara ya Kilimo sasa ndio tunayoisimamia ni kwamba Waheshimiwa Wawakilishi wamezungumza mambo mengi sana wametushauri, wametukosowa wamependeleza mambo mengi sana nawapongeza sana na sisi tunawaahidi tutafanya vile walivyotelekeleza lakini pia kubwa nawaomba

tushirikianae kwa maana utekelezaji wa bajeti zote hizi unategemea ushirikiano baina ya yetu sote sisi wawakilishi na hata wananchi kwa ujumla.

Kwa hivyo, naawahidi kwamba suala walilolitaja la umwagiliaji ni kweli ni suala ambalo kweli linahitaji kutiliwa mkazo tutafanya hivyo, suala la kuimarisha mifugo nalo tutafanya kuimarisha mifugo na ndio maana imeundwa taasisi maalum inaitwa *ZALIRI* (*Zanzibar Life Stock Recite Institution*) hii itasaidia sana kufanya utafiti juu ya mifugo na uzalishaji wake ulio bora ili kuongeza mapato na kuleta tija kwa wananchi.

Kuna suala pia la Makurunge wametaja tumeshaliwekea kwa kweli tutakwenda Makurunge kama tulivyoagizwa na Baraza letu tukufu la Mapinduzi tutakwenda kushughulikia suala la Makurunge ili kuona mambo ambayo tunaweza tukayafanya kule Makurunge kwa ufanisi zaidi kwa maana lengo la kule Makurunge ni kuongeza mapato hapa petu Zanzibar kwa hivyo kuchukua lengo lile la kupewa eneo lile ili tuweze kuongeza mapato.

Kuna suala jengine ambalo wametutaka waheshimiwa tulifate hili suala la ugani wanasema wanaohitimu masomo pale Kizimbani wapelekwe kwa wananachi hilo ndio lengo. Tutunategemea kila tawi au kila eneo lililokusudiwa basi lipate bwana au bibi shamba mmoja atakae kuwa pamoja na wakulima ili kutatua matatizo yao kama inavyoelekea.

Halafu la mwisho lakini sio hilo peke yake yako mengine ni kwamba wamesema tuwasaidie wale wakulima ambao wamepata athari kwenye mazao hilo ni lengo la serikali kumsadia mwananchi yoyote anayepata maafa au athari kwenye uchumi wake. Kwa hivyo naahidi wahehsimiwa wajumbe tutafuta njia za kuwasaidia wakulima wetu. Baada ya kusema hayo sasa nitasema tu kwamba tunakusudia kufanya mambo yafuatayo katika bajeti yetu hii.

Kwanza kabisa tukubaliane kwamba bajeti imeshakamilika kwa ufanisi mkubwa sana kilichobaki sasa ni utekelezaji katika wizara yetu ya kilimo tumejiandaa kwenda sambamba na utekelezaji wa bajeti hii huku tukizingatia kwamba tunayo bajeti iliyopangwa kwa utaratibu na mikakati maalum ambayo inalenga kwenye maendeleo husika. Kwa hivyo kwanza kabisa tutasimamia sana bajeti hii tutaisimamia kwa karibu zaidi bajeti hii kwa uwazi kwa umakini na umahiri mkubwa na kufuata taratibu za kifedha hili tutaoanisha utekelezaji katika vipindi mbali mbali vya muda mfupi, muda wakati na mrefu kwa kuzingatia vipa umbele vya serikali.

Tutaendelea utaratibu mzuri wa ukusanyiji wa mapato na matumizi kama ilivyoainsha katika mipango ya maendeleo ya serikali tutahakiikisha kwamba mambo yanahusu bajeti pamoja na takwimu zake yanainishwa kwa uwazi na yapatikana wakati wowote yanapohitajika, pia tutakuwa tayari katika kuitetea na kuelezea upembuzi yakinifu wa bajeti inayotekezwa. Pia tutakuwa tayari kuwasilisha inapohitajika mahesabu sahihi ya bajeti husika. Aidha tutapanga, tutadhibiti na kusimiamia utekelezaji wa bajeti kwa ukaribu zaidi kuhakikisha kwamba ufanisi yaani *performance* kutathimini kwa maana *evaluation* nimeyatia hayo kwa sababu inaweza kuwa Kiswahili kimekwenda kombo

kwa hivyo watu watafsiri kwa hivyo ninavyosema *evaluation* na *value for money* yanaendana na mapendekezo ya bajeti yaani yatakuwa *integral to the budget process.*

Pia tutafanya kubaini yaani *identification,* kutathmini yaani *to asses* na kusimmaia kwa karibu zaidi matarajio ya muda mrefu ya maendeleo na matatizo ya kifedha yaani *financial risk* zinazoweza kutokea. Tutaboresha yaani ku-*promote* tunaboresha hadhi yaani *integrity* na kiwango cha makisio ya bajeti kwa mpangilio wa kifedha na utekelezaji wake kibajeti kwa kufanya uhakiki wa mara kwa mara.

Tutahakikisha kwamba uwepo wa *asset register* mahsus pamoja na mambo yake yanayohitajiwa yaani *depreciation* na mambo mengine *evaluation* na kadhalika yanakwenda sambamba na na mali ziliopo. Tunasama tutakuwa *flexible* na mahitaji ya serikali pamoja na mabadiliko ya teknologia ikiwemo pia na mabadiliko ya tabia nchi yaani *climate change* tutaongeza eneo la umwagiliaji maji kama tulivyosema tufanikisha uvuvi wa bahari kuu yaani *blue economic*, tutashiriki kikamilifu katika kutekeleza kwa vitendo ilani ya Chama cha Mapinduzi maelekezo ya Mkuza III na kadhalika, pamoja na kudumisha ushirikiano, mshikamano, umoja, undugu, ujirani mwema, urafiki na upendo kwani haya ndio mambo ambayo yatatuletea salama, amani pamoja na utulivu mambazo ndizo nguzo kubwa za maendeleo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nasema mimi nisiendelee sana kwa sababu hii bajeti iko vizuri tusije tukazungumza mambo mengi tena, ikaja ikawa tunatia maji tembo yetu. Kwa hivyo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia. Twendeni tukaitekeleze bajeti hii kwa ufanisi ili tuweze kuleta maendeleo yanayotakiwa. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, sasa hivi nimpe nafasi Mhe. Said Soud tumempata mchangiaji mwengine Waziri wa Afya Mhe. Hamad Rashid Mohammed. Mhe. Said Soud karibu.

Mhe. Said Soud Said: (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti yetu hii ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambayo tunategemea kwamba ndio pekee itakayotuongoza katika kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Kwa hivyo, kwanza napenda kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, pamoja na Makamu wa Pili wa Rais kwa kuyaelekeza yale yote ambayo yanahitaji kufanywa katika kipindi hiki tunachoelekea.

Vile vile nachukua nafasi hii kuwataka Wazanzibari wote tushirikiane kwa pamoja katika kutekeleza yale yote yatakayoelekezwa na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa hakika kitabu hiki ambacho kinaelekeza au vitabu vyote vilivyoelekeza bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ni vitabu ambavyo vimeidhinishwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa maana hiyo mimi nikiwa ni

mmoja wa serikali napaswa kusema kwamba bajeti hii imekamilika na ni bajeti pekee itakayowaelekeza Wazanzibari kufanikiwa mambo yao.

Mhe. Mwenyekiti, bajeti hii pia imeweza kwenda mpaka kwenye ilani ya Chama cha Mapinduzi. Katika ukurasa wa 124 kifungu namba 69, ilani imesema kwamba imeidhinisha miradi 35 yenye thamani ya dola bilioni 1.6, ilani hiyo hiyo pia imesema kwamba itaweza kuleta ajira karibu 1,365 ili zitakazoweza kuwafanya Wazanzibari kujikwamua.

Sasa sisi kama serikali tuna wajibu wa kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi na kuhakikisha kwamba Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi yale yote aliyoyaagiza yanafanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar Mhe. Ali Mohammed Shein, ameweza kuyakwamua mambo mengi sana ambayo yalikwishakwama kutokana na kwamba uchumi ulikuwa umedororo. Lakini hali ya uchumi ya Zanzibar imekuwa na kila mtu anashuhudia maendeleo yaliopo. Haya yote yameweza kufanikiwa chini ya uongozi wa Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na watendaji wake, kuwa makini katika kusimamia upatikanaji wa fedha na ndio yaliyoweza kumpa nguvu Mhe. Rais kuyakwamua yale yaliyokwama katika nchi yetu hii ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, tulikuwa tumeshuhudia uwanja wa Mao Tsetung kwamba ulikuwa sasa ni uwanja wa kulaza ng'ombe tu, hakuna lolote linaloendelea. Lakini leo uwanja wa Mao Tsetung sio muda mrefu utaanza kufanyakazi na Wazanzibari wataweza kufurahia matunda ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ilikuwa haina uwezo wa kuwapeleka watu kutoka Unguja na Pemba vile inavyotakiwa, na tukashuhudia meli za watu binafsi zikiuwa watu walio wengi katika visiwa hivi. Lakini kwa uwezo wake na busara zake tumeweza kupata meli ya kisasa ambayo inaweza kufanyakazi hizo, pamoja na changamoto lakini kesho kutwa meli hii itaanza kazi na Wazanzibari wataweza kutumia usafiri huu wa mara kwa mara.

Mhe. Naibu Spika, tulikuwa tunashuhudia ongezeko la bei la *TANESCO* kwa *ZECO* ya Zanzibar, lakini chini ya busara zake leo deni hilo limebakia chache sana na tunajivunia Wazanzibari kwamba tunaliondoa deni hili kwa utaratibu uliokubalika chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, uchumi wetu umekuwa na umekua katika mazingira makubwa sana kiasi cha kwamba hata Rais ameweza kuwafikiria wazee wa nchi hii kwa kuwapatia fedha shilingi 20,000, ili na wao waweze kuona kwamba wako katika taifa lao na wanaongozwa kwa uadilifu mkubwa chini ya kiongozi wao.

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi nataka niseme kwamba iko haja kwa wawakilishi wote kuhakikisha kwamba tunapitisha bajeti yetu hii na tunahakikisha kwamba tunatoa nguvu kwa mawaziri walio na wizara, tunatoa mashirikiano kwa njia zote majimboni ili kuona

miradi ya maendeleo iliyokusudiwa inafanywa. Sisi kama viongozi, sisi kama serikali tunaahidi kusimamia hoja hizo ambazo zimetolewa kama changamoto ili kuhakikisha kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanikiwa kuleta maendeleo kwa Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, nawaomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kuhakikisha kwamba tunasimama katika majimbo yetu kutetea ilani ya Chama cha Mapinduzi, kutetea Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kutetea Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar, ili kuhakikisha kwamba tunaishi kwa amani na utulivu.

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wawakilishi na waheshimiwa wananchi wanaonisikiliza, bila ya kuwepo kwa amani basi hakuna maendeleo. Kwa hivyo ni wajibu wetu sasa kushikamana katika kulinda amani hii, ni wajibu wetu sisi sasa kuona kwamba tunapiga hatua moja baada ya nyengine kusogeza maendeleo. Licha ya kwamba kuna watu hawajui maendeleo yanapatikana wapi na yanakuja vipi, lakini ninachotaka kusema tuhakikishe kwa pamoja chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwamba tunajenga nyumba moja, na tunapojenga nyumba moja tunakubaliana tushikamane.

Mhe. Naibu Spika, mimi leo sitaki kusema mengi nitasubiri kwenye *briefing*, ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Said Soud Said Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum. Sasa tumpishe Mhe. Waziri, atakuwa ndiye mchangiaji wa mwisho na baadae Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango atakuja jioni kwa ajili ya kufanya majumuisho. Mhe. Waziri wa Afya karibu.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Awali ya yote naomba kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma na Utukufu kwa kutujaalia kuendelea na shughuli zetu za Baraza kwa salama na amani, na tumemaliza kufunga mfungo wa mwezi wa Ramadhani mtukufu kwa salama na amani *Alhamdulillah Rabil Allamin.*

Pili Mhe. Naibu Spika, naomba kumshukuru sana Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein ambaye ameweza kuisimamia nchi yetu kwa amani na utulivu, lakini ametuletea bajeti hapa ambayo kwa kweli kama tutaisimamia vizuri basi nchi yetu inaweza kupiga hatua nzuri sana ya kimaendeleo.

Vile vile naomba nimshukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kuweza kusimamia shughuli za utendaji wa kiserikali, na shughuli za Baraza hapa ndani kwa uadilifu mkubwa. *(Makofi)*

Tatu, naomba nimshukuru sana kipekee Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na timu yake kwa kuwa makini sana katika kusimamia uchumi wetu na maendeleo ya nchi yetu. Kazi wanayoifanya ni kubwa, nzito na ngumu sana. Lakini yeye na timu yake wameweza nchi yetu leo kubaki katika mfumo wa kiuchumi ambao duniani unatambulika. Kwanza wameweza kudhibiti sana mfumko wa bei si jambo rahisi hata kidogo. *(Makofi)*

Vile vile tumejitahidi kuweza kukuza ajira ndani ya nchi yetu na tatu, tumeonekana kabisa kwamba ukuaji wa uchumi wetu umebaki kwa asilimia 7 na kuendelea kwa kipindi kirefu sana. Nasema haya mambo matatu ni mambo makubwa sana katika kusimamia uchumi sio kazi ndogo na sio kazi rahisi hata kidogo.

Mhe. Naibu Spika, lakini nataka nimshukuru kipekee Mhe. Rais kwa kuweza kusimamia huduma za jamii afya na elimu ikiwa bado wananchi kwa kiwango kikubwa sana serikali inachangia badala ya wananchi kuchangia. Nasema nalo ni jambo ambalo sio rahisi hata kidogo, sio nchi nyingi sana zinaweza kufanya hivyo. Kwa hivyo, naomba sana tulisimamie hili na tumpongeze Rais wetu, tusimamie uchumi wetu ili uendelee kuhimili hizi huduma za jamii ziweze kulipiwa na serikali.

Mhe. Naibu Spika, katika kuchangia kwangu kulikuwa na mambo kama mawili au matatu yalijitokeza ndani ya Baraza lako, naomba nichukuwe nafasi hii kutoa maelezo kidogo. Jambo la kwanza tunalo suala zima la madaktari wa Cuba mwaka 2013 kwamba madaktari walikuwa wanalipwa fedha nje ya utaratibu. Kwanza nikubali nakiri kweli lilitokea hilo tatizo na serikali ikachukua hatua. Hatua ya kwanza ni kuwafukuza kazi wale ambao walihusika wakati huo na pili kuangalia utaratibu mzima kama ulikosewa ukarekebishwa na sasa hivi hakuna tena tatizo hilo ambalo lilikuwepo hapo nyuma.

Kwa hivyo, nasema ni kweli lilitokea na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu akahoji na hatimaye serikali ikachukua hatua kama vile ambavyo limependekezwa. Kwa hivyo, sio jambo ambalo ni endelevu, limemalizika na haliendelei hivi sasa. Kama kuna ushahidi mpya wa jambo hili linaendelea, naomba tuupokee tutaufanyia kazi, lakini katika *record* zetu kwa sasa hivi hakuna daktari yeyote wa Cuba anayelipwa nje ya utaratibu ule ambao umekubalika kiserikali. Hili lilikuwa jambo la kwanza.

Jambo la pili suala la madeni. Ni kweli serikali yetu inadaiwa na hata katika bajeti yetu tuliyopitisha hapa inaonekana kabisa bado serikali inaendelea kukopa. Kwa hivyo, tulikuwa tuna madeni tunayalipa na mengine hayamaliziki tunaya- *carry forward*. Huu ni utaratibu wa kawaida wa kuendesha serikali wala sio jambo kubwa.

Mhe. Naibu Spika, tukumbuke tu katika *supply* ya madawa imefikia asilimia 82 ya mahitaji na asilimia 82 tuliyofikia ndani yake tulikuwa na madawa tunakopa. Kwa hivyo, ni kweli kabisa yako madawa tunakopa na serikali inaelewa na tumepanga katika utaratibu wa bajeti tunaoendelea nao sasa hivi kuanza kuondosha hayo madeni kidogo kidogo. Kwa hivyo, sio kosa kudaiwa, kosa ni kwamba je tunalipa au hatulipi, tunalipa na ndio maana tumeendelea kupata *supply* ya madawa kama kawaida. Mimi sioni kama ni jambo la kupiga kelele sana *MSD* kweli wanatudai, kuna wengine juzi tu.

Moja ambalo tumelikuta hivi karibuni waligoma hawa ku-*supply* madawa kwa sababu wanadai. Jambo ambalo tumewaahidi ni kwamba tuleteeni madawa tutawalipa, hii ni serikali na wakaheshimu na waka-*supply* madawa. Kwa hivyo, ni kweli kabisa yapo madai kidogo ya kama 3.9 bilioni serikali inajua na hata jana wakati wa bango kitita Mhe. Rais aliahidi kabisa tutakaa kitako tuone *how best we can do* kumaliza haya

matatizo ya madeni yaliopo. Hili ni jambo la kawaida katika serikali wala sio jambo la kushtua sana hata kidogo, ilimradi tunalijua deni letu halali, tunalijua ni deni ambalo linaweza kulipika na serikali yetu ina uwezo wa kulipa kabisa italipa bila ya wasiwasi wowote.

Kwa hivyo, tunawaambia Waheshimiwa Wajumbe, hatukukopa kwa maana ya kukopa, tulikopa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi wetu, ni sisi sisi tunapiga kelele kama watu wakienda hospitali dawa hakuna, serikali lazima itafute utaratibu wa kuhakikisha dawa zinapatikana. Tumetafuta utaratibu dawa zimepatikana na *Alhamdulillah* watu wanapata huduma kama inavyostahiki. Kwa hivyo, nasema hili ni jambo ambalo nataka niliseme ni jambo ambalo tunalifanyia kazi vizuri na hatuna wasiwasi nalo.

Jambo la tatu Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba kutoa huduma hizi bure sio jambo rahisi hata kidogo. MRI pale kupima ni bure, ukienda kwenye hospitali ya *private* ni shilingi 700,000/- wakati mwengine mpaka shilingi 1,500,000/-, zile *reagent* zake tu kuzihudumia pale si chini ya shilingi 300,000/- au 400,000/-.

Kwa hivyo, lazima tukubali kwamba serikali chini ya Chama cha Mapinduzi imebeba mzigo mzito. Tunahitaji kuipongeza sio jambo rahisi hata kidogo. Nasema si serikali nyingi ambazo zimethubutu kufanya, nyingi zimeshindwa katikati, sisi tunaendelea kufanya kazi hiyo na tuandelea kufanya kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, hivi asubuhi nilikuwa Mnazi Mmoja Hospital, kuna madaktari bingwa kutokwa Marekani wamekuja, kutoka Abudhabi na kutoka Spain wameshangaa kituo chetu kile cha *Neuro* kazi ambayo imefanyika pale ni kubwa sana, nzuri sana. Wakasema kwa kweli wataendelea kuleta madaktari bingwa kuwasaidia wananchi wetu, kama serikali haikufanya *investment* ile pale wasingekuja madaktari bingwa hawa kuja kuweza kuwahudumia watu wetu.

Mhe. Naibu Spika, nasema hizi ni juhudi za serikali lazima tuzipongeze tuzisimamie pamoja na sisi hatusemi kwamba wawakilishi wakiona tatizo wasiseme, waliseme tu, waje watuone maofisini watwambie tutasaidiana katika kutatua matatizo haya. Haya ni mambo ya kutumia kila siku, ni kama vile unakunywa chai, leo sukari ipo nyumbani kesho haipo, ni utaratibu wa kawaida katika serikali.

Mhe. Naibu Spika, nilitaka niseme hili kwamba kwa kweli tunashukuru sana huduma zinazopatikana zinaendelea kuboreshwa siku hadi siku. Mimi nataka nishukuru sana, mara hii Mhe. Rais, tumetoka kwenye bajeti ya 72 billion, na kufika 93 billion, hilo sio jambo rahisi hata kidogo. Tumetoka kwenye madawa kutoka 8 billion tumekwenda kwenye 20.9 billion nasema sio jambo rahisi hata kidogo. Kwa hivyo, nasema tupokee haya ambayo tumeyapitisha na mimi nataka niwashukuru sana waheshimiwa wajumbe kwa kupitisha bajeti yetu. Tumekwenda kwenye kamati ya bajeti, tumekwenda kwenye kamati ya huduma ya jamii, wamepitisha bajeti ya afya, tupewe muda tuifanyie kazi. Kazi kubwa sasa ni kusimamia *value for money* katika fedha tulizopata, kazi kubwa ni kusimamia vifaa tunavyovinunua vinawahudumia wananchi, kazi kubwa tunazofanya ni kwenda kwa wananchi kusikiliza matatizo yao na kutatua matatizo yao.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa wajumbe, kwa kuwa muda uliobakia utakuwa haumtoshi Mhe. Waziri kwa ajili kufanya majumuisho, na kwa kuwa hakuna mjumbe mwengine yoyote ambae ametaka kuchangia.

Kwa hivyo, mimi nichukue fursa hii Waheshimiwa Wajumbe kwanza kabisa kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Rais wetu mpendwa wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake uliotukuka. Wakati tukijadiliana hapa mengi ambayo tumeyazungumza tumeona kwamba Mhe. Rais wetu ana nia njema kabisa, pamoja na wasaidizi wake wote ambao wanamsaidia, akiwemo Makamu wa Pili wa Rais, kwa kutupangia mipango mizuri kabisa ambayo itatuelekeza kule ambako tunakutaka ambayo ni maendeleo ya nchi yetu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe, nichukue fursa hii vile vile kumpongeza na kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, pamoja na watendaji wake wote kwa kutuletea mipango mizuri na leo tumeweza kujadili. Waheshimiwa Wajumbe wameweza kuuliza maswali, lakini vile vile Waheshimiwa Wajumbe wameweza kuishauri serikali na hatimae tunaamini kwamba Mhe. Waziri akija hapa atatupa majibu yale ambayo tumeyauliza, lakini atapokea ushauri wetu ambao tumeutoa. Nakupongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Waheshimiwa Wajumbe, nikiwa namalizia hilo nimepata tangazo hapa ambalo linahusiana na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake Habari na Utalii, wakutane katika chumba cha Kamati No. 2 juu, mara tu baada ya kuakhirishwa kikao hicho.

Baada ya kusema hayo machache Waheshimiwa Wajumbe, sasa nisitishe kikao hichi hadi saa 11:00 jioni. Nakuombeni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa Mhe. Waziri saa 11:00 jioni anakuja kwa ajili ya majumuisho, nawaomba sana mfike mapema ili tuweze kufanya shughuli yetu mapema na kumaliza mapema. Baada ya kusema hayo, ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe.

(Saa 6:35 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)
(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, wachangiaji wote walikamilika wakati wa asubuhi. Sasa kwa heshima na taadhima naomba nimwite Mheshimiwa mtoa hoja, Waziri wa Fedha na Mipango ili aweze kujumuisha Bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia afya njema, lakini pia kutujaalia uzima na kutuwezesha kukutana tena leo hii alasiri hii kwa ajili ya kufanya

majumuisho ya Hotuba ya Bajeti ya Serikali, lakini vile vile Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2018/2019.

Mhe. Spika, nipokee pongezi zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe, wengi wametoa pongezi nyingi kwa hotuba nzuri, lakini vile vile wametoa pongezi kwa utekelezaji mzuri na hasa katika suala zima la ukusanyaji wa mapato. Lakini mafanikio hayo yana sababu zake, na miongoni mwa sababu hizo ni sera zetu nzuri tulizonazo, lakini na mipango yetu mizuri katika nchi hii, lakini yote hayo ni uongozi makini wa Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein. Naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais kwa mafanikio yake haya au mafanikio yetu tuliyopata katika nchi yetu, lakini kwa uongozi wake wa busara na hekma na uono wake katika masuala ya kuendeleza uchumi, lakini pia kuleta ustawi katika jamii. *(Makofi)*

Pia nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, nae amekuwa msaada mkubwa kwa Mhe. Rais, lakini vile vile amekuwa akituongoza vyema na kutuelekeza vyema katika utekelezaji wa shughuli zetu katika Wizara yetu ya Fedha na Mipango.

Nakupongeza wewe Mhe. Spika, lakini pia niwapongeze Naibu Spika, niwapongeze Wenyeviti wote wawili kwa kuliongoza Baraza letu kwa hekma lakini vile vile kusimamia mijadala iliyofanywa na Waheshimiwa Wajumbe tokea jana na hii leo. Nichukue fursa hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote waliopata fursa na ambao hawakupata fursa, waliochangia kwa kusema na hata wale waliochangia kwa maandishi. Kwa sababu michango yao, fikra zao zitatusaidia sana katika kuimarisha utekelezaji wa majukumu yetu kwa mwaka ujao wa fedha 2018/2019.

Mhe. Spika, niwapongeze sana Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri kwa mashirikiano makubwa. Bajeti ya Serikali haikamiliki bila ya mashirikiano ya Sekta zote za Serikali. Kwa hivyo, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Manaibu Mawaziri, lakini pia Mhe. Mwanasheria Mkuu nathamini sana mashirikiano ambayo mnatupatia.

Niwashukuru Makatibu Wakuu wakiongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi. Lakini vile vile niwashukuru sana watendaji wa Wizara yangu, tukianza na Katibu Mkuu Ndg. Khamis Mussa Omar, Naibu Katibu Mkuu, Katibu Mtendaji, Makamishna wote, Wakurugenzi, Afisa Mdhamini, lakini pia na Wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara zikiwemo *ZIPA, ZRB, ZSSF, TRA, BIMA* na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali pamoja na *PBZ* na wafanyakazi wote wa taasisi zote hizo nilizozitaja. Kwa kweli mimi binafsi nafarajika sana na mashirikiano na misaada mikubwa ninayoipata kutoka kwao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na Wajumbe wake wote, nimshukuru kwa mchango wao waliotoa kupitia hotuba yao iliyosomwa na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa, Mhe. Asha Abdalla Mussa. Lakini pia nimshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Baraza, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo na Wajumbe wake wote, tumefanyakazi vizuri sana kupitia Kamati hizi na Wizara yangu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hotuba zangu zote mbili zimepata bahati ya kuchangiwa na Waheshimiwa Wajumbe 28. Wajumbe 22 walichangia kwa kusema, lakini Wajumbe saba walileta michango yao kwa maandishi. Mhe. Spika, naomba niwatambue wote hao.

1. Mhe. Asha Abdalla Mussa
2. Mhe. Mohamed Said Mohamed
3. Mhe. Jaku hashim Ayoub
4. Mhe. Ali Suleiman Ali
5. Mhe. Simai Mohammed Said
6. Mhe. Hamza Hassan Juma
7. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil
8. Mhe. Suleiman Sarahan Said
9. Mhe. Omar Seif Abeid
10. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali
11. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
12. Mhe. Rashid Makame Shamsi
13. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini
14. Mhe. Miraji Khamis Mussa
15. Mhe. Bahati Khamis Kombo
16. Mhe. Shehe Hamad Mattar
17. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
18. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
19. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
20. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi
21. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
22. Mhe. Waziri wa Afya

Waliochangia kwa maandishi:

1. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ
2. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil
3. Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto
4. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
5. Mhe. Said Omar Said
6. Mhe. Mgeni Hassan Juma
7. Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji

Mhe. Spika, nianze kutoa ufafanuzi na maelezo kidogo kwa hoja zilizotolewa na Kamati ya Bajeti. Kabla ya kuanza kutoa ufafanuzi huo, lakini niseme tu kwamba maoni mengi ilikuwa ni ushauri ambao niseme tumeupokea ushauri huo. Lakini vile vile nieleze kwamba baadhi ya hoja zilizozungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe tayari zilikwishatolewa ufafanuzi na Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri wakati walipokuwa wakijumuisha hotuba za Wizara zao. Sitotoa ufafanuzi huo kwa sababu maelezo hayo naamini yanatosheleza sana.

Mhe. Spika, lakini pia Mhe. Waziri wa Afya ametoa ufafanuzi amenisaidia kujibu baadhi ya hoja. Lakini pia Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Dkt. Makame Ali Ussi nae ametoa ufafanuzi. Lakini vile vile Mhe. Said Soud Said nae alisaidia katika kutoa ufafanuzi. Kwa hiyo, hayo waliyoyaeleza wao sitayagusa katika maelezo yao.

Mhe. Spika, kuna hoja ya Mheshimiwa ya biashara ambayo hii ilizungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi, kwamba biashara baina ya Bara na Zanzibar inaonekana kuwa na matatizo na hasa kushuka kwa uhaulishaji wa bidhaaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara. Hili lilizungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi na walionesha *concern* hiyo.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba takwimu zetu zinaonesha kuwa biashara baina ya pande hizo mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimebadilika na kwamba kuna upungufu wa bidhaa zinazohaulishwa kwenda upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Zipo sababu za kutokea jambo hilo, moja ya sababu ni kwamba kama tulivyowahi kueleza hapo nyuma kidogo ni mabadiliko ya sheria ya *VAT* yaliyofanywa na wenzetu wa upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2016. Sasa yale yameweka masharti ya kuhaulisha biashara kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar, kwanza hilo. Kwa maana hiyo, kwa biashara zinazotoka, zimewekwa masharti ya kwamba biashara zinazohaulishwa kuja huku Zanzibar zimekuwa *zero rated* upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuondosha ule utaratibu wa zamani wa kurejesheana *VAT* kuwa kila upande ni wakala wa mwenzake. Utaratibu huo umeondoka na hii imeleta kidogo kutetereka kwa suala zima la biashara baina ya pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, vile vile kwa bidhaa zinazotoka hapa Zanzibar kwenda Tanzania Bara kumetokea mabadiliko ya kodi lakini pia usimamizi wa viwango, na hayo nayo kwa upande mwengine yameathiri. Lakini sisi ndani ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tunaona umuhimu wa kukuza biashara baina ya pande zetu mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nasema hivyo kwa sababu Muungano wa kisiasa wa nchi mbili ni lazima vile vile uwezeshe kuimarika kwa chumi za pande zote mbili za Jamhuri. Kwa hivyo, hilo ni suala muhimu, lakini vile vile sisi Muungano wetu ni wa kisiasa na tupo katika soko moja. Kwa hivyo, kwa kutambua hilo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaendelea na juhudi, kwa sababu tunaendelea na juhudi ya mazungumzo na wenzetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuona kwamba tunarudisha mfumo ambao utaimarisha biashara katika pande zetu mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo, mazungumzo hayo sisi hatutasita tutaendelea kuzungumza na wenzetu ili kuona umuhimu huo kwa ajili ya kuleta faida kwa wananchi wa pande zote mbili, lakini hasa kukuza chumi zetu kupitia biashara. *(Makofi)*

Lakini pia Kamati ilizungumzia umuhimu wa kuimarisha miundombinu ya kuingia nchini, na hapa tukizungumza miundombinu ya kuingia nchini tunazungumza Uwanja wa Ndege na naamini Waheshimiwa Wajumbe nyote mashahidi kwa jinsi serikali inavyochukua jitihada kubwa sana ya kuhakikisha tunakamilisha jengo letu la *Terminal III* na juhudi hizo zitaendelezwa. Lakini pia niseme tu kwamba jitihada kubwa zaidi

zitachukuliwa na tayari nimezungumza ndani ya Baraza hili kwamba mara baada ya kumalizika kwa kikao hichi cha bajeti, Wizara zetu nne zitakutana kwa ajili ya kuzungumza suala la ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri. Kwa hivyo, haya ni masuala ambayo sisi tunaendelea nayo na tutayafanyia kazi kwa sababu tunajua umuhimu wa kuwa na miundombinu imara katika maeneo ya uingiaji nchini.

Mhe. Spika, kuna suala la Kamati ilizungumzia kwamba vipaumbele hasa vya utafiti, lakini pia na kipaumbele cha kujenga uwezo wa watenda kazi havikufafanuliwa, Naomba hapa nitoe ufafanuzi kwamba utafiti ni jambo muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi wa nchi yoyote ile, bila ya utafiti hatua za kukuza uchumi zinaweza zikachelewa sana. Kwa kuelewa hilo serikali inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein imetoa umuhimu mkubwa sana katika suala zima la utafiti. Na ushahidi wa hayo ninayoyasema ni kwamba taasisi tatu za utafiti zimeanzishwa. Kuna Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ambayo ipo Kizimbani, kuna Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ipo pale Kizimbani, lakini vile vile Taasisi ya Afya nayo pia imeanzishwa na itatumia majengo yaliyojengwa na *African Muslim Agency* pale Tunguu. Kwa hivyo, hii ni ushahidi tosha kwamba serikali hii ina dhamira ya dhati ya kuhakikisha tafiti zinaendelezwa katika nchi hii.

Lakini jambo jengine ni kwamba kila wizara ina idara ambayo imepewa jukumu la kusimamia masuala ya utafiti, nayo ni Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, kwa masuala ya utafiti kisekta nayo yanaratibiwa kupitia idara hii. Lakini katika mwaka wa fedha wa 2018/2019 serikali imetenga fungu maalum la fedha chini ya Tume ya Mipango kwa ajili shughuli za utafiti, nalo hilo ni ishara nyengine inayoonesha wazi kabisa dhamira ya serikali katika kukuza masuala ya utafiti.

Mhe. Spika, ukitaka kujua uchambuzi wa hizi tafiti serikali ilishirikiana na *COSTECH* kuandaa *National Reserach Agenda* ambapo kuna kitabu kizima kinachoeleza *research* zote zilizopewa kipaumbele za kuendeleza uchumi na ustawi wa jamii katika nchi yetu. Wajumbe wa Kamati tukiipitia *National Research Agenda* hiyo tutaona jinsi gani zilivyochambuliwa.

Mhe. Spika, kuna masuala ya kujenga uwezo nayo yamepewa umuhimu unaostahiki, na hata wakati nasoma Muelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2018/2019 nilisema kwamba serikali imedhamiria kujenga uwezo wa wataalam na mabingwa katika fani mbali mbali. Hilo nililisema wazi na nikataja baadhi ya sekta, afya ikiwemo, kilimo, mafuta na gesi, hizo ni baadhi ya sekta ambazo zinapewa kipaumbele. Na serikali imeweka utaratibu maalum kwa vijana wanaochukua kozi hizo, basi kupata upendeleo katika ufadhili wa masomo na katika sekta ya afya. Kwa mfano sasa hivi tuna madaktari ambao wapo nchi mbali mbali wanasoma, lakini pia serikali ina mpango wa kupeleka madaktari na mabingwa katika masomo kwa ajili ya kuweza kujenga uwezo wa watendakazi katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kuna suala zima lilizungumzwa la fedha zinazopangwa kwa miradi na programu za maendeleo zitolewe kama zilivyopangwa. Hii ndio jukumu la serikali na ndio azma ya serikali ya kuhakikisha kwamba fedha zinazopangwa kwa shughuli za kazi za kawaida lakini kwa mipango ya maendeleo, miradi ya maendeleo, programu za

maendeleo, zinatolewa kama zilivyopangwa. Na tumepiga hatua kubwa katika eneo hili na takwimu zinaonesha, taarifa zetu zinaonesha kwamba tumetoa fedha nyingi zaidi kama serikali hata kuwashinda washirika wetu wa maendeleo. Kwa maana ya *percentage wis*e sisi tumetoa *percent* kubwa zaidi ya fedha tulizoahidi kuzitoa. Wakati mwengine tulichelewa si kwa sababu ya kwamba fedha hazikuwepo, lakini kwa sababu ya masuala mengine yakiwemo masuala ya mchakato wa manunuzi yenyewe ulikuwa unachukua muda na shughuli hizo zitaendelezwa katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Spika, walitaka kujua pia fedha zilizotengwa kwa ajili ya jengo la Mahkama Tunguu shilingi milioni 900 na wakasema kwamba zimetumika shilingi milioni 500. Shilingi milioni 500 hizo zimetumika kwa ajili ya kazi za awali zikiwemo kutafuta Mshauri Elekezi, lakini kufanya michoro ya jengo na nina furaha kusema kwamba michoro ya awali imeshaandaliwa na tayari fedha zimeshatengwa kwa ajili ya kuanza kwa ujenzi huo katika mwaka wa 2018/2019.

Mhe. Spika, kuna suala la Deni la Taifa lilizungumzwa na hili naomba niliseme kwa mara nyengine tena, na liko wazi katika ukurasa wa 18 wa kitabu chetu tumelieleza wazi kabisa kwamba hadi kufikia Machi, 2018 deni letu lilifikia shilingi bilioni 519.7 ikilinganishwa na mwezi wa Machi, 2017 deni letu lilikuwa ni shilingi bilioni 377.1. Sasa hii ni sawa na ukuaji wa asilimia 37.8. Lakini pia nilizungumza kwamba deni la ndani ni shilingi bilioni 158.3 na deni la nje ni shilinig bilioni 361.4. Sababu za kuongezeka kwa deni hili tuliziweka wazi kwamba moja ni kutolewa kwa fedha za ujenzi wa jengo la *Terminal III* ambazo fedha hizo ni za awamu ya mwanzo zimetolewa jumla ya dola za Kimarekani milioni 35.2 sawa na Tsh. bilioni 78.9. Lakini vile vile tulikopa ndani shilingi bilioni 30 tulipangiwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 tukope jumla ya shilingi bilioni 30 lakini tumekopa shilingi bilioni 20. Lakini pia tumelipa viinua mgongo kwa wastaafu vya jumla ya shilingi bilioni 17.7 kwa wastaafu 1,075. Lakini pia tulizungumzia mabadiliko ya kiwango cha kubadilishia fedha kwa maana ya *exchange rate* hivyo vitu ndivyo vilivyo sababisha hili deni letu kukua.

Mhe. Spika, lakini pamoja na kukua huko tulisema kwamba bado deni hili ni asilimia 16.8 tu ya pato letu la Taifa. Kukopa ni lazima kwa nchi yoyote na nchi zote zinakopa. Katika kuharakisha maendeleo lazima tukope, lakini katika kukopa tunatakiwa tuwe makini na kile tunachokikopa na sababu ya kukopea, hilo moja. Lakini la pili, tusivuke kile kiwango ambacho kinakubalika cha deni. Kwa maana kiwango kinachokubalika cha deni ni asilimia 50 ya pato la Taifa, kuna nchi zinakopa mpaka asilimia 45 ya pato lao la Taifa. Kwa hivyo, kiwango hicho ndio kinachoamua uwezo wako wa kurudisha deni. Kwetu sisi tupo kwenye asilimia 16.8, bado ni kiwango cha chini sana. Kwa hivyo, bado deni letu sisi tunaweza kulihimili, mapato yetu yanaweza kulipa deni hilo na bado tuna nafasi zaidi ya kuendelea kukopa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna suala jengine hili ambalo naamini kabisa Waheshimiwa Wajumbe wengi wanalisubiri kwa hamu sana, na ni suala la ulinzi wa viwanda vyetu. Lakini suala ambalo nililizungumza kupunguza unafuu wa ushuru wa forodha ambao tunautoa kwa bidhaa hasa za mchele na sukari na Waheshimiwa Wajumbe wengi walilizungumza suala

hili. Nakumbuka Mhe. Hamza Hassan Juma alizungumzia kwamba yote anayakubali na namshukuru sana lakini hili alitaka maelezo ya kina.

Mhe. Spika, naomba hapa niseme kwamba kwanza waheshimiwa naomba sana mtuamini lakini pia muiamini serikali yenu. Serikali ambayo inaongozwa na Rais makini sana Dkt. Ali Mohamed Shein. Nyinyi ni mashahidi kwamba wakati wote Dkt. Shein anaangalia maslahi ya wananchi kwanza. Mambo yote tunayoyafanya haya au mnayoyaona yanafanywa ni kwa maelekezo yake lakini yanamlenga mwananchi, hasa mwananchi wa chini katika nchi hii. Kwa hivyo, mimi siamini kwamba itatokea hata siku moja tuje na wazo hapa ambalo linapingana na azma hiyo ya Mhe. Rais, Dkt. Ali Mohamed Shein, lakini vile vile azma na sera za Chama chetu cha Mapinduzi hakuna suala hilo hata siku moja. *(Makofi)*

Lakini lazima tukubali, na wakati mwengine lazima tukubali kuwaambia pia na wananchi wetu ukweli na wakaelewa, tusitake kuwafungia wananchi wetu katika *cocoon* tukawa tumewafungia wakati dunia inabadilika na inabadilika kwa kasi sana. Lakini hata ukanda wetu huu unabadilika na unabadilika kwa kiasi kikubwa sana. Katika ushuru unaotozwa kwa bidhaa muhimu za chakula nadhani hapa Zanzibar ndio tunatoza kiwango cha ushuru cha chini kabisa. Wakati *East African rate* ni asilimia mia. Kwa mfano, tukichukua bidhaa ya sukari inatakiwa itozwe asilimia mia moja ya dola 460, ile *declaration value* thamani ya uingizaji wenyewe ya tani moja dola 460. *East African rate* ichajiwe asilimia mia moja. Sisi hapa tunachaji asilimia 10 ushuru wa forodha ni kiwango cha chini sana, lakini hiyo tulikuwa tunafanya wakati ule ambapo hatuna uzalishaji wa ndani, sasa tuna kiwanda tukiendelea kuchaji kiwango hicho kidogo kile kiwanda hakitodumu, kile kiwanda hakitokuwa na soko kwa sababu yule hataweza kushindana na sukari inayoagizwa kutoka nje.

Lakini vile vile tunauona ugumu na wao hao Kiwanda cha Sukari kupeleka sukari yao nje ya Zanzibar, sasa wataiuza wapi. Sisi huku tunataka ku-*promote* viwanda kwa maana tuna sera ya kukuza viwanda nchini kwa ajli ya kuchangia maendeleo ya uchumi wa nchi hii, hiyo moja tuna *policy objective* hiyo. Lakini kwa upande wa pili tuna *policy objective* ya kuwalinda walaji wananchi wetu ili waweze kumudu gharama za maisha. Kwa hivyo, tuna *policy objective* mbili na zote tunazihitaji, madam zote tunazihitaji sasa ni lazima tufanye *trado,* tutafute *balance,* tutafute pahala *point* ambayo itatusaidia kukuza viwanda lakini vile vile kuwasaidia wananchi wetu. Jambo hilo ndio serikali inalolifanya, hatukusudii kuweka viwango vitakavyowaumiza wananchi wa nchi hii, lakini tunakaa kujadiliana kile kiwango ambacho kitasaidia kukuza viwanda vyetu, kukuza fursa za ajira na kukuza mchango wa uchumi wa hivyo viwanda, mchango wake katika uchumi na maendeleo ya nchi hii.

Mhe. Spika, mimi nina bahati nzuri lazima niseme hapa kwamba nina watu wataalam wazuri sana katika masuala ya kodi. Nina Katibu Mkuu Ndg. Khamis Mussa ni mtaalam mzuri sana katika masuala ya kodi. Lakini pia nina Mkurugenzi wa Sera za Kodi ni mtaalam mzuri sana, tuna Ndg. Hafidh pale ni wataalam wazuri sana, tuna Kamishna Seif hawa wote wamebobea katika masuala haya, lakini tuna Baraza makini la Mawaziri

ambalo huwa tunajadiliana katika masuala haya na mwisho wa habari tunafuata maelekezo sahihi ya Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kwa hili mimi nashauri sana Waheshimiwa Wajumbe tusiwe na wasi wasi, viwanda tunavitaka lakini vile vile tunataka kuwalinda wananchi wetu ili waweze kumudu gharama za maisha. Sasa hayo yote mawili lazima tuyape nafasi na katika kuyapa nafasi si vibaya kuongeza kidogo ushuru kwa bidhaa hizo ili yote mawili tuweze kuyafanikisha na ndicho kinachokusudiwa na ndicho kilichoelezwa katika hotuba yangu. Tukiendelea tu kuwadanganya wananchi kwamba bado tuwe na viwango vya chini, kwa sababu sisi kwa mfano sukari tunachaji asilimia 10 lakini *declaration value* ya dola 200 sio ile ya *East Africa* ambayo ni dola 460 wakati inatakiwa ichajiwe kiwango cha asilimia 100. Kwa maana tani moja ingechajiwa dola 460, sisi tunachaji asilimia 10 ya dola 200, ni kiwango kidogo. Kwa hivyo, kuongeza kidogo si tatizo, tusije tukapeleka *signal* mbaya kwa wananchi wakaona kwamba bei zitapanda, bado kabisa serikali hii haina dhamira hiyo.

Mhe. Spika, nitoe mfano mwengine, sisi tunataka kukuza viwanda na wakati tulipopitisha hotuba hapa ya Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda tumefurahia ule mkakati wa serikali wa kukuza viwanda nchini, sasa jitihada za kukuza viwanda hivyo ni hii. Kwa sababu hivi sasa mchango wa viwanda kwetu ni asilimia ndogo sana inachangia katika pato la Taifa wastani wa asilimia 17 tu ni kiwango kidogo. Uchumi wetu bado unategemea sekta za asili *(traditional sector)* za kilimo na hakuna nchi ambayo inategemea *traditional sector* katika kukuza uchumi wake, hata hizo nchi zinazoendelea zinaitwa nchi za viwanda, zimeendelea kwa sababu zina viwanda sio kilimo peke yake. Sasa hapa ni lazima tukubaliane katika hili.

Mhe. Spika, lakini pia unapotaka kukuza hata hicho kilimo chenyewe basi lazima kiwe na *linkage* za sekta za viwanda, lazima ukiunganishe bidhaa zinazozalishwa katika kilimo ziende viwandani ili ziweze kusarifiwa na kuweza kupata soko, lakini vile vile kukuza ajira na fursa za ajira katika ile *valin chain* lazima ifanyike hivyo.

Mhe. Spika, hivi sasa tunatarajia kutekeleza mradi wa umwagiliaji maji katika sekta hii, na tayari tumeshaukubali kupitia mkopo nafuu wa serikali ya Korea ya Kusini, mradi ule ukifanikiwa na tukiweza kuongeza uzalishaji bado tutakuja na nafasi ya kuwalinda wazalishaji, hatutakuwa na nafasi tena ya kuagiza michele ya bei rahisi huko nje tuje tuwauwe wakulima wetu haitowezekana. Kuna wakati fulani nilipata fursa ya kwenda Japan katika nchi inayozalisha mchele kwa gharama kubwa sana ni Japan lakini bado wanaendelea na juhudi za kuzalisha mchele huo na hawategemei mchele rahisi kutoka kwa majirani zao Vietnam. Kwa hivyo, hili ni jambo linalokubalika, leo tunaanza na viwanda viwili hivi, Kiwanda cha Unga wa Ngano, Kiwanda cha Sukari kutafuta unafuu wa kote kote kwenye viwanda lakini vile vile unafuu kwa watumiaji walaji wa bidhaa hizo ambao ni wananchi wetu. Tunatafuta unafuu huo lakini hatuna budi kuondoka hapa tulipo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nitoe mfano mwengine katika miaka ya 90 mapato yetu kwa asilimia kubwa yalikuwa yanategemea mapato kutoka Idara ya Forodha, asilimia kubwa sana karibu

asilimia 67 zilikuwa zinatokana na mapato yanayokusanywa na Idara ya Forodha. Kwa hivyo, uchumi wetu ulikuwa unategemea zaidi huduma za biashara na mataifa ya nje. Unapoagiza vitu kutoka nje ujue kwamba unasaidia kukuza fursa za ajira katika nchi zile, na kwako wewe unabaki na janga la vijana wako kukosa fursa za ajira. Nashukuru sana kwa mwaka 2018/2019 makusanyo ya Idara ya Forodha yatakuwa ni karibu bilioni 165.9 na kwa makusanyo ya ndani ambayo tunayatarajia ya shilingi bilioni 807.5 hiyo ni asilimia 20.5. Kwa hivyo, uchumi wetu unaimarika kwa kutegemea mapato ya ndani zaidi kuliko biashara na mataifa ya nje. *(Makofi)*

Mh. Spika, muelekeo huo ndio muelekeo sahihi ambao nchi yetu inabidi ielekee huko. Kwa hivyo, ningewaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wote waliokuwa na wasi wasi na jambo hili waondokane na wasiwasi huo, kuna haja ya kulinda viwanda vyetu, Kiwanda cha Sukari kilikwisha kufa, waliopata fursa mimi nilipata fursa ya kukitembelea kabla ya kuchukuliwa vile, kilikuwa ni chuma chakavu. Sasa mwekezaji huyu ametumia fedha nyingi kuwekeza kiwanda kile, tunahitaji kama serikali kutoa muelekeo wa kukisaidia kiwanda kile ili tuweze kukuza fursa za ajira na kuweza kuanza angalau viwanda vyetu viwili hivi basi tuweze kupata kukua. Hata kwenye kiwanda kwa mfano Kiwanda cha Maziwa cha Bakhresa kitakapofika muda uwezo wetu wa kuzalisha maziwa wa ndani utakapoimarika ni lazima tutakuja na *measure* za kuhakikisha kwamba tunaongeza ushuru kwa bidhaa zinazotoka nje. Hilo haliwezi kuepukika kama tunataka kwenda na sera ya kukuza fursa za viwanda hapa nchini. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nadhani Waheshimiwa Wajumbe wamenielewa sana kwenye hili, Mhe. Jaku Hashim Ayoub alilizungumza hili, lakini vile vile na Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf wote walilizungumza suala hili naomba sana tukubaliane tuondoke kwenye *cocoon* hii tuanze kuwafungulia wananchi wauone ukweli wa dunia, wauone ukweli wa kanda yetu zinavyoendelea kiuchumi na sisi tuingie katika mkondo huo hasa katika kukuza viwanda nchini. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Jaku Hashim Ayoub alizungumzia suala la mabadiliko katika jengo la *Chawl Building*, ni kweli kuna mabadiliko kidogo sana yaliyofanyika, na mabadiliko hayo yamefanyika hasa ile sehemu yenye mkabala na duka la Muzammil, lakini mabadiliko yenyewe yaliyofanyika ni kuliondoa duka lililokuwa linauza *perfume* katika sehemu ile kwa ajili ya kuweka ngazi ya kwenda juu kwenye *apartments*. Hayo ni mabadiliko yalikuwa ya lazima kufanyika katika jengo lile. Lakini vile vile upande wa marikiti huku kuna sehemu ilikuwa kuna mlango lakini nao umeondolewa kwa ajili ya kuweka *ATM* ni huduma muhimu katika eneo lile la kibiashara. Kwa hivyo, hayo ndio mabadiliko lakini mambo mengine yote yamebaki kama yalivyokuwa isipokuwa umefanyika ukarabati wa kuliboresha jengo lile.

Mhe. Spika, kuhusu *ZRB* kutumia nguvu, mimi niwahakikishie kwamba *ZRB* itaendelea kutumia busara, hekma na haya ndio yanayofanyika, wale wanaodaiwa kodi wengi wanaitwa, kunakuwepo na mazungumzo wanasikilizwa hoja zao na wengine wanaletwa kwangu tunazungumza nao na mwisho wa habari tunakubaliana jinsi ya kulipa madeni yao ya kodi. Lakini kubwa katika hili ningewaomba sana wenzetu wote walipa kodi wakalipa kodi kwa hiari kuepusha usumbufu wowote ule, na kama wana hoja za msingi

taratibu za kisheria zimewekwa za kutoa malalamiko yao, wafuate huko kama wana malalamiko lakini hakuna haja ya kulazimisha matumizi ya nguvu katika ulipaji wa kodi, kodi hii ni kwa ajili yetu sote pamoja na wao. Uchumi wa nchi yetu utakapoimarika utakapokua utatoa fursa zaidi za kibiashara na uwekezaji ambao zitawanufaisha na wao pia, kwa hivyo hakuna sababu ya watu kufikiria kujilimbikizia wao wakati uchumi wa nchi unadorora, uchumi lazima ukue ili na wao wapate fursa zaidi za biashara lakini pia na wawekezaji wapate fursa zaidi za uwekezaji.

Mhe. Spika, suala la wakulima wa mwani kusaidiwa hili linafanyiwa kazi serikali imewahi kutoa boti kwa wakulima wa mwani, mafunzo wanapatiwa, lakini huduma za utafiti vile vile zinafanywa kupitia wizara inayohusika Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Lakini hivi karibuni serikali inadhamiria kuweka Kiwanda cha Usarifu wa Mwani na mimi mwenyewe nakumbuka kwa maelekezo ya Mhe. Rais nimefanya mazungumzo na *ADB*, nimefanya mazungumzo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili kuona suala la kuweka usarifu wa zao la mwani linapewa kipaumbele katika misaada lakini vile vile katika ufadhili utakaotolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Kwa hivyo, suala hilo lipo na linafanyiwa kazi vizuri.

Mhe. Ali Suleiman Ali mchango wako tunauthamini sana, pongezi zote ulizotoa, lakini haja ya kusimamia vizuri tenda tunachukua, matengenezo ya bandari zetu ikiwemo bandari ya Wete na Mangapwani nafikiri na ya Mpigaduri kama nilivyosema serikali inachukua juhudi ya kuhakikisha kuwa tunakuwa na bandari nyingi katika maeneo yetu ya Unguja na Pemba, ili tuweze kukuza usafirishaji wa watu lakini vile vile bidhaa katika pande zetu mbili za Jamhuri na pande zetu mbili za Zanzibar Unguja na Pemba, lakini pia baina ya Zanzibar na maeneo mengine. Ujenzi wa barabara kujenga vikuta vya pembeni ushauri wako pia tunauchukua.

Mhe. Spika, nachukua pia ushauri wa Mhe. Simai Mohammed Said wa kwamba barabara inayojengwa ya Bububu hadi Mkokotoni iwekewe fursa maalum kwa ajili ya huduma *facilities* mbali mbali ikiwemo *optic fiber,* alizungumzia suala la maji, suala la umeme, nadhani hilo ni suala la sekta ambayo watalishughulikia. Mhe. Simai pia alizungumzia kuhusu shamba la Bagamoyo na hapa naomba nilieleze hili kwamba matumizi ya shamba lile yamebadilika, wenzetu wa Halmashauri ya Bagamoyo wamebadilisha matumizi ya eneo lote lile na wametuarifu rasmi kama serikali na serikali imeridhia. Sasa badala ya kuimarisha masuala ya kilimo na ufugaji katika shamba lile lililokuwa shamba la Bagamoyo RAZABA sasa litatumika kwa ajili ya majengo ya makaazi na majengo ya biashara. Kwa hivyo, hili tayari serikali imeshaliridhia na linatokana na mapendekezo ya Halmashauri ya Bagamoyo kwamba lile eneo sasa ni mji hatuwezi tena tukaenda tukaanza kufuga katika maeneo ya mji, hatuwezi kufuga ng'ombe katika maeneo ya mji.

Mhe. Spika, suala la *withholding tax* nilisema katika hotuba yangu kwamba tunaandaa muongozo, baada ya kuandaa muongozo huo ile *Withholding Tax Guidelines* tutatoa taaluma kwa wananchi ili waweze kuielewa. Mhe. Simai Mohammed Said asiwe na wasi wasi hilo linafanyiwa kazi. Madai ya wananchi kwa iliyokuwa benki ya *FBME* hili nimeshalieleza hata katika kikao hiki kinachoendelea wakati najibu maswali ya Barazani nilijibu hili ya kwamba suala hili hivi sasa lipo kwa mfilisi na mfilisi ni *Depositer*

Insurance Board (Bodi ya Amana) iliyo chini ya *BOT* na kwa hatua za mwanzo tayari wale wote waliokuwa na akaunti zao pale wamelipwa shilingi 1,500,000/- na hii ni kwa mujibu wa sheria. Lakini pia nilizungumza na naomba niendelee tena kuzungumza leo kwamba kupitia Bodi hii ya Amana wanaendelea kuhakiki madeni na mali za benki hiyo na serikali itaendelea kufuatilia ili kuona haki za wananchi wake zinapatikana. Sisi kama serikali tukishirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Benki Kuu bado tutaendelea kulisimamia suala hili ili kuona haki zinapatikana za wale waliokuwa na akaunti katika benki hii. Jambo lenyewe linachukua muda kwa hivyo ningeomba sana wale wote walioathirika na suala hili basi wawe na ustahamivu wakati linaendelea kushughulikiwa.

Mhe. Spika, Mhe. Simai Mohammed Said pia alitaka mambo kadhaa katika Jimbo la Tunguu lakini hasa katika eneo lake la Tunguu kasema kuna wakaazi wengi wanaongezeka, shughuli za biashara. Tunakubaliana na fikra hiyo na maendeleo yatapelekwa, maendeleo ya fursa za kiuchumi na kijamii zitakuwa zinapelekwa katika maeneo yote kwa mujibu wa uwezo wa serikali, lakini vile vile na haja itakayojitokeza katika maendeleo. Nilikwishamuahidi hapa wakati ninajibu swali lake kwamba hata huduma za *ATM* katika maeneo yale Benki ya Watu wa Zanzibar itayazingatia maombi yao, ili kuona kama kuna haja ya kuweka huduma hizo katika maeneo *strategic* basi itafanyika kama walivyoomba.

Mhe. Spika, suala la *Skills Devolopment Levy (SDL)* alizungumzia kwamba skuli za *private* zimeomba kwamba zisilipe *SDL*. Kwanza, hili ni suala la kisheria, lakini vile vile kupitia Jumuiya ya Wamiliki wa Skuli Binafsi walileta ombi la kuomba kwamba *SDL* iondolewe katika skuli za *private,* waliomba na hili sisi tulilipeleka katika Kamati ya Wadau kwa maana *Tax Reform, Tax Force* walikaa wakalijadili hili na wakaona kwamba ombi hili halina mashiko. Kwa hivyo, bado tunasisitiza sisi kama ilivyo kwa sekta nyengine hatuna haja ya kubagua wao wanafanya biashara, basi ada hii na wao wanapaswa kulipa, wafanyabiashara wailipe ada hii. Lakini hoja yao walikuwa wakizungumzia kwamba wao pia wanatengeneza ujuzi, lakini kuna hoja nyengine inayozungumza kwamba hata hao walimu wanaowatumia walifundishwa, walijengewa ujuzi, na walijengewa ujuzi kwa kutumia fedha, na fedha ndio hizi kwa hivyo hakuna sababu ya kusema wao wasilipe ada hii, ni suala lile lile tulipe kodi, tulipe ada kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma alizungumzia suala la kuongeza, alizungumzia kwamba kuna baadhi na hasa alizungumzia mfumo wa kupitisha bajeti zetu, akasema bajeti ikishafika hapa inakuwa vigumu sasa kupata fedha kwa ajili ya yale mambo ambayo Waheshimiwa Wawakilishi wanaona yana umuhimu zaidi. Alitoa mfano wa *CDF* ni kweli hili tulilizungumza hata kwenye Kamati ya Bajeti kuona haja hiyo kama Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili wanaweza kuongezewa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kutoka kiwango cha sasa cha milioni 20 kwa mwaka hadi milioni 25. Tukasema kwa sasa hivi hali hiyo haiwezekani kutokana na hali ya mapato yetu, lakini vile vile na majukumu mengi tuliyojipangia katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Lakini tulisema hali ikiimarika ya uchumi wetu na mapato yetu, basi kama huko nyuma serikali ilivyofikiria kuongeza kiwango hichi kitaongezwa, kiwango hichi kilikuwa ni shilingi milioni tano tu huko nyuma kabla ya kuundwa kwa Sheria ya Mfuko wa Jimbo, baada ya kuundwa kwa sheria hiyo kima hichi kiliongezeka hadi kikawa shilingi milioni kumi, kikaongezeka tena kikawa milioni kumi na tano, sasa hivi shilingi milioni ishirini. Hali yetu ikiimarika na tuombe hivyo Mwenyezi Mungu atujaalie hali yetu iimarike kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kiwango kitaongezwa zaidi. Mimi mwenyewe kweli nina jimbo ni Mwakilishi wa Jimbo na ningetamani pia hata kingefika shilingi milioni hamsini kama kinakwenda kuhudumia wananchi kama uwezo huo upo basi kifanyike, lakini kwa sasa tustahamili kwa kiwango ambacho kipo hichi kinatokana na uwezo wa ukusanyaji wetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, deni la *ZECO* alisema aaa kwani wakati tunadaiana kuna ulazima kwamba lazima watujibu, kiserikali ni lazima watujibu kwa sababu kuna leo na kesho, sisi tuliokuwepo leo sio tutakaokuwepo kesho, kwa hivyo maandishi ni muhimu katika masuala yoyote ya makubaliano baina na serikali zetu mbili. Ndio maana bado sisi tunaendelea kulifuatilia suala hili ili basi yale mapendekezo ambayo tumeyatoa sisi kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yajibiwe kwa maandishi ya kukubalika kwake ili deni hili liweze kusawazishwa.
Visima vya Ras Al Khaimah 150 tumefikia hatua gani. Mwaka jana vilipangwa kuimarishwa visima 20 na tuko katika hatua nzuri, lakini kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imepangwa tuimarishe visima vyengine 20, na lengo kwamba hata ikifika mwaka 2020 basi visima vyote 150 viwe vimekamilika. Hii kuchimba visima ni suala moja, kuchimba kisima ni rahisi, lakini kuweka miundombinu yake na kuweka mabomba ya kuunganisha ni gharama kubwa sana na ni lazima serikali ifanye taratibu kutokana na hali na uwezo wa nchi. Kwa hivyo, tukubali kwamba mwaka jana tuliweka visima 20, mwaka huu unaokuja wa fedha tutatengeneza tena visima 20, lakini baadae nitazungumza suala zima la uimarishaji wa sekta ya maji ambalo kwa kweli linatoa matumaini makubwa sana. Lazima tupongeze sana juhudi za serikali kutokana na mwelekeo huo. *(Makofi)*

Suala la unafuu nimeshalizungumza, suala la Ziwa la Mwanakwerekwe Mhe. Hamza Hassan Juma alizungumzia ni vyema yale maji yasiondolewe tuyajengee na hasa kwa kuhifadhi vyanzo vya maji. Ni wazo moja ambalo amelitoa Mhe. Hamza lakini kwa mazingira ya bwawa lile lilipo ni vyema akubaliane na mipango ya serikali ya kuliondoa ziwa lile. Kwa sababu linatokana na kuchimbwa mchanga katika eneo lile na maafa mengi yanatokea katika sehemu ile, kwa hivyo si vyema kitu ambacho hakikuwa *designed* katika mipango miji yetu tukakiweka tu kwa sababu kiko pale. Tukubali kukiondoa, niseme tu kupitia *ZUSP* awamu ya pili tayari wapo katika hatua za mwisho kuandaa michoro kwa ajili ya kuyaondoa maji yale kupitia kwa Mabata, lakini yatapitia Amani yatakwenda zake mpaka Sebleni, yataondoa maji ya Sebleni yatapita pale Kibandamaiti, Kwa Juma Pweza yatakwenda zake mpaka kwa Abass Hussein na kuishia baharini. *(Makofi)*

Mhe. Spika, maji yale tuyaondoe lakini pia serikali ina mpango wa kuinua barabara katika eneo lile ili sasa iwe salama barabara ile kupitika kwa wakati wote, na hilo

litafanywa ndani ya mwaka wa fedha 2018/2019 sambamba na kuondoa maji katika barabara ya Uwanja wa Ndege lakini vile vile kutengeneza daraja katika eneo la Jumbi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil alizungumzia suala la mashirika ya umma kuchangia mapato ya serikali, ulizungumza mengi na mengi ya pongezi tunayapokea na suala hili la mashirika ya umma kwa kweli tunalisimamia kikamilifu na tunahakikisha kwamba mashirika yote yanachangia *dividend* kwa serikali kama azma ya serikali ilivyokusudia. Mhe. Spika, katika hili baadhi ya mashirika wanajua kwamba hatuna masihara nalo mapato lazima yatokane na mashirika hayo kwa sababu yameanzishwa kwa ajili ya kufanya biashara. *(Makofi)*

Mhe. Mohamed Said Mohamed alizungumza suala la pato la Taifa alitaka kujua linatokana na nini hasa hili pato la Taifa. Kimahesabu pato la Taifa linajumuisha matumizi yetu sote *consumption,* lakini na uwekezaji wote *investment,* lakini na matumizi yote ya serikali *(Government Expenditure),* lakini pia na thamani ya bidhaa zinazoingizwa nchini (*imports),* lakini katika *formula* hiyo sasa baada ya kuyajumlisha yote hayo unatoa thamani ya bidhaa ambazo tunazisafirisha nje ya nchi, hapo ndio unapata pato la Taifa kwa maana ya *GDP*. Ni kiashiria muhimu sana cha ukuaji wa uchumi na kinatoa *comparison* baina ya nchi na nchi.

Lakini pia kuna suala zima la pato la Taifa kwa mtu, maana yake ukishakulipata pato la Taifa unagawa sasa na idadi ya wananchi katika nchi. Hicho nacho ni kiashiria muhimu sana cha uchumi kwa maana ya *economic indicator,* lakini hakimainishi kwamba ukiwa na kiwango kikubwa cha *per capita income* kwamba wewe ni tajiri hapana, inategemea na idadi ya wananchi wako na pato lako la taifa. Vipo viashiria vyengine ambavyo vinapimiwa pia kujua kiwango cha umaskini kama *gini coefficient* kwa maana sasa ule mgawanyiko wa hilo pato la Taifa kwa makundi mbali mbali na watu mbali mbali katika jamii.

Sasa kwa hapa Zanzibar sisi familia zetu kwa wastani zina watu watano nukta moja (5.1). Sasa Mhe. Mohamed Said Mohamed alizungumzia kwamba shilingi hizi elfu tano akazichambua kwa maana atanunua samaki, ananunua mchele, ananunua mafuta. Lakini tunachozungumza sisi elfu tano hiyo ni kwa kila mtu mpaka mtoto aliyezaliwa leo ambapo hali sawa na mtu ambaye mwenye nguvu na anafanya kazi, lakini wote hao katika *average* hii wamejumuishwa pamoja. Lakini hata wazee waliopindukia miaka 75 nao wamo humo, sasa kwa kila mtu kwa familia ya watu watano unazungumzia shilingi 25,000 kwa hesabu rahisi kabisa. Lakini hata ukiichukua hii shilingi elfu tano yenyewe hii ni zaidi ya dola mbili au karibu dola mbili na kiwango cha kimataifa cha umaskini ni kiwango cha matumizi ya dola moja kwa mtu tumeshakivuka. Kwa hivyo, tunavyozungumzia kwamba hali yetu ya uchumi ni nzuri na inaimarika tukubali hivyo kwa vigezo hivi ambavyo nimejaribu kuvielezea. *(Makofi)*

Alizungumzia suala la Tume ya Pamoja ya Fedha ni eneo muhimu kwa sababu mambo mengi sana yanahitaji uwepo kwa Tume ya Pamoja ya Fedha na suala ambalo lipo kwa mujibu wa katiba. Sisi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tunaendelea kuzungumza na

wenzetu na tutafanya kikao chengine baina ya Wizara ya Fedha na Mipango ya SMZ na Wizara ya Fedha na Mipango ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuangalia yale maeneo ambayo bado hadi sasa yanakuwa ni changamoto za Muungano, ili tuweze kuyatatua au kutoa maoni katika kamati ile kuu inayoongozwa na Mhe. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Alizungumzia pia suala la kutoa elimu kuhusu ushuru wa *stamp,* hili kweli ni muhimu na tuliahidi tutafanya kazi hiyo, tumekuwa tukiifanya na tutaendelea katika mwaka wa fedha ujao kwa kuendelea kuwaelimisha wananchi na walipa kodi wote kuhusiana na umhimu na viwango vya ushuru wa *stamp* viliopo.

Mhe. Spika, Mhe. Rashid Makame Shamsi alitoa pongezi nae alisema kwa kiasi gani tumeweza kutekeleza vipaumbele kwa mwaka 2017/2018, tumetekeleza kwa kiasi kikubwa. Mimi nikuombe tu mheshimiwa na najua kabisa utanikubalia kwa hilo ukisoma mapitio ya hali ya uchumi kwa mwaka 2017 na utekelezaji wa programu za maendeleo kwa mwaka 2017/2018, tumeeleza kila programu na hatua zilizofikiwa za utekelezaji. Ningekuomba sana ukipitie najua ni kitabu kikubwa lakini utapata kwa ukamilifu yepi tumeweza kuyatekeleza na kwa kiasi gani na yepi ambayo bado yamebaki kutekelezwa kwa kiasi gani. Lakini tumeweka *commitment* kwa ile miradi na programu ambayo haikuweza kukamilika katika mwaka wa fedha 2017/2018 itakamilishwa. Ni *commitment* ya mwanzo ya kuhakikisha kwamba inatekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2018/2019. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Suleiman Sarahan Said alitupa ushauri mwingi na maoni yake tunayapokea na tunamshukuru sana, lakini alizungumzia kuhusiana na vifaa vya ujenzi wa barabara *UUB* na katika hili niseme kwamba mchakato wa manunuzi kidogo ulicheleweshwa. Kwa sababu ulihitaji umakini zaidi wa kujua *specification,* ili zile zana zinazonunuliwa zisije zikanunuliwa halafu zisiwe na *value for money* au kikaja kitu ambacho sicho kilichotarajiwa. Kwa hivyo, wenzetu wa Wizara inayohusika ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji walifanya kazi hiyo na hivi juzi mwezi wa Mei wametuletea sasa *quotation* zao na maombi ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mtambo wa lami, lakini vile vile kwa ununuzi wa *spare* na lile *paver*. Kwa hivyo, kwa hatua ya mwanzo serikali itatoa fedha hizo katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Spika, suala la kulinda viwanda vya ndani tayari nimeshalieleza, eneo la Bwawani alitaka liendelee kutumika kuwekwa kwa makontena. Hili niseme tu kwamba azma ya serikali ya eneo lile ni kulitumia kwa ajili ya uwekezaji, kuweka haiba nzuri ya mji, lakini vile vile kuweka maduka ya kisasa katika eneo lile, kuitengeneza ile hoteli yetu kuwa hoteli ya kisasa, lakini pia kuweka kumbi za mikutano shughuli ambazo zitaongeza na kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi katika nchi yetu. Tukiwa na huduma hizi tutaweza kuleta mikutano mikubwa ya kimataifa na wakija hapa watatumia huduma zetu, watatumia hoteli, watatumia kila kitu. Kwa hivyo, hii watakuwa wanachangia zaidi katika ukuaji wa uchumi. Maeneo kwa ajili ya kuweka makontena yapo mengi kwa sasa hivi yapo kwa muda lakini maeneo yapo Maruhubi tunaweza kutumia kuweka huduma kama hii. Mimi bado nakuomba Mhe. Suleiman Sarahan Said tuliache eneo hili liendelee kubaki kuwa ni eneo la uwekezaji. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna suala ambalo lilizungumzwa na watu wengi kuhusiana na maji, hili lilizungumzwa na Mhe. Omar Seif Abeid lakini na Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini. Niseme kwamba serikali imeweka malengo *(target)* kwamba vijiji vyote vya Unguja na Pemba viwe vimefikiwa na maji safi na salama ifikapo mwaka 2020. Kwa namna hiyo, sasa hivi usambazaji wa maji upo kwa asilimia 70.2 kwa maeneo ya vijijini, lakini basi ikifika mwaka 2020 angalau basi tuwe tumefikia asilimia 88.3, hilo ndio lengo lililowekwa kwa mujibu wa Dira ya Maendeleo na *MKUZA III.* Lakini kwa mijini lengo letu lilikuwa hivi sasa tuko asilimia 87. 2 tufikie asilimia 98.4 ikifika mwaka 2020. Juhudi kubwa sana zinafanywa na serikali yetu katika kuhakikisha kwamba maji safi na salama yanapatikana katika maeneo yote ya Unguja na Pemba. Tuna taarifa kwamba kwa maeneo ya Pemba upatikanaji wa maji upo katika hali nzuri sana. *(Makofi)*
Mhe. Spika, matatizo yaliyopo hapa katika kisiwa cha Unguja yatatatuliwa kwa serikali kutekeleza mipango na programu za maendeleo nyingi ikiwemo programu ya *ADB* ambayo inaitwa *ADF 12.* Programu hii imechimba visima 9 na ukarabati wa visima 21 na kwa sasa vyote vimeshakamilika, lakini kuna mradi huu unaofadhiliwa na mkopo nafuu wa *Exim Bank* ya India una jumla ya dola za Kimarekani milioni 92. Maeneo mengi yatanufaika na mradi huu yakiwemo maeneo ya Mfenesini na vitongoji vyake vyote, maeneo ya Dole, Masingini, Mkorogo, Kitutani, Maungani na Dimani.

Lakini kwa ule mradi wa *ADB* unakusudia kuchimba visima katika maeneo ya Bumbwisudi na kulaza mabomba kuja nayo mabomba hayo mpaka kwenye matangi ya Welezo, lakini pia yashushwe mpaka kwenye matangi ya Mnara wa mbao, lakini vile vile matangi yaliyopo pale Saateni ambapo panachimbwa tangi jengine. Wenzetu hawa wa *ZAWA* wanakusudia kwamba matangi hayo yatakapokamilika basi eneo lote la Mji Mkongwe na maeneo ya jirani yaweze kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Lakini kuna mradi mwengine wa *JICA* ambao una karibu dola milioni 100 nao unakuja kwa ajili ya shughuli za maji, upembuzi yakinifu umeshafanyika na tunatarajia kusaini mkataba huo mwezi Agosti mwaka huu. Maeneo mengine yatakayonufaika ni Welezo, Welezo ya Juu, Welezo ya Chini, Migombani na katika sehemu za magharibi ya Migombani nayo yote yatanufaika na maji safi na salama.

Lakini pia Serikali ya China nayo itatoa msaada wake katika uchimbaji wa visima vipya na kuweka mabomba katika maeneo mbali mbali ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Suala la visima vya Ras Al Khaimah tayari nimeshalitolea ufafanuzi. Kwa hivyo, hiyo ndio hali ilivyo na zaidi ya dola za Kimarekani milioni 200 zitatumika katika kugharamia miradi ya maji. Tunatarajia sana kwamba miradi ya maji itakapokamilika tatizo la maji kama halitoondoka basi litakuwa limepata ufumbuzi kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohammedali alizungumzia suala la Kamati ya Fedha ya Pamoja nalo nimeshalizungumza. Lakini pia alizungumzia suala la fedha za *TTCL,* mgao ambao umefanyika hivi karibuni unaotokana na faida ya *TTCL*. Ni kweli tunazo taarifa hizo kwamba hivi karibuni *TTCL* ilitoa *devidend* kwa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini kama nilivyosema kwa bahati mbaya sana ile akaunti ya pamoja ambayo ilitakiwa iwepo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania bado haijakuwepo, kwa hivyo hakuna utaratibu rasmi wa kugawana mapato ya Muungano. Ni suala ambalo tunaendelea kulizungumza na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atatujaalia litapata ufumbuzi wake kwa sababu pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zina nia safi kabisa ya kuimarisha Muungano. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf alizungumzia suala la nyumba za *ZSSF* za Mbweni kwamba hizo nyumba sio za bei nafuu na akataka nyumba zitakazojengwa Kwahani na zitakazojengwa sehemu za Chumbuni na maeneo mengineyo basi ziwe nyumba za bei nafuu zitakazoweza kuwanufaisha wananchi. Hilo hasa ndio lengo la serikali.

Nyumba za Mbweni jamani lile eneo ni *very prime*, alizungumzia hapa kwamba labda nyumba zile zingekuwa na thamani ya milioni 80. Lakini kiwanja tu katika eneo lile ni zaidi ya milioni 100, sasa utajenga nyumba gani pale iwe ya bei nafuu. Lakini Kwahani kutakuwepo na nyumba mchanganyiko na ndio madhumuni ambayo yanakusudiwa na bahati nzuri ile kampuni wamenipigia simu wanaingia kesho kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba wanaanzisha makaazi yao hapa, wanafungua ofisi yao hapa, wanakamilisha taratibu zote za kusajili kampuni yao na wapo tayari kwa ajili kuweka saini na kuanza kazi za ujenzi katika maeneo yale. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf alizungumzia suala la umeme wa jua, upepo na tupunguze utegemezi wa *TANESCO*. Ni kweli na serikali ina azma hii ya kuwa na matumizi ya nishati mbadala kwa kutumia nguvu ya jua, upepo, takataka na hata mawimbi wa bahari. Serikali kwa kushirikiana na *European Union* imefanya utafiti wa kina kabisa wa kujua uwezo wa kutumia nishati hizo na ripoti imetoka hivi karibuni imeonesha kwamba tuna jua la kutosha la kuweza ku- *generate power* kwa kutumia chanzo hicho. Lakini vile vile wanaendelea na utafiti kwa ajili ya nishati ya upepo ambao utafiti huo utaendelea kwa mwaka mmoja zaidi.

Lakini kwa upande wa jua mazungumzo yanafanyika, serikali inaangalia jinsi na namna gani ya kuweza kuwakaribisha wawekezaji ambao wapo tayari kuwekeza katika uzalishaji wa umeme kwa kutumia nishati ya jua. Hili ni muhimu kwa sababu tumeelezwa kwamba *cable* yetu hii tayari inaanza kuzidiwa matumizi. Hivi sasa tunatumia karibu *two-third* ya *capacity* ya hii *sub marine cable* yetu na kwa *speed* hii ya maendeleo na uwekezaji iliyopo ni lazima tuwe na nishati mbadala. Kwa hivyo, hatu- *replace* kusema kwamba hatutotumia umeme wa *TANESCO* hapana, lakini tutakuwa na vyanzo vyengine ambavyo vitaongeza uwezo wetu katika kuwa na nishati bora zaidi, lakini vile vile na nishati ambayo ina bei nafuu.

Mhe. Spika, Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini alizungumzia suala la mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya *MND*, mfumo huu upo chini ya Tume ya Mipango kuna Idara Maalum na ina Mkurugenzi wake. Tayari viashiria vyote kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini vimeandaliwa na ripoti zinatayarishwa, zinatolewa robo mwaka, nusu mwaka na mwaka mzima. Hizi taarifa tulizowaletea muelekeo, mapitio ya hali ya uchumi kwa

mwaka 2017/18 na mapitio ya utekelezaji wa programu za maendeleo ni matokeo ya kazi za idara hii muhimu ya ufuatiliaji na tathmini *(Monitoring and Evaluation). (Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Yussuf Hassan Iddi alitaka kujua programu zilizokuwa hazikuweza kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2017/18 na moja ya programu hizo ambazo tulizipanga ni Programu ya Bandari ya Mpigaduri ambayo kama nilivyokwisha kusema tunaendelea kuzungumza na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu mradi huu. Lakini pia na Mradi wa Umwagiliaji Maji kwa sababu bado uko katika mchakato wa kumpata *contractor* kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu itakayohusika na utekelezaji wa mradi huu. Lakini maelezo ya kina yapo kama nilivyosema katika kitabu cha kwanza cha Mapitio ya Hali ya Uchumi mwaka 2017 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar mwaka 2017/18.

Mhe. Spika, yapo madeni ingawaje sasa hivi siwezi kumpa takwimu, lakini tuna madeni kwa maana ya madeni ya muda mfupi ambayo yale madeni yanakwenda mpaka miezi 12 ambayo yanajumuisha viinua mgongo *(gratuity)*, lakini vile vile madeni ya wazabuni haya yote yanajumuishwa katika madeni ya muda mfupi, lakini tuna madeni ya muda mrefu yale madeni ya *treasury bills.*

Mhe. Spika, jengine alilozungumzia Mhe. Yussuf Hassan Iddi kwa nini gawio la *BoT* limechanganywa na la Mashirika. Kila mwaka huwa tunaweka lengo la kupata gawio la bilioni 4 kutoka *BoT*. Katika mwaka wa fedha 2018/19 bado tumeweka kiwango hicho hicho cha bilioni 4, lakini kimaandishi tumeweka bilioni 9 zikimaanisha kwamba bilioni 4 zinatokana na *BoT* na bilioni 5 zitatokana na *dividend* kutoka kwa mashirika ya serikali. Kwa hiyo, bado ni bilioni 4 na tumeweka bilioni 4 hiyo kwa sababu *BoT* haitengenezi faida kwa maana ya kufanya biashara, haipo pale kwa lengo la kufanya biashara. Lakini hii faida wanayotengeneza inatokana na zile *operation* zao wanazozifanya na wanafanya *operation* nyingi, kwa mfano wanafanya *operation* ya utoaji na usambazaji wa sarafu hiyo ni moja, kunakuwepo na *charge* ambayo inatozwa kwa ajili ya huduma hiyo ya utoaji wa sarafu.

Lakini vile vile riba zinazotozwa kwa benki za biashara, pia huwa wanafanya uwekezaji. Sasa inapotokezea faida na ndio maana unaona lengo letu tumeweka bilioni 4 lakini ikitokea faida kubwa zaidi tunapata zaidi. Ndio maana mwaka uliopita 2017/18 tumepata gawio la bilioni 13. Lakini si busara kuweka lengo kubwa zaidi kwa sababu hawa wafanyabiashara ikitokea kutokana na hizi huduma ambazo zinatolewa ndio faida ile tunaipata. Unaweza ukakuta mwakani isiwe bilioni 13, tunaomba Mwenyezi Mungu watengeneze faida iwe kubwa zaidi lakini msije mkatuuliza tena kwa nini mwakani inakuwa bilioni imeshuka kutoka bilioni 13 ni kwa sababu hizo. Lengo sio lengo la kufanya biashara, kwa hivyo faida sio lengo la *BoT* ni matarajio ya *operation* zao.

Deni za *ZECO* hivi sasa juhudi kubwa sana inafanywa ya kuhakikisha kwamba *ZECO* wanalipa ankara zote zinazopokelewa kila mwezi kwa mujibu wa matumizi, kwa hivyo hakuna malimbikizo zaidi ya madeni. Deni lililobaki kule nyuma ni deni lile lile ambalo tunaendelea kuwasiliana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuona kwamba deni hilo linalipika kwa utaratibu wa kukubaliana juu ya madeni tunayodaiana.

Mhe. Spika, Mhe. Mwanaasha Khamis Juma alizungumza kwa nini tunasema tumefanikiwa katika usajili wa namba binafsi (*private registration numbers*), kwa nini tumefaidika wakati hakuna kodi yoyote iliyokusanywa. Kama anakumbuka Mhe. Mwanaasha wakati nikitoa hotuba yangu mwaka wa fedha mwaka jana na mwaka huu tunaomalizia nao 2017/18 tulizungumzia kwamba serikali haikusudii kwamba kile ni chanzo cha mapato. Kuwa na namba binafsi serikali haipendelei kwa sababu tunataka kuweka usawa wa jamii yote. Tuliweka kiwango kikubwa wakati mwengine unaweka kodi kubwa kuzuia lile jambo lisifanywe. Lakini kwa wale watu wanaotaka kufanya basi walipe katika gharama ambayo inastahiki. Sisi tunasema kwa sababu hakuna aliyejitokeza lile lengo tulililokusudia la kujenga usawa katika jamii yetu umeweza kufanikiwa ndio maana yake.

Mhe. Spika, pia alizungumzia suala la misongamano katika benki yetu, nafikiri kazungumzia suala la kuwa *mobile banking* na *internet banking*, lakini nimeshawahi kulitolea maelezo mengi tu kwamba serikali inajitahidi kuanza kuongeza mfumo wake wa kibenki *(core banking system)* kuupanua zaidi. Lakini kutoa mafunzo ya kutumia *ATM* kwa wananchi ambapo mafunzo yanatolewa kwenye *television* tunayaona *ZBC*. Lakini vile vile masuala ya kutumia *internet banking* na kutumia *M Pesa, Ezy Pesa*, hayo yote yanawasaidia wananchi. Kwa hiyo, taaluma inazidi kutolewa na sio serikali kuwalazimisha lakini wananchi wenyewe kukubali sasa kutumia huduma na teknolojia hii.

Mhe. Spika, suala la *EFD* lilizungumzwa na baadhi Waheshimiwa Wajumbe, niseme tu tupo katika hatua nzuri, lilitakiwa lianze mwaka 2016/17 lakini masuala ya *tender* kwa wakati ule aliyejitokeza ilikuwa ni kampuni moja ikawa haina ushindani na kwa namna hiyo ikabidi sasa tufanye *re-advertisement* ambayo ilifanyika tarehe 22 Novemba, 2017 lilitoka tangazo jengine jipya na kuna kampuni karibu 10 zilionesha nia *expression of interest* ya kushiriki katika kwanza kujenga mfumo. Maana yake kununua zile mashine ni kitu mbali, kujenga ule mfumo wenyewe. Walishiriki na baada ya kufanyiwa tathmini ya kina hizo *expression of interest* kampuni nne (4) zilionekana ndizo zinazo *qualify* sasa kualikwa rasmi kwa ajili ya kuleta *proposal* zao zikiwemo *proposal* za kiufundi (*technical*) na ile ya kifedha (*financial*). Kwa hivyo, sasa wameanza kuleta na tunatarajia hivi karibuni zitafanyiwa tathmini na baada ya hapo ile kampuni itakayoshinda tutaingia nayo mkataba na shughuli hizi za kujenga mfumo kwanza zitaanza na baadae kununua zile *gadget* kwa ajili ya kusambazwa kwa watoa huduma mbali mbali na hasa tutaanza kwa wale watoa huduma wakubwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naamini nimejitahidi kwa kiasi kikubwa sana kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe. Naomba niwashukuru kwa mara nyengine tena, nikushukuru wewe na niwashukuru wajumbe wote kwa kunistahamilia na naomba nitoe hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante sana mtoa hoja Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Waheshimiwa Wajumbe, baada ya majumuisho hayo mazuri kabisa ambayo yametolewa na Mhe. Waziri wa Fedha ametoa hoja na hoja imeungwa mkono. Sasa naomba nichukue nafasi hii kuwahoji wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ya Bajeti wanyanyue mikono, wanaokataa … *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, basi hiyo itoshe kuwa ushahidi kwamba hakuna aliyekataa na waliokubali inavyoonekana wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe, kwanza kabisa nitangulize shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa namna ambavyo amejumuisha hapo, ametoa maelezo ambayo yalikuwa yamekaa vizuri sana na ametumia kama saa moja na dakika kumi kufanya shughuli ya majumuisho. Kwa bahati nzuri tumeshapiga kura kwamba waliokubali wameshinda. Katika orodha yetu tuliyonayo hapa katika shughuli za leo kwenye *order paper* hatuna shughuli inayoendelea. Kwa heshima na taadhima nichukue nafasi hii sasa nitangaze kuwa naakhirisha shughuli za Baraza la Wawakilishi mpaka kesho saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 12:07 jioni Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 27/06/2018 saa 3:00 asubuhi)